**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 29 Juni, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kwa Kuwasilisha Hati. Naomba niwashukuru nyote jinsi tulivyoshirikiana kwa pamoja kuweza kumsindikiza mwenzetu Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, katika safari yake ya mwisho.

Waheshimiwa Wabunge, napenda niwashukuru Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge, lakini pia *TWPG* kwa kushirikiana vizuri sana kuweza kumsindikiza mwenzetu kwa heshima; na kipekee naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atutolee salamu za shukrani kwa Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais alivyokuwa karibu nasi kila dakika kwa mawasiliano hadi hapo jana kule Njombe.

Waheshimiwa Wabunge, narejea tena Mungu ailaze roho ya Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, mahali pema peponi. *Amin.*

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Hifadhi ya Taifa *(TANAPA)* kwa mwaka 2005/2006 (*The Annual Report and Accounts of the Tanzania National Parks for the Year 2005/2006).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 106

**Ubovu wa Barabara za Jiji la Dar es Salaam**

**MHE. MUSSA A. ZUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa sura ya nchi yetu iko katika Jimbo la Ilala; na kwa kuwa barabara nyingi za Jiji la Dar es Salaam ni mbovu sana hali inayosababisha msongamano wa magari na kusababisha maeneo ya Mjini kutopitika kwa urahisi, na hivyo kuleta sura mbaya ya Jijini kwa wageni na wenyeji; na kwa kuwa, sifa kuu ya Mjini ni kuwa na barabara nzuri:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua kero hiyo?

(b) Kwa kuwa, Halmashauri hazina uwezo, kwa nini maeneo ya Upanga, Kariakoo, Jangwani, Gerezani na Ilala yasiboreshwe kwa kiwango cha lami kupitia Mpango wa Zamani wa *JICA?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeliona tatizo la ubovu wa barabara za Jiji la Dar es Salaam hususan eneo la katikati ya Jiji na imeanza kuchukua hatua za kuondoa kero hiyo ili kurahisisha mwenendo wa magari na shughuli za kiuchumi ambazo ziko katikati ya Jiji la Dar es Salaam.

Aidha, kwa kupitia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Serikali imeingia Mkataba na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan *(JICA)* ili kuandaa mpango wa uboreshaji barabara za Jiji na kuanzisha Mfumo wa Sera ya Usafiri Jijini ambapo Shirika hilo litaandaa *Master Plan*. Taarifa ya awali *(Inception Report)* imekwishajadiliwa na wataalam washauri na kwa sasa hivi *study* inaendelea.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli Halmashuri nyingi hazina uwezo wa kuboresha barabara zake kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, Serikali inajitahidi kuongea na Wahisani mbalimbali ili barabara za maeneo ya mijini hususan Dar es Salaam ziweze kuboreshwa kwa kiwango cha lami kama ilivyokuwa kwenye mpango wa uboreshaji barabara wa *JICA*. Sambamba na hilo Serikali pia itaendelea kuzifanyia matengenezo barabara zake zilizo katika hali ya kutengenezeka zikiwemo barabara za Halmashauri ya Manispaa ya Ilala na matengenezo hayo yatategemea na mahitaji kulingana na hali ya mtandao wa barabara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwezo mdogo wa Bajeti ya Maendeleo, Serikali imekuwa ikizihimiza Halmashauri zote nchini kutumia vyanzo vya mapato yao kujenga na kuimarisha miundombinu ikiwemo barabara.

Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ni mojawapo kati ya Halmashauri zilizoanza kutekeleza maelekezo haya ambapo kati ya mwaka 2004/2005 hadi 2006/2007 barabara kadhaa za lami zimejengwa kwenye Kata ya Gerezani, ambapo ni kilomita 1.965,

Jangwani kilomita 1.1, Upanga Magharibi kilomita 0.7, Upanga Mashariki kilomita 1.7, Kipawa kilomita 2.2, Kiwalani kilomita 1.4, Tabata kilomita 1.2, Buguruni kilomita 0.8 na Mchikichini kilomita 0.37, jumla ya fedha zilizotumika ni shilingi bilioni 3.9.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, ningeomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa vile Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo unachangia kodi ya mafuta kwa wingi sana. Je, Serikali sasa iko tayari kuipatia Mfuko Maalum au kuuongezea fedha zinazotolewa kwenye Mfuko wa Barabara wa Dar es Salaam ili barabara zote ziweze kutengenezwa?

La pili, Manispaa ya Ilala tayari imeanzishaanza mikakati ya kuzungumza na wafadhili mbalimbali kuhusu namna ya kutukopesha ili tuweze kutengeneza barabara zetu, na barabara zetu zikiwa nzuri thamani ya nyumba zetu nayo itapanda. Je, Serikali iko tayari kupitia Bunge hili kusaidia Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ili kuweza kukopa kwa kupatiwa *Government Guarantee?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za *Road Toll* ni kweli fedha katika Halmashauri kwa sasa hivi zimeongezwa kwa kiasi kikubwa na nina uhakika kwamba Mkoa wa Dar es Salaam kutokana na mambo ya kiuchumi pamoja na barabara zake kuimarishwa watapewa mgao unaolingana na Mkoa huo na miundombinu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kukopa Serikali inawakopesha wale ambao wanaleta maombi Serikalini. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri wakae katika Vikao vyao waandike barua Serikalini na Serikali iko tayari kuwa-*guarantee* na ipo mifuko mingi ya mikopo.

Kwa mfano hata katika Serikali za Mitaa kuna Mfuko wa Mikopo wa Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, ni jukumu la Halmashauri husika katika kuandika michakato yao na Serikali itakuwa tayari kuwa-*guarantee*.

Na. 107

**Posho ya *Risk Allowance* kwa Madaktari na Manesi**

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa, madaktari na manesi wako hatarini zaidi kuambukizwa magonjwa mbalimbali hasa ambayo hayana tiba kama UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma.

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuwalipa Madaktari na Manesi donge nono kama *Risk Allowance* kwa moyo wao wa kujituma na kuwatibu na kuwahudumia wagonjwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mbunge wa Chakechake, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa madaktari na wauguzi wako karibu na wagonjwa, na ni kweli kuwa kuna uwezekano wa wao kuambukizwa magonjwa kama Kifua Kikuu na UKIMWI wakati wa kuwahudumia. Kwa kuzingatia hali hiyo, Wizara imeweka miongozo ya jinsi ya kutoa huduma kwa wagonjwa wa UKIMWI na Kifua Kikuu na magonjwa mengine ya kuambukiza. Aidha, Wizara hutoa vifaa maalum vya kujikinga na hatari ya kuambukizwa magonjwa hayo (*protective gears*). Ugonjwa wa Kifua Kikuu unaambukizwa kwa urahisi kwa watu walio na lishe duni na kinga hafifu. Hivyo, wauguzi na madaktari sio "*Prone Group*" la maambukizi haya kama walivyo watoto wadogo na waathirika wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa Ukoma kufuatana na biologia ya vimelea vyake ni vigumu kumwambukiza mtu isipokuwa kama kuna mahusiano ya karibu na ya muda mrefu na mgonjwa kama ilivyo kwa mama na mtoto anayepakatwa. Kwa vile wauguzi na madaktari uhusiano wao na wagonjwa huwa ni wa kikazi, siyo rahisi kuambukizwa Ukoma toka kwa mgonjwa. Aidha, Wizara haijawahi kupokea taarifa kutoka mahali popote duniani kuhusu daktari au muuguzi aliyeambukizwa Ukoma kwa kumhudumia mgonjwa.

Mheshimiwa Spika, hapo awali Serikali ilikuwa ikitoa *Risk Allowance* kwa wauguzi na madaktari na watumishi wengine. Baadaye posho zote ikiwemo *Risk Allowance* zilikusanywa na kujumuishwa katika mishahara yao ili kuwaongezea kiwango cha mshahara na kumwongezea kiwango cha mafao wakati anapostaafu. Aidha, Serikali inaendelea kuangalia namna ya kuboresha zaidi maslahi ya watumishi wa umma wakiwemo madaktari na watumishi.

Na. 108

**Uuzaji wa Mahindi ya Wakulima**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO (k.n.y. MHE. FUYA G. KIMBITA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, ni nia ya Serikali kuinua hali za maisha ya wananchi wote kwa kuondoa umaskini; hasa ikizingatiwa kuwa, asilimia kubwa ya Watanzania ni wakulima wadogo wadogo na wa kati:-

(a) Je, kwa nini kumekuwepo na utaratibu wa kufunga au kukataza biashara ya mazao hasa mahindi na nchi jirani hasa ikizingatiwa kuwa, baadhi ya maeneo, wakulima wanajaliwa kuvuna mahindi kwa wingi sana kiasi kwamba, inawawia vigumu kuyahifadhi na kwamba, wakiyauza nje wanapata bei nzuri zaidi?

(b) Je, si kweli hata kama utakuwepo upungufu wa mahindi kwamba, tukiagiza mahindi *in bulk* tunayafikisha hapa nchini kwa bei nafuu kabisa tofauti na ile tunayoweza kuwauzia majirani zetu?

(c) Je, Serikali iko tayari kutoa tamko la kutowazuia wakulima hapa nchini kuuza mazao yao ikiwa ni pamoja na mahindi kwa majirani zetu ili kutowakatisha tamaa kwa nia ya kuongeza kipato na uzalishaji zaidi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kumjibu Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mbunge wa Hai, swali lake lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuzingatia hali ya chakula nchini, ni kweli kuwa wakulima katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu wamekuwa wakivuna mazao ya chakula yakiwemo mahindi kwa wingi na hata kuwa na ziada ya kuweza kuuzwa katika maeneo mengine ndani na nje ya nchi. Serikali imeweka utaratibu wa kusitisha uuzaji wa mazao ya chakula nje ya nchi, wakati baadhi ya maeneo ndani ya nchi yanakuwa hayana chakula.

Kwa mfano, kutokana na baadhi ya maeneo ya nchi kuathiriwa na upungufu wa chakula katika mwaka 2006/2007, katika kipindi cha mwezi Julai, hadi Desemba, 2006 Serikali ilisitisha uuzaji wa mazao ya chakula nje ya nchi.

Hata hivyo, kufuatia tathmini ya hali ya chakula iliyofanywa na Wizara mwezi Novemba, 2006 na kuonyesha dalili za matarajio ya mavuno mazuri ya vuli kutokana na mvua za vuli kunyesha vizuri na mvua za msimu kuanza kunyesha katika wakati wake na kwa viwango kizuri, Serikali iliridhika na hali hiyo na kuruhusu tena biashara ya vyakula nje ya nchi kuanzia mwezi Januari, 2007 hadi sasa. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, si kweli kuwa wakati wote wa upungufu wa chakula mahindi kichele *in bulk* yakiagizwa kwa wingi kutoka nje ya nchi yatafikishwa na kuuzwa nchini kwa bei nafuu ikilinganishwa na yale ambayo wakulima watayauza nchini au nchi jirani kwa bei kubwa. Kwa mfano, mwaka 2003/2004, wakati wa upungufu mkubwa wa chakula , tani 10,000 za mahindi yaliagizwa kutoka nchi ya Kenya, mahindi hayo yalinunuliwa kwa bei ya shilingi 258.23 kwa kilo, na gharama ya kuyasafirisha hadi nchini yalifikia shilingi 384.68 kwa kilo, wakati bei ya wastani ya soko wakati huo ilikuwa shilingi 259.57 kwa kilo.

Uhakika wa wakulima kuwa wakiuza mahindi yao nchi jirani kwa bei kubwa, mahindi yatakayoagizwa kutoka nje yatakuwa ya bei nafuu hapa nchini, unategemea soko lilivyo kwa wakati huo.

(c) Mheshimiwa Spika, serikali haiko tayari kutoa tamko la kudumu la kutozuia au kuzuia uuzaji wa mazao ya chakula nje ya nchi, bali itatoa uamuzi baada ya

kufanya utafiti wa hali ya chakula nchini. Endapo baadhi ya maeneo ya nchi yataonekana kuwa na upungufu wa chakula, Serikali haitaruhusu uuzaji wa mahindi nje ya nchi.

Aidha, endapo hali ya chakula kwa nchi nzima itakuwa ni ya kuridhisha, Serikali itaruhusu uuzaji wa chakula nje ya nchi kwa kiasi ambacho hakitaathiri hali ya chakula nchini.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza kuhusu suala hili.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuongeza *Strategic Reserve* ili hali hii ya kuyumba iweze kupungua?

(b) Je, kuna utaratibu gani wa kuweza kuwa na *price stabilization* ili kuyumba kuweze kupungua?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, naomba urudie swali lako, nimemwangalia Naibu Waziri naona kama hakukusikia vizuri.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, (a) Ilikuwa kwamba je**,** Serikali haioni umuhimu wa kuongeza Akiba ya Chakula *Strategic Reserve* ili kwamba hali hii ya kuyumba yumba iweze kupungua wakati tunapokuwa na mazao ya kutosha na wakati mazao yanapokuwa machache?

(b) Moja, ya sababu inayofanya wananchi wetu wakimbilie kuuza mazao yao nje ni kwa sababu ya bei kupanda na kuteremka. Je, Serikali inafikiria utaratibu gani wa kuwa na *price stabilization mechanism*. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Spika, kwanza sheria ya *SGR* ilianzishwa na Sheria namba 10 ya mwaka 1991. Sheria hii iliruhusu ama kiwango kikubwa kabisa cha kuhifadhi chakula ni tani 150,000. Napenda kusema kwamba tani hizo 150,000 madhumuni yake ilikuwa ni kusaidia wakati matatizo ya chakula yanapotokea katika maeneo mbali mbali nchini kwa muda wa miezi mitatu tu kabla Serikali haijaagiza chakula kutoka nje ya nchi. Kwa hiyo, naweza kusema kwamba tangu *SGR* hii ianzishwe hatujawahi kuhifadhi chakula kinachofikia tani 150,000. Kutokana na kwanza na mahitaji, lakini pili ni kutokana na uwezo kwamba kuhifadhi chakula chenyewe ni gharama kubwa sana, usafirishaji wa vyakula kuvifikisha kwenye yale maghala lakini pamoja na madawa kwa ajili ya kuhifadhia chakula hicho ni aghali sana. Ndiyo maana kiwango hicho hatujawahi kukifikia tangu *SGR* ianzishwe.

Mheshimiwa Spika, katika suala la *price stabilization* tukubaliane kwamba wakati huu ni wakati wa utandawazi na ni wakati wa soko huria. Kwa hiyo, Serikali haiwezi kujiingiza tena katika masuala ya *price stabilization* lazima *supply* na *demand* ndiyo itakuwa ina-*dictate price* inakuwa vipi?

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa suala la maafa na hasa suala la janga la njaa si suala linaloweza kutabirika katika nchi yetu ya Tanzania, wakati mwingine linakuwa kubwa na wakati mwingine linakuwa dogo kutokana na muda hasa tatizo hilo linapojitokeza. Kwa kuwa, basi maafa hayo ndiyo yanayopelekea aidha, Serikali kuwa na Hifadhi kubwa ya Chakula ambacho kitasaidia ama kuwa na hifadhi ndogo ya chakula. Je, Wizara haioni kwamba sasa umefika wakati Sheria hiyo ifanyiwe mabadiliko ili iweze kusaidia kuruhusu hifadhi ya chakula kwa kiasi kinachohitajika ambapo haitaipelekea Serikali kuagiza chakula kingi nje ya nchi na kuwaruhusu wakulima wetu wakapata nafasi ya kuuza mazao yao nje ambapo watasaidiwa kupata fedha za kuweza kuwasaidia katika mahitaji yao ya kila siku na kuondoa umaskini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba Sheria hii ilipitishwa na Bunge na hivyo kama kutakuwa na haja ya kuongeza *Reserve* Bunge hili hili litaletewa waongeza hiyo *Reserve.* Lakini niseme kwamba kuna kitu kinaitwa Utoshelevu wa Chakula. Utoshelevu wa Chakula kusema kwamba chakula kimepungua nchini ama hakijapungua ni kutokana na kwamba tunajumlisha chakula kilichozalishwa msimu huu na kile kilichobaki katika msimu uliopita na kulinganisha na matumizi kwa maana ya binadamu, mifugo, chakula kinachotumika kwa ajili ya mbegu na chakula kinachopotea baada ya mavuno. Utoshelevu wa Chakula unatofautiana mwaka hadi mwaka kutokana na idadi ya watu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mwaka jana 2006/2007 kulikuwa na Makisio ya idadi ya watu milioni 38 na mahitaji yalikuwa ni tani milioni 9.7 za chakula. Mahitaji ya mwaka 2007/2008 yanakadiriwa kwamba yatafikia tani milioni 10,043,000. Kwa sababu tunakadiria kwamba tutakuwa watu milioni 39. Kwa hiyo, kama kutakuwa na haja baada ya kufanya utafiti kwa tafiti zetu ambazo tunazofanya kila mwaka ambazo ziko tano, Januari, Februari, Mei, Agosti, na Novemba basi tunaweza tukafanya mabadiliko ya sheria hiyo. Lakini kama nilivyosema kwamba tangu ianzishwe Sheria ya *SGR* hatujawahi kuhifadhi chakula tani 150,000 kwa sababu ya gharama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, jibu la ziada.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi napenda kutoa pole kwa msiba mkubwa uliotupata Bunge hili na Taifa nzima kwa ujumla. Nakushukuru sana ulivyotuongoza katika mazishi yale.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, nitumie nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana; na nimpongeze Mheshimiwa Jenista Mhagama, muuliza

swali kwa sababu Wilaya yake ni moja ya Wilaya zinazozalisha mahindi mengi sana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ugomvi uliopo hapa siyo kiasi cha chakula ni kwa sababu *SGR* bei yao ni nzuri sana kwa wakulima. Sasa kinachojaribu kutafutwa hapa ni jinsi gani *SGR* itanunua mahindi mengi kuliko inavyopaswa. Lakini labda niliweke wazi kwamba kwenye Sheria ile tumesema *SGR* ni *buyer of last resort* yaani ni mtu wa mwisho katika soko kuingia.

Lakini tatizo la kwamba wakulima hawapati bei nzuri kwa mazao yao tunalielewa, tunalifanyia kazi na tunaangalia uwezekano wa kuanzisha Bodi itakayoshughulikia *serials* kama mahindi na vitu vingine. Nalo tutalizingatia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. Tunahamia Wizara ya Usalama wa Raia sasa. Kabla sijamwita muuliza swali, ninazo salamu hapa kutoka kwa Mheshimiwa Haroub Said Masoud, akimpongeza Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kwa kuvaa shati ambalo rangi yake inapendeza anavyosema yeye mwenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 109

**Hali za Askari Polisi Nchini**

**MHE. MAIDA H. ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jeshi la Polisi ni Idara yenye kazi ngumu sana katika kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Taifa letu; na kwa kuwa, mazingirra ya kazi yao na makazi ni duni sana ikilinganishwa na ukubwa wa majukumu waliyopewa ambapo hata ofisi hazina vifaa vya muhimu kama viti, na kwa kuwa, kati ya Wizara zilizopewa fedha kidogo katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 ni Wizara ya Usalama wa Raia:-

Je, Serikali imeandaa mikakati gani ya uhakika katika kipindi hiki cha mwaka 2007/2008 ili kurekebisha hali hiyo na hivyo kuboresha utendaji kazi na hali za maisha za Askari wa Jeshi hilo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maida Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Askari Polisi wanafanya kazi ngumu na muhimu sana lakini katika mazingira yenye upungufu mkubwa wa vitendea kazi, kutokuwa na makazi bora na ya kutosha, pamoja na maslahi madogo yasiyolingana na umuhimu na unyeti wa majukumu yao.

Wizara ya Usalama wa Raia kupitia Tume ya Rais ya kuboresha mishahara ya watumishi wa Serikali imeshatoa mapendekezo ya mishahara kwa Askari Polisi. Maboresho hayo yakifanyiwa kazi yatapunguza kwa kiasi kikubwa makali ya maisha kwa askari wetu na hivyo kuinua ari ya utendaji kazi na kuongeza ujasiri katika jukumu la kulinda raia na mali zao.

Jeshi la Polisi pia limeanza mpango wa ukarabati wa ofisi zikiwemo za Makao Makuu ya Polisi, Mikoa, Vikosi, na Wilaya ili zilingane na hali ya sasa. Jeshi la Polisi lina mpango wa muda mrefu wa kuboresha hali ya makazi kwa Askari wake. Katika mpango huu kwa kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008 hadi 2009/2010 Jeshi litajenga nyumba za Askari kwa Awamu kulingana na upatikanaji wa fedha toka Serikalini kupitia bajeti ya kila mwaka. Vilevile Serikali ina mpango wa kujenga nyumba za Askari kwa kushirikiana na Taasisi za Fedha hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia *NSSF* wamekubali kujenga maghorofa 30 ambapo maghorofa 25 yatajengwa Dar es Salaam na 5 Zanzibar. Taratibu za kuwezesha mpango huo kuanza zinaendelea vizuri. Aidha, tunaendelea na mauznguzmo na Taasisi nyingine za fedha ili kuona uwezekano wa kujenga maghorofa mengine 30 kwa nia ya kufikia lengo letu la maghorofa 60 kama ilivyokubaliwa hapo awali.

Lengo la mipango hii yote ni kuhakikisha kwamba Askari wote wanaishi katika mazingira bora na katika makambi yao ili kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi mkubwa.

Aidha, nichukue nafasi hii kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kulitumikia Taifa na watu wake kwa uadilifu mkubwa licha ya kuwa katika mazingira magumu ya utendaji kazi wake. Hii ni ishara ya wazi ya uzalendo wa hali ya juu ya viongozi na Askari wa kawaida ndani ya Jeshi la Polisi.

**MHE. MAIDA H. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Pamoja na kuwa Wizara imeandaa na imetoa mapendekezo ya mishahara ya Askari hao. Je, itaangalia vipi kurekebisha suala la ucheleweshaji au kutowalipa posho Askari ambao huwa wanalazimika kutumwa ndani ya nchi na nje ya nchi na wakati Wizara inajua kuwa kazi zingine zinahatarisha maisha yao?

(b) Serikali imesema kwa kushirikiana na Taasisi za Fedha ina mpango wa kujenga maghorofa matano Visiwani Zanzibar. Je, ni maghorofa mangapi yamepangwa kujenga Pemba na tukiangalia kuwa Mkoa wa Kaskazini Pemba zipo nyumba za Askari mbovu ambazo wamezihama hazikaliwi na wapo Askari wengi zaidi wana shida ya makazi ya kuishi na familia ndani ya Mkoa huo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, (a) kuhusu posho, Serikali imejitahidi kutenga posho kila mwaka kwa ajili ya Askari kutekeleza wajibu wao; na ni hivi karibuni tu Serikali imeongeza posho za *ration allowance* kutoka shilingi 28,000 kufikia shilingi 50,000. Lakini hata hivyo, Serikali pia inafanya jitihada kupunguza deni na matatizo mbalimbali ya Askari Polisi.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA**: Hivi karibuni Serikali imelipa shilingi bilioni 5.4 kwa madeni yote ya nyuma ya Askari Polisi. Ni Mkoa mmoja tu uliobakia wa Mtwara na hatua za mwisho zimefikia ili kumaliza madeni hayo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na *nature* ya kazi yenyewe hata ukipanga Bajeti vipi wakati mwingine hujitokeza mambo muhimu ambayo husababisha bado askari waendelee kudai. Kwa hiyo, tunaomba askari wetu waendelee kuwa na moyo wa kuvumilia huku Serikali ikijitahidi kutafuta ufumbuzi wa kutatua kabisa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maghorofa Pemba. Nia ya Serikali ilikuwa ni kujenga maghorofa 60, 50 pale Kurasini na 10 Zanzibar. Lakini kutokana na fedha tulizozipata kwa kuanzia tutajenga maghorofa 30 kama nilivyosema katika jibu langu la msingi. Maghorofa 25, Kurasini na 5 Zanzibar. Tutafanya kila jitihada ili katika maghorofa 5 hayo na Pemba yawemo kwa sababu mpango wa mwanzo ulikuwa tujenge maghorofa 3 Pemba. Kwa mgao huu tutajitahidi kujenga angalau maghorofa 2 Pemba na 3 pale Zanzibar, Ziwani. (*Makofi)*

**MHE. SAVELINA S. MWIGAJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nampongeza Mkuu wa Mkoa wa Kagera kwa kazi anayoifanya kwenye Jeshi hili la Usalama wa Raia. Swali.

Kwa kuwa matatizo ya Jeshi hili la Polisi liko sehemu zote ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuwasaidia Askari wa Mkoa wa Kagera kuliko kutoka Bukoba Mjini kwenda kupatroli Simbaga na Kimisi na kutoka Biharamulo. Lini Serikali itaona umuhimu wa kuwawekea kambi angalau katikati, kambi ya kudumu?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA**: Mheshimiwa Spika, Serikali hivi sasa kupitia Jeshi la Polisi linafanya tathmini ya kuangalia, kujenga vituo vya Polisi na Ofisi za Polisi mbalimbali kwa nchi nzima na mara itakapomalizika tathmini hiyo kwa kufuata vigezo vya Polisi tutajua wapi na wapi tuwe na vituo na wapi tuweke kambi kwa nia ile ile ya kuimarisha ulinzi na usalama. Lakini ushauri wa Mheshimiwa Mbunge tumeuchukua na tutaufanyia kazi ikionekana inafaa kufanya hivyo tutafanya mara moja. *(Makofi)*

Na. 110

**Upekuzi wa Gari za Abiria Katika Vituo vya Polisi – Zanzibar**

**MHE. ALI KHAMIS SEIF** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika baadhi ya Vituo vya Polisi vya Mikoa ya Tanzania Zanzibar ambapo gari ya abiria zinatakiwa zisimamishwe kwa ajili ya kupekuliwa:-

(a) Je, hiyo ni sheria au utaratibu tu?

(b) Kama ni sheria au utaratibu. Je, mbona Mikoa ya Tanzania Bara hali hiyo haionekani?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIS** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Na. 7 ya Mwaka 2004 *(The Criminal Procedure Act, N0. 7/2004*) na Sheria ya Usalama Barabarani Na. 7 ya Mwaka 2003 (*The Road Traffic Act, Na. 7/2003*) pamoja na Sheria ya Jeshi la Polisi (*The Police Force and Auxiliary Services Act, Cap 322 R.E. 2002*) zikisomwa pamoja na *Police General Orders.* Askari Polisi amepewa mamlaka ya kusimamisha na kuipekua gari yoyote kwa madhumuni ya kulinda usalama wa wananchi na mali zao. Anaweza kufanya hivyo kwa kuweka kizuizi (*Road Block*) barabarani au kusimamisha gari hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Sheria kama hizo ziko Tanzania Bara ambapo wanatumia Sheria za Usalama Barabarani ya Na. 30 ya mwaka 1973, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Na. 9 ya Mwaka 1985, Sheria ya Jeshi la Polisi na Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi *(The Police General Orders)* pamoja na maelekezo mengine yatolewayo kila mara na Inspekta Jenerali wa Polisi kwa mujibu wa sheria za nchi kwa madhumuni ya kuimairisha ulinzi wa wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania Visiwani mara nyingi vizuizi hivyo huwekwa kwenye vituo vya Polisi, kwa kuwa vituo vingi vya Polisi huko Zanzibar vipo katika barabara kuu. Kwa upande wa Tanzania Bara vizuizi vinawekwa kwenye eneo lolote la barabara *(Point)* inapoonekana kuna umuhimu kuweka kizuizi hicho. Lengo la kuweka vizuizi ni kuimarisha ulinzi wa wananchi na mali zao.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa vituo hivi viko vya kudumu katika vituo vya Polisi vya Zanzibar. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kuwa utaratibu huu sasa uondolewe?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika suala la msingi kuweka kwetu vizuizi ni kwa nia ya kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

Ningependa kutoa wito kwa wananchi wasione ni usumbufu katika kufanya hivyo ili waone tunashughulikia usalama wao. Kwa hivyo hali ambapo mtakapoona imekuwa ni nzuri ya kuridhisha na ya kutosha hakuna uhalifu nchini hatutokuwa na tatizo la kuondosha vizuizi. Lakini pale ambapo hali inaonyesha kuna wasiwasi lazima tufanye hivyo kwa kulinda raia wetu na mali zao.

Na 111

**Muda Maalum wa Viwango vya Sifa Kwa Mabasi Yaendayo Mikoani**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, usafiri wa mabasi yaendayo Mikoani umekuwa ukisababisha ajali mara kwa mara na kusababisha vifo vya wananchi na kwa kuwa, mabasi yaliyo mengi ni chakavu sana:-

Je, Serikali haioni kwamba, ungewekwa muda maalum wa kuweka viwango vya sifa kwa mabasi yaendayo safari za mbali na kuyaondoa yale mabasi chakavu?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ajali za barabarani zimekuwa zikitokea mara kwa mara ikiwa ni pamoja na ajali za mabasi yaendayo Mikoani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sifa na viwango vya mabasi ya abiria, Wizara ya Miundombinu kupitia *SUMATRA* imeandaa kanuni za viwango vya magari ya abiria ya usafiri wa umma zinazoainisha muundo wa nje, sura ya ndani, nafasi baina ya viti, idadi ya milango, sehemu za dharura na kadhalika. Vile vile katika kanuni hizo, Serikali imependekeza kuwa leseni kwa Mabasi ya abiria ya Mjini na Mkoani zitolewe tu kwa mabasi yaliyo na viwango vya ubora na muda maalum wa kutumika tokea kuundwa kwake.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na mkakati wa Kitaifa wa kudhibiti ajali za barabarani, *SUMATRA* imeteua Mshauri Mwelekezi kufanya utafiti kuhusu ajali za barabarani ikiwa ni pamoja na kujenga mfumo wa kisasa wa kubaini ajali za barabarani na utunzaji wa takwimu za ajali hizo yaani "*Developoment of Road Traffic Accident System and Data Base*". Mapendekezo ya utafiti huu yatasaidia Serikali kubuni njia bora za kupambana na changamoto hii. Utafiti unatarajiwa kukamilika mwisho wa mwezi Julai, 2007.

Mheshimiwa Spika, juhudi za kutoa elimu kwa umma kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu zitaimarishwa ili kujenga mshikamano baina ya Serikali, wananchi na wadau mbalimbali kwa nia ya kujenga uelewa na matumizi bora ya barabara katika kukabiliana na janga la ajali za barabarani

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Jeshi la Polisi linaandaa utaratibu maalum wa vituo vya kukagua ratiba ya mabasi hasa yanayokwenda mikoani ili kuonyesha muda wa kuanza na kumaliza kwa ajili ya ufuatiliaji wa karibu na magari hayo na kuepuka mwendo wa kasi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu inakusudia kuanzisha utaratibu wa ukaguzi wa magari wa lazima (*Mandantory vehicle inspection*) utakaohusisha pia Sekta binafsi ili kuimarisha ukaguzi wa mara kwa mara na hivyo kudhibiti ajali zinazotokana na ubovu wa magari. Aidha, mpango mpya wa utoaji wa leseni za udereva utasaidia kuwa na ubora na sifa za madereva wa mabasi na magari yote kwa ujumla.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niiulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa zamani mabasi yote ya abiria yalikuwa yana milango ya dharura kitu ambacho hivi sasa hakipo, Serikali haioni kwamba hivi sasa umeshafika wakati wa kurudisha utaratibu huo mzuri?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu ya msingi nilieleza kanuni mpya zitakazotumika kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa abiria katika magari mbalimbali ya kuchukua abiria hapa nchini. Moja katika kanuni hizo limo hili suala la kuweka milango ya dharura. Kwa hivyo tumeona kwamba wakati umefika na muda si mrefu Kanuni hizo zitafanya kazi mara tu baada ya kutangazwa na gazeti rasmi la Serikali kwa kutiwa saini na Waziri anayehusika na Miundombinu.

**MHE. TEDDY KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa mabasi haya yana *insurance* ya *third part* mara nyingi. Je, Serikali inaonaje kuwalazimisha mabasi yote ya abiria yafanye *comprehensive insurance* ili inapotokea ajali basi abiria walipwe pamoja na basi lenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie kwamba ushauri wake ni mzuri na tumeupokea na tunashauriana tutazame utaratibu gani unafaa kutumika ili kuhakikisha usalama wa raia na mali zao.

Na. 112

## Stahili za Walimu

**MHE. MARTHA M. MLATA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wamekuwa wakidai stahili zao Serikalini kwa muda mrefu sasa:-

(a) Je, Serikali itawalipa lini fedha/stahili zao?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, kwa kutowalipa Walimu haki zao inazidi kuwafanya wawe wanyonge na kuwakatisha tama?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI(MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mosses Mlata, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wamekuwa wakidai stahili zao za matibabu, gharama za uhamisho, posho za kujikimu na nauli za likizo. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2006 hadi Juni 2007, jumla ya madai ya Walimu wa Shule za Sekondari shilingi 1,974,802,370/= yalipokelewa.

Kati ya hayo, madai ya jumla ya shs. 1,604,813,658/= yalihakikiwa na kulipwa. Jumla ya madai ya shs. 369,983,712/= yalihakikiwa na kulipwa kadri yanavyohakikiwa. Mchanganuo wa malipo ni kama ifuatavyo:-

| MADAI | KIASI KILICHOLIPWA SHS. | BADO SHS. |
|---|---|---|
| Matibabu | 60,218,880/= | 9,659,520/= |
| Uhamisho | 1,199,048,346/= | 250,100,837/= |
| Posho za kujikimu | 162,052,280/= | 110,228,355/= |
| Nauli za likizo | 183,502,125/= | NIL |
| **JUMLA** | **1,604,813,658/=** | **369,988,712/=** |

Kwa upande wa walimu wa Shule za Msingi, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilifanya uhakiki wa madai ya walimu katika Halmashauri zote mwezi Februari, 2007. Madai yaliyohakikiwa na kuwasilishwa Hazina kwa ajili ya kuandaliwa malipo ni kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| Uhamisho | Shs. 5,841,000,000/= |
| Masomo | Shs. 860,000,000/= |
| Likizo | Shs. 691,000,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| Matibabu | Shs. | 524,000,000/= |
| Kujikimu | Shs. | 18,000,000/= |
| Waliofariki | Shs. | 21,500,000/= |
| **JUMLA** | | **Shs. 7,154,000,000/=** |

(b) Mheshimiwa Spika, sambamba na mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika kusajili Shule Mpya, madai ya walimu yataendelea kuwepo kutokana na uteuzi wa Wakuu wa Shule, uhamisho na ajira mpya za walimu. Nia ya Serikali siyo kuwakatisha tamaa walimu na kuwafanya kuwa wanyonge.

Serikali itaendelea kutenga katika bajeti fedha za kulipa stahili za walimu mapema kadri itakavyowezekana. Aidha, Serikali inaziagiza Halmashauri kuzingatia matumizi yaliyotengwa katika Bajeti zao kwa ajili ya posho mbalimbali za walimu. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza. Kwa kuwa inaonyesha kwamba bado kuna deni la kuwalipa hawa walimu stahili zao. Je, Naibu Waziri anaweza kunieleza ni sababu zipi zinazopelekea ucheleweshwaji wa malipo haya?

Swali la pili. Kwa kuwa kuna Kurugenzi nyingi au Halmashauri nyingi ambazo zimekuwa sugu kulipa stahili za walimu hawa. Je, Serikali inatambua hilo na inawachukulia hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, kwanza sababu za ucheleweshaji au stahili za walimu ni nyingi lakini chache ni moja madai kutokuwa na viambatisho stahili, maelezo kutofautiana na viambatisho na mwisho na kubwa ni uhaba wa fedha wakati huo madai yanapoombwa.

Mheshimiwa Spika, sina taarifa kuwepo kwa Halmashauri sugu. Lakini naomba tu nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa Waziri anayehusika na Halmashauri yupo nina hakika atafanyia kazi.

Na. 113

**Kasi ya Ujenzi wa Madarasa na Upatikanaji wa Walimu**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi sasa kila Mkoa unajitahidi kujenga madarasa ya Sekondari kwa ajili ya wanafunzi waliofaulu kuingia Sekondari; na kwa kuwa, madarasa hayo yanahitaji walimu wenye uwezo wa kufundisha Sekondari; na kwa kuwa, ni rahisi kujenga darasa ikishapatikana fedha tu, tofauti na kumwandaa mwalimu:-

(a) Je, ni madarasa mangapi yamejengwa tangu matokeo ya darasa la saba yatolewe?
(b) Je, Serikali ina mipango gani mizuri ya kupata walimu wazuri katika kasi hizo tunazokwenda nazo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, matokeo ya darasa la saba yalipotolewa mwezi Desemba 2006, kulikuwa na madarasa ya kutosha wanafunzi 231,282 tu kati ya wanafunzi 468,279 waliofaulu. Baada ya hapo jumla ya madarasa 4,243 yalijengwa ili kuchukua wanafunzi 169,729 zaidi kati ya wanafunzi 236,992 waliokuwa wamekosa nafasi ya Elimu ya Sekondari. Kwa hiyo, jumla wanafunzi 401,011 sawa na asilimia 85.6 ya waliofaulu darasa la saba wameingia Kidato cha kwanza mwaka huu 2007.

(b) Mheshimiwa Spika, mafanikio makubwa yaliyotokana na ushirikiano kati ya Serikali na wananchi katika kujenga Shule za Sekondari yamesababisha mahitaji makubwa ya walimu. Katika mwaka 2007 ambapo shule mpya 1,084 zimesajiliwa ongezeko la mahitaji ya walimu lilifikia 9,671. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali ilichukua hatua za dharura kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuajiri wataalam 792 wakiwemo wenye Shahada ya Ualimu 471, Wale wenye Shahada isiyo ya Ualimu 206 na Stashahada ya Ualimu 115;

(ii) Kuajiri kwa mkataba walimu wastaafu 250;

(iii) Kuendesha Mafunzo Maalum ya Ualimu ya muda mfupi kwa wahitimu 5,456 wa Kidato cha Sita wenye ufaulu wa *"Principal";* na

*(iv)* *"Pass"* mbili au zaidi na kuwapanga kufundisha katika Shule za Sekondari.

Aidha, walimu 3,170 na Stashahada waliohitimu Februari 2007, waliajiriwa kwa utaratibu wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo za dharura, Serikali inayo mipango mizuri ya kupata walimu wazuri kila mwaka. Mwaka 2008 tunategemea kupata walimu kama ifuatavyo:-

(i) Kutoka katika Vyuo vya Ualimu vya Stashahada walimu 4,500;

(ii) Kutoka katika Vyuo Vikuu:-

- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walimu 600;
- Chuo Kikuu Kishiriki Dar es Salaam walimu 520;
- Chuo Kikuu Kishiriki Mkwawa walimu 870;
- Chuo Kikuu Huria cha Tanzania walimu 214; na
- Chuo Kikuu Tumaini Iringa walimu 29

**JUMLA 6,733**

Hivi sasa Wizara yangu inapitia upya Andiko la Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) ili kuzingatia upanuzi wa Vyuo vya Ualimu viweze kukidhi mahitaji ya sasa ya walimu.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza masuala mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri pia napenda nimwulize kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shule za Sekondari zinahitaji zipate meza, viti, maabara pamoja na mambo mengine muhimu. Je, shule hizi mambo hayo zinayo?

Swali la pili. Je, walimu hao wanaoajiriwa stahili zako ziko vipi kama vile mishahara pamoja na nyumba wanazipata kwa kawaida au wanazipata kwa taabu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa idadi ya shule mpya tulizojenga mwaka huu sio rahisi kwamba vitu vyote vimeweza kupatikana. Tunajua kuna upungufu mkubwa sana wa viti, meza pamoja na maabara katika shule zetu.

Lakini Serikali ya Awamu ya Nne ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, imetenga fedha za kutosha katika Bajeti inayofuata. Ni matarajio kwamba tutazingatia kuhakikisha kwamba tunapata vile vifaa ambavyo vinakosekana katika madarasa hasa madawati, meza pamoja na ujenzi wa maabara na nyumba za walimu. Watanzania wanaendelea kusubiri kwa hamu ili walau waweze kushiriki vizuri katika mpango huu.

Kuhusu suala la stahili za walimu. Ni kweli kama hata suala lililopita Mheshimiwa Naibu Mwantumu Mahiza alikuwa anajibu juu ya stahili za walimu. Serikali itaendelea kutilia mkazo kuhusu suala la malipo ya walimu na kwa walimu hawa watarajali pamoja na walimu wa *Crash Programme*. Mpango uliokuwa umeandaliwa ni kuwapelekea fedha kabla wao hawajafika katika mikoa.

Kumbe wameweza kulipwa mapema wanapofika kuripoti katika mkoa wanapata na fedha zao tayari zimeshaingia katika mkoa ule. Huo ni mpango ambao tumeuona ni mzuri na umepunguza malalamiko mengi sana kwa walimu hasa wapya wanaokwenda kuanza kazi zao.

Na. 114

**Uwiano wa Ng'ombe Wanaozaliwa na Kuchinjwa**

**MHE. RAJAB AHMAD JUMA** aliuliza:

Kwa kuwa, katika hali ya kawaida (kusipokuwa na magonjwa ya wanyama) kiasi kikubwa cha ng'ombe na mbuzi huchingwa kila siku mbali na wale wanaokufa vifo vya kawaida:-

Je, kuna uwiano gani wa kihesabu kati ya ng'ombe wanaozaliwa na wanaochinjwa ndani ya kipindi cha mwezi mmoja?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. CELINA O. KOMBANI) (K.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rajabu Hamad Juma, Mbunge wa Tumbatu kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa idadi ya mifugo inayochinjwa hapa nchini ni kubwa, ambapo wastani wa ng'ombe milioni 2,000,000 na mbuzi na kondoo 2,500,000 huchinjwa kwa mwaka katika machinjio. Uchinjaji mkubwa uko kwenye miji yenye idadi kubwa ya watu kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Tanga, Moshi, Dodoma na Morogoro.

Aidha, ni kweli kwamba upo uwiano kati ya ng'ombe wanaozaliwa na kuchinjwa ambao ndio msingi unaofanya kundi la mifugo kuendelea kuwepo na pia kuongezeka.

Kwa kawaida ng'ombe wanaochinjwa huwa ni madume, maksai, majike tasa ama wale waliozeeka. Aidha, ipo pia mifugo inayokufa mauti ya kawaida kama alivyotanabahisha Mheshimiwa Mbunge na hasa kutokana na magonjwa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vipo vigezo mbalimbali vinavyotumika kupima viwango vya uzalishaji wa mifugo hapa kwetu, viwango vinavyotumika kimahesabu ni pamoja na uwezo wa uzalishaji (*calving rate*) asilimia 40-50; vipindi kati ya mzao mmoja hadi mwingine (*calving interval)* miezi 18 -27; vifo asilimia 10 – 20; uondoaji wa Mifugo *(offtake rate*) asilimia 10 – 20, umri wa kuchinja ng'ombe miaka sita au zaidi. Viwango hivi hutumika kukokotoa idadi ya mifugo iliyotoka na kuongezeka katika kundi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2006/2007 jumla ya ndama 3,083,330 walizaliwa ikichukuliwa kwamba asilimia 10 yaani ndama 308,333 walikufa kutokana na sababu mbalimbali ina maana ng'ombe milioni 2.8 walibakia kwa mwaka sawa na ng'ombe 231,250 kwa mwezi. Kutokana na uwiano nilioutoa hapo juu ng'ombe walioondolewa kwa ajili ya kuchinjwa ni milioni 1.85 kwa mwaka sawa na ng'ombe 154,167 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mahesabu hayo hapo juu uwiano kati ya ng'ombe wanaozaliwa na kuchinjwa unakadiriwa kuwa 3:2. Uwiano huu unaonyesha kwamba kutakuwepo na ongezeko la ng'ombe katika kundi, kwa kuwa kila ng'ombe wawili wanaochinjwa ndama watatu wanazaliwa na kufikia umri wa kuchinjwa.

Mheshimiwa Spika, katika ufugaji wa kisasa na wa kibiashara unaolenga soko, mifugo huchinjwa katika umri mdogo, chini ya miaka minne. Hali hii hufanya uvunaji uwe wa haraka na kufanya ufugaji uwe wenye tija.

Hivyo napenda kutumia fursa hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wenzangu wanaotoka katika majimbo yenye mifugo mingi ya nyama tuendelee na kuhamasisha wafugaji juu ya ufugaji wa kibiashara ikiwa ni pamoja na kuuza mifugo yetu kwa ajili ya kujipatia kipato.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nataka kuungana tena na Wabunge wenzangu kutoa rambirambi zangu kwa familia na marafiki wote wa Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, Mungu aiweke mahali pema peponi. *(Amin)*

Baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Waziri wa Mifugo ningependa kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sasa hivi Tanzania nia yetu ni kuingia katika soko la ulimwengu la kuuza nyama nje ya nchi yetu; na kwa kuwa mpaka sasa hivi suala la pembejeo kwa mfugaji kwa kweli limekuwa duni mno.

Je, Serikali haini umuhimu wa kumpa pembejeo huyu mfugaji kama zifuatazo aina zote za chanjo. Kwa mfano chanjo ya ugonjwa *foot and mouth diseases* ugonjwa wa minyoo, ugonjwa wa mapafu *ECF* na kadhalika. Kwa sababu tukisema mchungaji mmoja mmoja achanje, unachanja wewe lakini unakwenda kupeleka mahali wenzako hawakuchanja kwa hiyo inakuwa kama umefanya kazi bure.

Je, Serikali haioni hili jambo iwafanyie wafugaji angalau nao wajisikie kwamba inawajali?

**WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Spika, Serikali inaipa sekta ya mifugo changamoto kubwa na inaelewa kwamba sekta ya mifugo itachangia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha maisha ya Watanzania. Katika Bajeti ya mwaka jana Serikali imetenga shilingi bilioni 1.50 kwa ajili ya ruzuku ya dawa za kuogeshea mifugo na hiyo ilikuwa mara ya kwanza kwa miaka kadhaa.

Katika mwaka huu pia Serikali imejitahidi kutenga fedha kwa ajili ya ruzuku ya madawa ya mifugo na hasa dawa za majosho. Ninaelewa kwamba kuna magonjwa kadhaa mingine ambayo yanahitajia kupatiwa madawa kwa msaada wa Serikali.

Lakini kufuatana na ufinyu wa Bajeti Serikali kila mwaka inajitahidi kutenga fungu kubwa zaidi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba hasa magonjwa yale ambayo ni magonjwa yanayoitwa *public good* yahakikishwe kwamba yanatibawa kwa huduma ya Serikali nashukuru sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa kufidia muda kidogo wa awali ambapo nilikuwa natoa matangazo nitaruhusu swali la mwisho kwa Wizara ya Miundombinu ambalo anauliza Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, kwa niaba ya Mheshimiwa Charles Keenja.

Na. 115

**Matatizo Yanayoikabili Reli ya Kati**

**MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA (k.n.y. MHE. CHARLES KEENJA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Reli ya Kati ilijengwa na Wakoloni wa Kijerumani zaidi ya karne moja iliyopita kwa utaalam uliokuwepo wakati huo; na kwa kuwa, reli hiyo sasa inakabiliwa na matatizo mengi kiasi kwamba safari za abiria na mizigo zinaanzia Dodoma badala ya Dar es Salaam:-

(a) Je, reli ya Kati na matawi yake ya Mwanza na Mpanda yanakabiliwa na matatizo gani na Serikali imechukua hatua gani za kuyaondoa?

(b) Je, kusafirishwa kwa mizigo mizito kwa barabara kati ya Dodoma na Dar es Salaam hakutasababisha barabara hizo kuharibika mapema kuliko ilivyokusudiwa, na je, Serikali inachukua hatua gani za kufupisha muda wa kutumiwa kwa utaratibu huo?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani za kuhakikisha kwamba, inajengwa reli mpya ya ubora wa Kimataifa na yenye uwezo wa kubeba abiria na mizigo mikubwa na kwa kasi ili ikamilike kabla ya mwaka 2015?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, reli ya *TRC* inajumuisha Dar es Salaam, Tabora, Mwanza, Dar es Salaam, Tabora na Kigoma na matawi yake (Kaliua – Mpanda na Kidatu – Kilosa) inakabiliwa na matatizo yafuatayo:-

Uchakavu wa *Engine* ambapo asilimia 84 ya zile zinazofanya kazi zimepita umri wa kufanya kazi kwa ufanisi, kutokana na maboresho katika teknolojia ya huduma za reli Duniani imekuwa ni vigumu kupata vipuri kwa wakati kwani viwanda vinavyotengeneza vyombo hivyo sasa havipo au vinatengeneza mali ya kisasa zaidi.

Njia ya reli ya kati imechakaa na inahitaji matengenezo makubwa ili iweze kuhimili mahitaji ya sasa ya kiutendaji. Reli nyingi ni za zamani na husababisha kukatika katika au kuvunjika mara kwa mara na kuhatarisha usalama. Uzito wa reli kati ya sehemu mbalimbali za njia ni mdogo nao ni kati ya paundi 45 hadi 56 kwa yadi kwa reli ya Mpanda; na paundi 55 kwa yadi reli ya Manyoni – Singida , paundi 56 hadi 80 kwa yadi reli ya kati na paundi 45 hadi 60 kwa yadi kwa reli ya Tabora Mwanza. Hali hii inapunguza uwezo wa kubeba mizigo kutokana na uwezo mdogo wa kuhimili uzito yaani *(axle load)* unapita juu ya reli.

Mheshimiwa Spika, katika kuyaondoa matatizo hayo, Serikali imeamua kukodisha huduma za uendeshaji wa reli hii kwa lengo la kupata ufanisi. Pia nia ya Serikali ni kuboresha reli hii kwa kuweka reli yenye uzito wa ratili 120 kwa yadi na kutengeneza sehemu korofi. Hivi sasa maeneo korofi yanashughulikiwa kwa kubadilisha reli zenye uzito mdogo na kuweka zenye uzito mkubwa ili ziweze kuhimili ubebaji wa mizigo na kuongeza mwendo. Aidha mwekezaji au mkodishaji huyu atapaswa kuongeza mabehewa na injini ili aweze kukidhi usafiri na usafirishaji abiria.

Mheshimiwa Spika, ni kweli usiofichika kuwa reli imara inahimili ubebaji wa mizigo mizito kuliko barabara. ongezeko la matumizi makubwa ya uchukuzi kwa njia ya barabara yanaathiri sana barabara zetu na hivyo kuzifanya ziharibike kuliko zinavyokusudiwa ndiyo maana katika suala la uendeshaji wa reli yetu msisitizo umewekwa katika kumtaka Mkodishaji arejeshe huduma za reli kuanzia Dar es Salaam kwenda bara kwa kuwekeza katika mabehewa na kurekebisha na kukarabati maeneo fulani ya reli yetu tota ratili 80 kwa yadi hadi ratili 120 kwa yadi.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza sekta ya usafiri wa reli Serikali nayo inayonia ya kujenga Reli kutoka Isaka Kigali. Hivi sasa upembuzi yakinifu unafanyika. Serikali ingependa sana kuongeza njia nyingine za reli, ila tatizo kubwa ni uhaba wa fedha katika programu ya uwekezaji katika sekta ya uchukuzi *(Transport Sector Investment Program*) uendelezaji na uboreshaji wa miundombinu ya reli nchini umewekwa wazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango utakaohakikisha ujenzi wa reli mpya ya ubora wa kimataifa ambayo ujenzi wake utakamilika kabla ya 2015.

**MHE.SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza tunaambiwa katika majibu kwamba asilimia 84 ya *engine* zimechakaa kiasi cha kwamba zimepitwa na wakati; kwanini hakukuwa na mkakati endelevu wa makusudi wa kuzi-*replace engine* hizi kadiri zilivyokuwa zinaendelea kuchakaa mpaka tumejikuta kana kwamba jambo hili limetufikia ghafla tu bila kuelewa?

Swali la pili, katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Serikali inaazima ya kujenga reli kutoka Isaka mpaka Kigali. Nataka kuitahadharisha Serikali na kwa kweli kuishauri Serikali isikurupuke na kuanza kufanya mradi huu na badala yake

iangalie *options* nyingine za kufika Kigari hususan kwa kuanzia Uvinza badala ya kuanzia Isaka. Je, Serikali ipo tayari kupokea ushauri huu?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU**: Mheshimiwa Spika, niseme kwamba si kwamba hatukuwa na mpango wakufanya kazi hiyo. Mkumbuke kwamba zoezi la kubinafsisha reli yetu kwa mpango wa kukodisha umechukua takriban miaka minane sasa na katika kipindi hicho mpango wa kwanza ambao ulikuwa unagharamiwa na Benki ya Dunia pamoja na Nchi za Ulaya hatukuweza kuendelea nao kuutekeleza kwa sababu reli hii ilikuwa *specified* kwa kubinafsishwa na ndiyo maana tumejikuta sasa hatukuweza kuendelea kuwekekeza na hali hii ndiyo imetufikasha hapa tulipo.

Lakini kwa hatua ambayo tumefikia sasa napenda nimwondolee Mheshimiwa Mbunge wasiwasi alionao, tumejipanga vizuri na juzi uongozi wa *RATES Ltd.* ambao utakuja kukabidhiwa reli hii mwezi wa tisa ulikuwa hapa Dodoma, sasa hivi unaelekea Tabora mpaka Kigoma. Lakini wanatupa matumaini sana wanasema wataweza kurekebisha maeneo haya kwa haraka sana.

La pili, hatukurupuki katika hiyo sehemu ya Isaka Kigali, tumejipanga vizuri kwa kushirikiana na Serikali ya Rwanda na ndiyo maana sasa hivi tunafanya upembuzi yakinifu na Mhandisi Mshahuri amepewa kazi hiyo ameanza kazi na tutaangalia njia hizo ambazo sasa hivi tunazo katika mpango wetu lakini katika mpango wa *central corridor* ambao tunashirikiana na Benki ya Dunia pamoja na Afrika ya Kusini. Ushauri ambao Mheshimiwa Mbunge ameutoa na sisi tunao tunapoangalia *alternative routes*. Kwa hiyo, tatakapofika katika hatua ya mwisho tutakuwa na taarifa zote kwa Mhandisi Mshauri ambaye anafanya sasa hivi na kwa wale ambao tunataka tuwapatie kazi hiyo katika maeneo mengine. Kwa hiyo, tunamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ushauri wake na sisi tuna mawazo mapana zaidi katika kushughulikia na kuimarisha Reli ya Kati katika muono mpana zaidi wa sasa na hapo baadaye.(*Makofi*)

**SPIKA:** Na-*declare interest* nadhani ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ni mzuri kwa sababu haionekani kuwa ni kwa faida ya nchi kuwa na reli *parallel* ambayo hatimaye itakuwa inafika palepale Tabora.

Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na kama kawaida tunayo matangazo na nitaanza na wageni. Kwa furaha kubwa kwa niaba yenu naomba niwatambulishe Waheshimiwa Wabunge kutoka Nchi jirani ya Jamhuri ya Kenya ambao wametutembelea hapa na niwaambie tu Waheshimiwa wageni wetu kwamba hapa tuna utamaduni wa kutambulisha Waheshimiwa kama ninyi mmoja mmoja. Kwa hiyo nitaomba niwatamke kwa majina ili Waheshimiwa Wabunge waweze kukutambueni mmoja baabda ya mwingine. Wakwanza ni Mheshimiwa Mhandisi Kalyue Mruiki, anafuatia Mhandisi Eric Nyamunga, anafuatiwa Mheshimiwa Profesa Christine Mangu, hawa jirani zetu wanasoma sana ni kama sisi tunao *PHD Holders* humu ndani.*(Makofi/Kicheko*)

Baada ya huyo anafuatiwa Mheshimiwa Charles Kilonzo, anafuatiwa na Mheshimiwa Mohammed Yussuf Haji huyu bila shaka ni kutoka Mombasa ama

Kaskazini Mashariki, anafuatiwa na Mheshimiwa Sammy Koech, na Mheshimiwa Steven Manoti. Wale pale. Wamefuatana na Maafisa wa Bunge la Kenya, atakuwa Bwana Mohammed Ali Mohammed na Bibi Mary Waruingi na Afisa Ubalozi wa Kenya Bwana Fred Lesudi. Karibuni sana jirani zetu tunafurahi sana tunapoikutana namna hii na ni jambo ambalo linazidi kuimrisha Ushirikiano wa Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Magreth Mkanga, anao wageni wake ambao ni Viongozi wa Chama cha Viziwi Taifa, sasa sijui kuna mtu karibu wa kuwasaidia wasimame, maana yake hawawezi kunisikia.

Mheshimiwa Mlawa ni Mwenyekiti, wamesimama wote ila Ndugu S. Mloo mweka Hazina, Rupi Maswanya Idara ya Wanawake, Dr. Mzale ni Mshauri, Octavian Msimba, Mkalimani Alika Ali Salim kutoka Koani Zanzibar na Ibrahim Mlosi Mkalimani. Karibuni sana tunafurajhi kuwa nanyi.

Naomba pia nimtambulishe Ndugu Thomas Ngawaiya aliwahi kuwa Mbunge hapa na ameambatana na Mkewe Mama Ngawaiya yule pale. Lakini mkewe simwoni naam amesimama Mama Ngawaiya nilidhani mngesimama pamoja wale pale Bwana na Bibi Ngawaiya karibuni sana. Sijui utagombea Jimbo gani lakini sasa hiyo itakuwa ni tishio kwa mmoja wetu hapa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Paul Lwanji, ameniomba niwatambulishe wageni wake ambaye ni Mkewe Mama Lilian Lwanji na watoto wao watatu Sechele, Diana na Lucy, wale pale karibuni sana. Mheshimiwa Lwanji anabahati ya kuzaa watoto wa kike tu. Kwa hiyo wale ambao wamebahatika kuzaa wavulana basi wachangamke changamke hapa.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu Semina, Jumamosi, kesho, kutakuwa na Semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote Semina hii ni ya *Unit Trust of Tanzania* na mada inahusu *Investment Life Unit Trust scheme.* Ni muhimu sana sana mambo haya kutazama akiba ya baadaye. Semina itaanza saa tatu asubuhi kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii Jenista Mhagama anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, mkutane leo tarehe 29 Saa saba Mchana Ukumbi namba 227. Mheshimiwa Job Ndugai Mwenyekiti wa Maliasili na Mazingira anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Maliasili na Mazingira mkutane leo ukumbi namba 231, itakuwa ni Saa Tano Asubuhi.

Mheshimiwa Abdallah O. Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi wakutane leo Saa Tano Asubuhi chumba namba 428. Mheshimiwa Mwenyekiti Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi anaomba leo Saa tano Asubuhi ukumbi namba 432.

## KAULI YA MAWAZIRI

### Tuhuma kuhusu Kampuni ya Meremeta na Mke wa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (*BOT)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tarehe 24 Juni, 2007 wakati akiwasilisha maoni ya kambi ya upinzani kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa Mbunge wa Karatu, alitoa tuhuma nzito, inayomhusu Gavana wa Benki Kuu. Taarifa yake haikushia kwa Gavana wa Benki Kuu tu, bali iliendelea kumtaja pia Mkewe wa Gavana na kumhusisha na kampuni ya *Time Mining* kuwa ni mmoja wa Wakurugenzi wa Kampuni hiyo, na alidai pia kwamba Kampuni ya Meremeta imeuzwa kwa kampuni ya *Run Gold* ambako mke wa Gavana anamiliki hisa.

Mheshimiwa Spika, napenda kunukuu sehemu ya hotuba yake kama ifuatavyo: "Taarifa niliyoitoa Bungeni kuhusu tuhuma inayomhusu Gavana wa Benki Kuu inamhusisha Gavana moja kwa moja au kwa uzembe katika upotevu au matumizi mabaya ya fedha za Serikali ndani ya Benki.

Taarifa hizo haziishi hapo, zinamtaja mkewe Anna Mganda kuwa mmoja wa Wakurugenzi wa Kampuni ya *Time Mining* ambayo ndiyo iliyokuwa inaendesha Kampuni ya Madini ya Meremeta na hatimaye imeuzwa kwa bei ya kutupa na baada ya *BOT* kulipa dhamana iliyoweka na Benki Kuu *Run Gold* ambako Ana Mganda mke wa Gavana pia ni mwenye hisa.' mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imesikitishwa na taarifa hiyo potofu ya Dr. Slaa, ambayo haina ukweli wowote na yenye lengo la kupotosha umma kuhusu Kampuni ya Meremeta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Meremeta ni Kampuni iliyoanzishwa mwaka 1997 kwa madhumuni ya kununua dhahabu isiyosafishwa kutoka kwa wachimbaji wadogo wadogo. Shughuli zake nyingi zilikuwa katika eneo la Ukanda wa Ziwa Victoria. Wamiliki wa kampuni hiyo ya Meremeta ilikuwa ni Serikali na Kampuni *TRENEX PTY LTD* kila mmoja akiwa na umiliki wa asilimia 50 ya hisa katika Meremeta.

Kwa mujibu wa makubaliano ya wanahisa, afisa mtenda mkuu wa Meremeta alikuwa anateuliwa na *TRENEX* na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Meremeta aliteuliwa na Serikali. Hivyo tangu kuanzishwa kwake Meremeta ilikuwa na uongozi wake.

Kampuni ya Meremeta ilitarajiwa kuwa na uwezo wa kununua dhahabu inayofikia kilo 300 kwa mwezi, hata hivyo, lengo hilo halikuweza kufikiwa kwa sababu mbali mbali kutokana na vifaa duni vilivyotumiwa na wachimbaji wadogo. Kutokana na hali hiyo, kampuni iliweza kununua kilo 40 tu kwa mwezi. Aidha, ushindani wa kibiashara kati ya Meremeta na wanunuzi binafsi wa dhahabu, vilevile ulichangia Kampuni ya Meremeta kushindwa kufikia lengo lililotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na ushindani wa kibiashara, mwaka 2000 Meremeta iliamua kuingia katika uchimbaji mkubwa wa dhahabu kwa kuanzisha mgodi

wa Buhemba, badala ya kutegemea kununua dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo wadogo tu.

Baada ya kuchukua uamuzi huo Kampuni ya Meremeta ilianza kukabiliwa na matatizo ya kifedha na ya kiutendaji iliyosababisha kuchelewa kukamilisha kwa mgodi wa Buhemba, na hivyo kuilazimu Serikali kuingilia kati ili kukamilisha mgodi huo. Mgodi wa dhahabu Buhemba upo na unaendelea kufanya kazi japo kwa kiwango kisichoridhisha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matatizo yaliyoendelea kuikabili Kampuni ya Meremeta, Serikali iliunda kikosi kazi yaani *task force* mwaka 2003 ili kuchambua matatizo ya Meremeta na kupendekeza hatua za kuchukua ili kunusuru mgodi wa Buhemba. Kikosi kazi kilikamilisha kazi yake na kutoa mapendekezo Serikalini kwa maamuzi, miongoni mwa mapendekezo ya msingi yaliyokuwa kubaliwa na Serikali yalikuwa:-

1. Kusitisha shughuli za Meremeta za kununua dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo wadogo.

2. Kuanzishwa kwa Kampuni mpya itakayomilikiwa asilimia 1 na Serikali jukumu la msingi ya kampuni hiyo mpya likiwa ni kusimamia na kuendesha mgodi wa Buhemba na kujishughulisha na utafutaji wa madini wa dhahabu kwa kuingia ubia na makampuni yenye mtaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kuwa Kampuni ya Meremeta haijawahi hata siku moja kuendeshwa na *Time Mining* kama anavyodai Mheshimiwa Dr. Slaa. (*Makofi*)

Madai yake Dr. Slaa, ni ya kubuni na hayana hata chembe moja ya ukweli. Katika Taarifa yake Mheshimiwa Dr. Slaa hakuishia hapo, anadai kuwa Mke wa Gavana wa Benki Kuu ni mmoja wa Wakurugenzi wa Kampuni ya *Time Mining* na kwamba kampuni ya Meremeta imeuzwa kwa bei ya kutupa kwa kampuni ya *Run Gold* ambako eti mke wa Gavana wa Benki Kuu pia ni mwenye hisa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kukanusha kauli hizi kwamba kampuni ya Meremeta imeuzwa kwa *Run Gold,* Kampuni ya Meremeta haijauzwa kwa mtu yoyote au kwa kampuni yoyote iwe kwa bei ya kutupwa au kwa bei ya kuruka. (*Makofi*)

Kama nilivyoeleza hivi pundi, Meremeta ilisitisha shughuli zake kwa mujibu wa sheria, kutokana na hatua hiyo mali na madeni ya Meremeta yamehamishiwa kwenye kampuni mpya *Time Gold* ambayo inamilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja. Mali hizo zinajumuisha pia migodi ya dhahabu ya Buhemba.

Mheshimiwa Spika, si kweli kuwa Mke wa Gavana wa Benki Kuu ni Mkurugenzi katika Kampuni ya *Time Mining* kama anavyodai Mheshimiwa Dr. Slaa, kampuni ya *Time Mining* ina mkataba na Serikali wa kuendesha mgodi wa Buhemba, kwa mujibu wa

Mkataba huo, *Time Mining* inawajibika kuipa Serikali orodha ya Wakurugenzi wa Kampuni hiyo.

Orodha ya sasa ya Wakurugenzi wa *Time Mining* ambayo Serikali inayo na ambayo kwa mujibu wa sheria ya kampuni lazima ionyeshe katika nyaraka zote za kampuni haina jina la mke wa Gavana wa Benki Kuu kama mmoja wa Wakurugenzi wa Kamapuni hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wakurugenzi wa *Time Mining* ni hawa wafuatao:- Kwanza Bwana Peti Visige, ambaye ni *Chief Executive Officer* na Wakurugenzi wengine wanne wafuatao:- Bwana Walter Louis, Bwana Tamag Mkoma, Bwana Simisan Kupe na Bwana Louis Vandawhat na mwisho Bwana Remmy Van Chapaverot. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, unaweza kuona katika *list* ya wakurugenzi wa Kampuni ya *Time Mining* ambao wako sita hamna jina la mke wa Mheshimiwa Gavana.

Kama nilivyosema madai ya Mheshimiwa Dr. Slaa kuwa kampuni ya Meremeta imeuzwa kwa kampuni ya *Run Gold* ni uzushi mtupu hamna ushahidi wowote na kusema kweli yanapaswa kukemewa kwa heshima zote zinazostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *Run Gold Resource Tanzania LTD* ina mkataba wa ubia na Serikali kupitia Kampuni ya *Time Gold* wa kutafuta madini ya dhahabu hapa nchi nje ya eneo la mgodi wa Buhemba.

Mheshimiwa Spika, hata kama madai ya Mheshimiwa Dr. Slaa, mke wa Gavana wa Benki Kuu anamiliki hisa katika Kampuni ya *Run Gold* yangekuwa ni ya kweli, madai hayo hayangeinyima Serikali usingizi, kwa sababu kampuni ya Meremeta haijauzwa kwa *Run Gold* na wala Serikali haina mkataba wowote na *Run Gold* ama wakala wa *Run Gold* wa kuwauzia mgodi wa dhahabu wa Buhemba.

Mheshimiwa Spika, haupo ubishi kuwa tuhuma zilizotolewa na Mheshimiwa Dr. Slaa ni tuhuma nzito na ambazo kwa bahati mbaya kinyume na taratibu zimeelekezwa kwa watu binafsi na kwa majina.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyodhihirishwa na kauli hii, tuhuma alizozitoa Mheshimiwa Dr. Slaa hazina ukweli wowote na wala haukutolewa ushahidi wowote wa kuzithibitisha.

Hali hii ikifumbiwa macho, ipo hatari ya kuligeuza Bunge lako Tukufu kuwa uwanja wa kuwakashifu watu wasio na hatia wala fursa. Mheshimiwa Spika, nitarudia, hali hii ikifumbiwa macho, iko hatari ya kuligeuza Bunge lako Tukufu kuwa uwanja wa kuwakashifu watu wasio na hatia wala fursa ya kujitetea mbele ya Bunge lako Tukufu. Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha! *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante kwa taarifa hiyo!

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008 - Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, bado ninao wachangiaji 28, lakini ni dhahiri leo itabidi tumalize kwa sababu kazi ya kupitisha Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ni ndefu kidogo kutokana na kuwa na Mawaziri wawili, Naibu na Mwisho Mtoa Hoja. Kwa hiyo, nilikuwa naona mpaka tena na kuingia kwenye vifungu, Jumatatu baada ya maswali, pengine twende moja kwa moja kwenye hatua hiyo ili tujiridhishe. Bora tuwahi kuliko kuwa katika hali ambayo tutahitaji pengine tuongeze muda.

Kwa hiyo, kama nilivyosema ninao wachangiaji 28, na nimepata maombi mengine, wengine wanataka watangulie, wengine wasiseme sasa na waseme baadaye. Mara nyingine mtaona kama ninaruka jina, ni kwa sababu nimeruka makusudi, ni kwa sababu tu nimepata maombi hapa mezani na siyo rahisi kueleza udhuru wa kila mmoja.

Kwa hiyo, kwa mfano kwa sasa naliacha jina la Mheshimiwa Kabwe Zitto ambaye yumo humu humu, ambaye ndiye wa kwanza kwa sababu maalum alizoniandikia na tutaanza na Mheshimiwa Mariam Kasembe, akifuatiwa na Mheshimiwa Haroub Masoud, wakati huo huo Mheshimiwa Ezekiel Maige ajiandae.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Mheshimiwa Hafidh, Mwongozo! Kanuni namba ngapi?

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, Kanuni 50(1). Kwa maelezo yaliyotolewa na Serikali hivi punde, nilikuwa nategemea kupata Mwongozo wa Spika kuhusu hizi tuhuma na nilikuwa nasubiri Mheshimiwa Spika, labda atatoa chochote kuhusiana na tuhuma hizi ambazo zimekanushwa rasmi na Serikali.

Lakini, naona hakuna chochote kilichotoka katika Kiti! Mheshimiwa Spika, hivi haya ndiyo yamekwisha bure hivi hivi? Kwa sababu utakuwa ndio mtindo huu, watu kuingia katika Bunge na kusema maneno au shutuma ambazo si za kweli. Sasa, Bunge hili linachukua hatua gani katika suala kama hili? Naomba Mwongozo wako!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya Kauli ya Waziri, huwa hakuna ulazima kwa Spika kusema kitu chochote. Na la pili, majibu yanatusaidia, lakini pia kuna hatari nyingine. Spika hawezi kuzuia Waheshimiwa Wabunge kusema yale wanayopenda kusema. Kwa sababu, leo hii hili limeonekana pengine si la kweli, lakini inawezekana mengine yatakayosemwa yawe ni ya kweli na hatuwezi kujua mpaka tusikie yamesemwa na tumesikia majibu yake. Kwa hiyo, suala hili mimi nalimalizia hapo. Ahsante sana! *(Makofi)*

Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mariam Kasembe hayupo, kwa hiyo sasa namwita Mheshimiwa Haroub Masoud.

**MHE. HAROUB SAID. MASOUD:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi kukushukuru wewe kunipatia nafasi hii ya kwanza asubuhi hii kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Lakini, kabla ya kwenda huko, natoa rambi rambi kwa kifo cha Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, kilichotokea juzi.

**SPIKA:** Waheshimiwa, tutoke kwa utulivu tafadhali, ili mwenzetu aweze kusikika!

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, alikuwa yupo katika Kamati ya Maendeleo ya Jamii, ambapo mimi binafsi ni Makamu Mwenyekiti. Alisaidia sana Kamati yetu, alikuwa mtu mcheshi, alikuwa mtu mvumilivu, alikuwa vile vile mtu mpenda watu. Kwa hali hiyo, namwombea dua, Mwenyezi Mungu amjalie alale pahala pema peponi, amin.

Mheshimiwa Spika, binadamu tuna tabia ya kusahamu. Kwa hiyo, naogopa nisije nikasahau kuunga mkono hotuba hii kwa kuendelea tu kuchangia. Kwa hiyo, nitamke rasmi kwamba naiunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wengi wamesema mengi, wameibugudhi, wameisema, lakini nasema kwamba: Si wengi ambao wanaamini na wanakubali kwamba wenzao wanafanya mazuri. Nitatoa mfano mdogo tu kabisa. Mheshimiwa Spika, Mtaani kwangu kulikuwa na wanawake wawili, Amina na Hawa, hawa walikuwa wake wenza. Lakini, baada ya kukaa muda mrefu, Amina alifariki, akabakia Hawa. Miaka kumi baadaye, huyu Hawa alitembelea maeneo ambayo Amina alizikwa, akaenda kutembelea makaburi bila kujua kwamba mke mwenzake alizikwa pale. Alitembelea makaburi, kalikuta kaburi moja linang'ara na zuri kabisa, akawaambia wale wenzake aliofuatana nao: "Huyu aliyelazwa hapa, nina hakika ni mtu wa peponi", akamwombea dua. Lakini alipokuja kuuliza kaburi hili ni la nani, kaambiwa ni Amina, akasema: "Hamad ndio maana ati limepasuka pale, mtu wa motoni huyu".

Mheshimiwa Spika, sasa, mtu yeyote anayetaka kukubughudhi, hachagui tusi la kukuambia. Kalisifu kwanza kaburi, lakini baadaye alipoambiwa la fulani, amesema mtu wa motoni. Sasa, si ajabu wenzetu wakabughudhi hotuba hii ya Waziri Mkuu na wakabughudhi kazi zote za Serikali ambazo zimefanywa katika Awamu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakwenda katika Mfuko wa Wajasiriamali, shilingi bilioni 21. Tumeambiwa na Waziri Mkuu hapa kwamba hadi tarehe 31 Mei, 2007, *CRDB* walitoa mikopo wananchi 6,765 sawa na bilioni 6.3. *NMB* nao wametoa kwa Wajariamali 15,024, sawa na bilioni 11.6. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni hatua kubwa. Asiyeona na asione, lakini hii ni dhahiri kwamba Serikali imepiga hatua kubwa sana. Lakini, sasa nataka kutoa angalizo, naamini Waziri Mkuu atafuatilia. Wanaopewa mikopo hii wengi wao ni watu maskini, kina mama

na vijana. Lakini, mambo ambayo nimeyashughudia mimi mwenyewe katika Jiji la Dar es salaam, inasikitisha! Wanapata mikopo ya Serikali na *Pride*, lakini Askari wa Jiji wamekuwa majeuri, wanatumia mabavu, hawatumii sheria katika angalau kuwaondosha kwa utaratibu hawa Mamalishe na Vijana wanaouza vitu mitaani. Mfano: Tulipokuwa katika Kamati, asubuhi moja alikuja Mheshimiwa Amer ambaye ni Mjumbe wa Kamati, analia machozi kwa sababu ameona kina mama wamepigwa marungu asubuhi kwa kuuza uji na maharagwe. Wamesukumwa, wameanguka, vyakula vyao vimemwagwa. Sasa, ninasema huu ni utawala bora? Kama ni hivyo, mimi nadhani Askari wa Jiji lazima wawajibishwe na waelezwe taratibu ambazo zinafaa kwa ajili ya kufanya kazi hiyo, kwa sababu kama tutaendelea hivyo, mikopo hii yote itapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, nilichoshughudia mimi mwenyewe binafsi, ninateremka Hotelini nasubiri gari ije kunichukua asubuhi, wauza kahawa nao wanafukuzwa kwa marungu na kahawa zao. Kahawa zao zimemwagika, vikombe vimevunjika. Sasa, mikopo hii itarejeshewa wapi? Mheshimiwa Spika, ninamwomba Sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, yeye ndiye Mkuu wa Serikali, ndiye Msimamizi Mkuu. Labda watu wa Jiji hawafahamu uwezo wao ni nini na wajibu wao ni nini.

Mheshimiwa Spika, sasa nitakwenda katika, upotevu wa pesa katika Serikali Kuu. Tunapozungumzia upotevu, watu wengi tuna dhana kuwa upotevu wote unafanywa na Wizara ya Fedha kwa jumla. Lakini, ukiangalia *Report* za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, upotevu huu umefanywa katika kila Wizara, Wizara nyingi sana. Mimi ninaamini Wizara ya fedha imefanya kazi yake nzuri, inasimamia kukusanya mapato na sisi tumepongeza sana na tunapongeza tena kwamba michango inayotolewa na Wizara ya Fedha ni ya umuhimu kubwa na lazima Wizara zote ziienzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini inasikitisha, kwa sababu Makatibu Wakuu ndio dhamana wa matumizi yote ndani ya Wizara zao, hawawajali Mawaziri wetu waaminifu, hawawajali viongozi wa juu, baadhi yao wanafanya mambo ambayo yanadhalilisha Serikali yetu. Mheshimiwa Spika, lazima sasa kwa maoni yangu, taratibu ya mambo ya mahesabu ndani ya Wizara zirekebishwe ili kumpa angalau mpini Waziri naye awe ana sauti.

Mheshimiwa Spika, kwa sheria za sasa hivi za matumizi, Mheshimiwa Waziri kakaa pale kama *figure* kwa sababu Katibu Mkuu ndiye *answerable* wa mwisho mwenye kuidhinisha hiki kitolewa na hiki kisitolewe.

Lakini vile vile upotevu mkubwa unatokea katika manunuzi. Baadhi ya Wahasibu wetu wa Wizara, baadhi ya Makatibu wetu matumizi yao yako ovyo kabisa, hayakubaliki na ukweli ndio upotevu wote uko huko. Lakini, lingine kama hilo halitoshi, marupurupu *(Imprest),* ni jambo ambalo linaloeleweka wazi kwamba yeyote anayekabidhiwa pesa kama ni *Imprest* kwa sheria zetu ambazo tunazo sasa, hatakiwi kupewa tena kama hajarejesha marejesho yake.

Lakini, tunaendelea, tunaendelea, tunaendelea! Lakini, kama hilo si kubwa, tunakubali Mawaziri wetu, Manaibu Waziri wanunuliwe magari ya *VX*, lakini cha

kusikitisha sana utakuta mpaka Wakurugenzi wa kawaida, magari yaliyokuwa yamo ndani ya *Pool* ya Wizara zetu ni *VX*. Kuna haja gani hiyo?

Mheshimiwa Spika, ninasema haya kwa sababu Kamati yetu chini ya Mwenyekiti wangu mahiri, Mheshimiwa Mama Mhagama, tulifanyiwa Semina ndogo Dar es salaam. Lakini aliyetoa mada ni mfanyakazi wa Wizara ya Fedha ambaye ni Mkurugenzi. Alituambia: “Ninyi Wabunge hamtusaidii sisi Wizara ya Fedha, mamilioni yatazidi kuendelea kupotea”. Sitaki kumtaja hapa maana asije akaandamwa! Akasema: “Yataendelea kupotea”. Anasema: “Kuna haja gani kama mimi ninunuliwe gari la VX na Wizara yangu, tununuliwe gari ambazo zinalingana na vyeo vyetu”.

Mheshimiwa Spika, sasa, hilo lakini linapita. Ukiangalia hapa Dodoma sasa hivi, Maafisa wa kawaida tu wanatembea na *VX*. Mamilioni na mamilioni ya pesa yanapotea.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiria kwamba tutakaporekebisha sheria za matumizi ndani ya Wizara, tukampa uwezo Waziri kila miezi mitatu a-*check* mahesabu yake, mimi nadhani haya yataondoka na kelele zitapungua.

Mheshimiwa Spika, zabuni vile vile: Zabuni zetu ni mbaya kabisa. Kweli zinafanywa hadharani, lakini upendeleo uko na mapotevu mengi ya pesa yanakuja katika hayo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha hapa, mara nyingi anasema anataka kuwasomesha Wahasibu. Mimi maoni yangu ni tofauti na hayo. Utakapomsomesha sana Mhasibu, ndiyo atakavyoiba zaidi, ni kweli! Yule mtu ambaye elimu yake ni ndogo, hana ujuzi wa kughushi *cheque* na kuiba kuliko yule aliyesoma.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano kidogo tu kabisa. Uamimifu hauna chuo, uaminifu ni roho yako mwenyewe binaadamu, mfano nitakupa.

Kuna mwimbaji mzuri sana anaitwa Ally Kibba, amemwimbia mdogo wake waliozaliwa tumbo moja, akamwimbia wimbo anamwambia: “Leo umekuwa shababi unaninyang’anya mchumba wangu!” Wamezaliwa tumbo moja! Huo ni ushahidi tosha kwamba uaminifu hauna chuo.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia hali ya uchumi ya Zanzibar. Wenzangu wengi wamezungumza. Lakini, siongei hayo kwa sababu wameishasema wenzangu, lakini nasema wafanyabishara ndogo ndogo wanaotoka Zanzibar kuja Dar es salaam wamepungua kwa sababu adhabu wanayoipata katika Bandari ya Dar es salaam, wanapekuliwa, wanatozwa ushuru, hatujui ushuru wa nini! Zamani tuliambiwa Zanzibar *route*, sijui nini na nini na kadhalika.

Wengi wameomba kwamba Waziri nimchukue Mkoani kwangu, Jimboni kwangu, mimi nasema nawaomba wawili tu Waziri wa Fedha niende naye Unguja pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Abdisalaam. Tukitoka Zanzibar, tutaingia ndani ya Boti pamoja, lakini ili asijulikane pale Bandarini Dar es salaam, Mheshimiwa Zakia Meghji,

Waziri wa Fedha tutamvisha baibui. Mheshimiwa Abdisalaam kwa sababu yeye si mvaaji wa kilemba, tutamvisha kanzu na kilemba na mimi nitakuwemo.

Tutachukua maboksi, tutatia vitu vya ovyo ovyo tutizame kwa sababu watakuwa hawamjui Waziri wao, hawamjui Naibu wao, watakavyopekuliwa watu na wale wengine ambao watakuwa wamechukua bidhaa zao ndogo ndogo, watakavyoadhibiwa pale. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atashuhudia mwenyewe, atajua kwamba watu wake wana adha.

Mheshimiwa Spika, lingine nazungumzia kuhusu nyumba ya Mwalimu Nyerere. Mheshimiwa Spika, nimesikia taarifa ambazo sijazithibitisha, nyumba iliyopo Magomeni. Wenzetu wa nchi zote hata Zanzibar, Marehemu Karume alipofariki, kijiji chake kiko jirani yangu mimi, kulikuwa hakuna nyumba.

Lakini, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kumthamini Kiongozi wao Mkuu walijenga nyumba pale ikawa kama ni nyumba ya historia. Sasa leo nimeshitushwa kusikia nyumba ya Mwalimu Nyerere iliyokuwa Magomeni ambayo watoto wote wamezaliwa pale, inataka kubomolewa, eti, linataka kujengwa jumba kubwa la kisasa la *National Housing* nadhani.

Mheshimiwa Spika, tunapoteza utamaduni wetu. Hatuwezi tukazungumzia suala la nchi hii kama Mwalimu Nyerere hatujaanza kumtaja. Nasema siyo nyumba tu, kama Mwalimu Nyerere alikuwa akivuta Kiko, basi mpaka kile ilikuwa kitafutwe kiwekwe. Kama alikuwa ana viatu vyake vya zamani, basi vilikuwa viwekwe, kalamu ya mwisho aliyokuwa akiandikia, iwekwe.

Leo tunaibomoa nyumba au tuna nia ya kuibomoa! Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu atumie busara zake, nasema nadhani uwezo anao kuzuia suala hilo. Hata kama wanataka kujenga, lakini ile nyumba ibakizwe, kwa sababu Pakistan, India na kwingineko vitu kama hivyo wanavienzi na watu wanapoingia katika maeneo yale wanaotoka nchi za nje wanapelekwa pale ili kuonyeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine; tunasikia kauli za baadhi ya watu sijui ni nani, wanasema kwamba Tanzania haikubaliki kiulimwengu kwa sababu ni mtumiaji mbaya wa pesa. Hivi karibuni, kama sikosei, tarehe 19 Juni, 2007, nilimsikia Balozi wa Denmark akizungumzia kwa vyombo vya habari baada ya kuja wageni kutoka nchi mbali mbali kuisifia sifa nzuri Serikali ya Tanzania kwa matumizi ya miradi mbali mbali waliyopewa pesa ili watumie.

Kama wageni wanatusifia sisi, sisi hatuwezi kujisifia wenyewe, ni aibu na ni fedheha kwa sisi wenyewe na kwa Serikali yetu. Mheshimiwa Spika, nawaomba wote ambao dhana yao ni hiyo, tujaribu sana kuuliza nchi za nje, vipi Tanzania inakubalika na vipi wenzetu wanatupenda sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii ni yetu sote, lazima kizuri kinachofanywa tukithamini, kibaya tukosoe. Lakini, tusiwe kila wakati tunakosoa wakati ambao mambo

mengi mazuri yanafanywa. Tanzania ni miongoni mwa nchi pekee katika Afrika ambazo kama kupewa tuzo, itapewa tuzo kubwa kwa ajili ya kurekebisha uchumi wake, kurekebisha matumizi yake. Baada ya hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana! *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, Ahsante sana! Namwita sasa Mheshimiwa Ezekiel Maige. Ila kabla sijamwomba Mheshimiwa Nkayamba aliyekuwa anafuatia katika orodha ajiandae, nitatoa nafasi kwa Mhshimiwa Gosbert Blandes, kwa sababu mtakumbuka siku nilipomwita alikuwa hajisikii vizuri.

Kwa hiyo, itakuwa sasa ni Mheshimiwa Maige, atafuata Mheshimiwa Gosbert Blandes, halafu ndiyo Mheshimiwa Sijapata Nkayamba.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi na niweze kuchangia hotuba ya Bajeti iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza, kama wenzangu ambavyo wamekuwa wakitoa salaam zao za pole, na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Msalala, naomba kutoa salaam za pole sana kwa Familia ya Marehemu Mbunge mwenzetu, Amina Chifupa Mpakanjia. Mungu aiweke mahali pema peponi roho yake.

Mheshimiwa Spika, pia naomba katika utangulizi nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo pia iliwasilishwa kwa umahiri mkubwa, na kwa maana hiyo naiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nina machache ambayo ninaomba kuyawasilisha ambayo pia naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba yote ninayoyawasilisha ni matatizo, maombi, shukrani kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Msalala kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niwasilishe salaam za shukrani na pongezi kwa Serikali za Chama cha Mapinduzi, kwa jinsi ambavyo Serikali hii ya Awamu ya Nne imefanya kazi kwa kasi iliyoonekana kwenye suala la Elimu.

Katika Jimbo langu la Msalala, wakati ninakuwa Mbunge kulikuwa na shule za Sekondari 5, hivi ninavyozungumza, tayari tuna shule za Sekondari 13. Ina maana kuna shule kama 9 hivi ambazo zimejengwa katika mwaka mmoja tu huu. Naomba niishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu kwani kama unakumbuka ni mwaka mmoja tu uliopita tulikuwa na njaa kubwa sana, tukaomba chakula, lakini mwaka mmoja baadaye kutoka kwenye hiyo, suluba ya njaa, wananchi wamehamasika vya kutosha, wametoa kidogo walicho nacho kuunga mkono jitihada za Serikali yao ili kujiletea hali nzuri ya Elimu.

Kwa hiyo, nawapongeza sana wananchi. Na pongezi za kipekee nitoe kwa wananchi wa Kata ya Segese ambayo kuna wakati walionyesha hali kubwa ya kuniamini mimi kama Mbunge wao baada ya kuwa kumetokea mvutano ni namna gani mchango ufanywe.

Lakini wakasema kwamba watafurahi sana wakinisikia kijana wao, nimezungumza nao. Utata uliokuwepo ukawa umeisha, shule ya pili ya Sekondari ambayo inaitwa Nyikoboko ikawa imekamilika katika kipindi kisichozidi miezi mitatu. Ninawapongeza na kuwashukuru sana kwa imani kubwa walioionyesha kwangu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na suala la Sekondari, yako mengi yaliyofanyika. Mawasiliano ya simu, sasa hivi kuna minara minne inamaliziwa kujengwa kwenye Kata za Bulige, Ngaya, Chela na Kinaga ambayo itafanya Jimbo zima la Msalala liweze kuwa na Mawasiliano kitu ambacho hakikuwepo kule nyuma. Binafsi, naona kama nina bahati kwamba nimepata Ubunge kwenye Awamu hii ya Nne ambayo inafanya kazi kwa kasi na kwa maana hiyo, kila kero ninayoiwasilisha inakabiliwa kwa kasi kubwa. Kwa maana hiyo, kazi yangu kwa kweli inakuwa ni rahisi sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba pia niishukuru Serikali yangu na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuwa Mbunge katika zama hizi za kasi ambayo kwa kweli inakidhi haja. Nataka nizungumzie kuhusu mgogoro wa muda mrefu ambao umekuwepo kati ya wananchi wa Kijiji cha Kakola na Serikali kwa upande mwingine, lakini pia na Mwekezaji wa *Barrick Gold Mine* au *Bulyanhulu Gold Mine*. Kijiji hiki kimekuwa kikiwa kwenye *dispute* kwa miaka 11 wakitaka haki yao ya kuwa pale kama kijiji, baada ya kuwa mgodi na wenyewe umepata miliki inayofika mpaka kwenye kijiji hicho. Kero hii tumekuwa tukizungumza na Serikali, lakini kwa sababu kero imekuwa ni ya muda mrefu, ilifika wakati wananchi wale wakaanza kukata tamaa kwamba pengine na mimi naweza kuwa nikawa nawadanganya. Lakini, nashukuru sana na naomba nimpongeze kipekee Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Ngeleja kwamba alifika, akawaeleza wananchi wale jinsi ambavyo tumekuwa tukifanya kazi kwa pamoja kuhusu jambo hili na kwa kweli kero hiyo ambayo imekuwepo kwa muda mrefu baada ya muda siyo mrefu wakawa wametangaziwa kwamba kijiji cha Kakola kitakuwa ni kijiji rasmi na wenzetu wawekezaji wa Kampuni ya Barrick wakawa wamekubali kuanza kutoa huduma au kuanza kukisaidia huduma muhimu za jamii ikiwemo maji na umeme.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mgogoro huo kutatuliwa, wananchi wale waliwasilisha maombi kwamba wananchi wa Kakola ni wachimbaji, walio wengi wako pembezoni mwa mgodi. Ombi lao kubwa ambalo pia waliwasilisha kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wakati huo, ni kwamba wapatiwe maeneo ya kuchimba au maeneo ya kufanya shughuli zao. Walishauriwa na Mhshimiwa Naibu Waziri kwamba wajiunge katika Vikundi ili iwe rahisi pia kufikiwa na Serikali. Naomba kulitarifu Bunge lako Tukufu kwamba tayari wako katika kikundi. Kuna kikundi cha Ushirika kinaitwa *Kasi Mpya Gold Mine Co. Ltd.,* ambacho kinajumuisha wanaushirika wengi ambao ni wachimbaji wadogo wadogo. Ombi lao kwa Serikali iwapatie maeneo ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirejee kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hotuba kama nilivyosema ni nzuri, lakini nataka nizungumzie kwenye suala moja muhimu, suala la kilimo. Nafikiri niseme labda ni kwa bahati mbaya kwenye hotuba ya Waziri Mkuu katika sekta ya kilimo hajataja neno pamba. Nimesoma kutoka ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho, ukurasa wa 30 na 31

amezungumzia mikakati ya Serikali kuboresha zao la kahawa, kuboresha zao la korosho, lakini kwa bahati mbaya sana neno pamba halimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tu niikumbushe Serikali umuhimu wa pamba na namna gani kama Serikali ikaweka nguvu zake katika kilimo cha pamba, mapinduzi ya kupambana na umaskini yatatokea. Mheshimiwa Spika, zao la pamba linalimwa katika Mikoa 14 kati ya Mikoa 21 ya Tanzania Bara. Zao la pamba kwa takwimu za mwaka jana liliongoza kwa uuzaji wa mazao ya kilimo nje kwa kuingizia Tanzania dola milioni 45, ikifuatiwa na zaoa la kahawa lililoingiza dola milioni 37, korosho iliingiza milioni 22.

Lakini, pia zao hili linalimwa na asilimia 40 ya Watanzania wote. Pia, asilimia 60 ya zao zima la pamba linatoka katika Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa huu wa Shinyanga ambao unalima asilimia 60 ya pamba kwa kiasi kikubwa tunajua kwamba umekuwa na matatizo makubwa ya kujitosheleza kwa chakula.

Kwa hiyo, zao lao muhimu limekuwa zao la pamba, lakini kwa miaka ya karibuni limekuwa likipata matatizo makubwa. Zao hili ambalo ni roho kwa maisha ya wananchi walio wengi wa Mkoa wa Shinyanga, limekuwa likilimwa katika mazingira duni sana. Kwa takwimu ambazo ni za mwaka jana, zinaonyesha kwamba uzalishaji wa pamba ulikuwa ni kilo 300 kwa hekta moja na lengo letu ni kufikia kilo 100 mwaka 2010. Asilimia 80 ya pamba ambayo tumekuwa tunailima tumekuwa tuki-*export* nje na mchango wetu kwenye soko la dunia ni kidogo sana kwa maana hiyo bei ambayo tunaipata kule tumekuwa hatuna uwezo wa ku-*influence* kutokana na mchango wetu kwenye eneo hilo.

Lakini, pia mbaya zaidi asilimia 70 ya pamba inayolimwa, hawatumii mbolea na asilimia 100 ya uvunaji wa pamba unafanywa kwa mkono.

Kwa hiyo, pamba hii ambayo inatoa mchango katika nchi kwa kiasi hicho, imekuwa ikilimwa katika mazingira ya suluba sana, kiasi kwamba wakulima walio wengi wamekata tamaa na mbaya zaidi sasa hata katika soko dogo lililopo, wanunuzi wamekuwa wakiwakopa wakulima. Kuna wakulima kwa mfano wa Kata ya Ngogwa, Kata ya Busangi katika Jimbo langu la Msalala wanadai mauzo ya pamba toka msimu wa 2004/2005. *(Makofi)*

Mauzo ya pamba toka msimu wa 2004/2005. Katika mazingira hayo inaonyesha kwamba hali ya zao hili kwa kweli ni mbaya. Kama Serikali itafanya haya ninayoyapendekeza ninaamini kwamba mapinduzi makubwa yatatokea. Nimefanya utafiti inaonyesha kwamba kama kweli tukiboresha uzalishaji kwa mfano, tuliwashauri wakulima watumie mbegu za kisasa, watumie mbolea kwa maana ya kwamba Serikali iongeze ruzuku ya mbolea katika zao la pamba na pembejeo kwa maana ya madawa na tukafanikiwa kuongezewa uuzaji hata kufikia kilo 1000 kwa hekta moja maana yake ni kwamba ifikapo mwaka 2010 *export* ya pamba itakuwa ni dola milioni 432. Ukiangalia kwenye *balance of payment* ambayo ni chanzo cha ku-*depreciate* kwa *Tshs* yetu ni

kwamba *balance of payment* ilikuwa ni *deficit* mwakajana, tulikuwa na *deficit* ya dola milioni 1,321. Ukiongeza uzalishaji wa pamba peke yake kufikia hizi *export* ya dola milioni 432 nilizozitaja *deficit* ya *balance* of *payment* itafikia dola 934. Kwa maana hiyo, kupungua kwa thamani ya *Tshs* kutapungua kwa ku-*assume* kwamba vitu vingine vibaki ilivyo hivi sasa.

Lakini zao la pamba likiimarishwa linaweza likatoa ajira kwa Watanzania zaidi ya milioni 1,500,000. Kwa maana hiyo mkakati wote tunaozungumzia kuongeza ajira, ajira inaweza ikapatikana tu kwa kuelekeza kwenye suala la pamba, hii ina maana hata maeneo mengine yanaweza yakachangia kwa ziada.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu zao hili linalimwa kwa wananchi walio wengi ambao ni maskini, uzalishaji ukiongezwa kufikia kilo 1,000 kwa hekta moja maana yake na umaskini utapungua kwa wastani wa asilimia 20. Kwa hiyo, kwa kifupi ni kwamba zao la pamba ni muhimu sana. Ninaamini kwamba Waziri wa Kilimo na Chakula, atakapokuja kuzungumzia au kuwasilisha bajeti yake ninaomba sana tutambue kwamba pamba ndiyo inayoongoza kwa *export* ya mazao ya kilimo, ni uhai wa wananchi zaidi ya asilimia 40 wa nchi hii. Ni uhai wa wananchi zaidi ya Mikoa 14 Tanzania Bara. Tukiweka nguvu hapo na kuwapatia mbolea na pembejeo ninaamini kwamba wananchi hawa wataweza kujikwamua na umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzungumzia barabara za vijijini. Nashukuru sana Serikali kwa kuongeza fedha kwenye mfuko wa barabara ili kuboresha barabara za vijijini. Lakini ombi mahususi kuhusu barabara za vijijini kwa mfano, barabara mojawapo ni ile inayotoka Kahama kwenda kwenye kata ya Burige ambayo kuna uzalishaji mkubwa sana wa mpunga, tukijitahidi kuiboresha barabara kama hizi, ninaamini kwamba wananchi ambao ni maskini tutawatolea umaskini wao. Wananchi wa Kata hiyo niliyoizungumzia ifikapo mwezi wa 10, 11, 12 wakati wa masika gari huwa hazifiki, pamoja na kuzalisha tani nyingi za mpunga lakini kilo ya mchele huwa inauzwa kati ya shilingi 100 mpaka 150.

Wakati Kahama mjini tu ambayo iko kama kilomita 70 kutoka kata hiyo, mchele unauzwa kilo moja kutoka shilingi 500 mpaka 600 lakini hauwezi ukafika. Kwa hiyo, unakuta kule wanauza shilingi 100 lakini mjini wanauza shilingi 500/600, bei hiyo hawawezi wakaifikia. Tukiboresha barabara za vijijini , mfano barabara kama hii tutaweza kusaidia sana wakulima wetu na kwa maana hiyo, umaskini tutaweza kupambana nao na watu hawa wataweza sasa walau kuchangia hata mipango mingine ya maendeleo kwa urahisi kabisa kuliko ambavyo wanavyohangaika kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kama nilivyoanza kusema awali naomba kusema kwamba naunga mkono hoja hii na naomba sana Serikali isaidie kuboresha barabara za vijijini. Tunatambua jitihada zinazofanyika lakini pia tafadhali tunaomba tuelekeze nguvu kwenye zao la pamba. Ni ukombozi wetu na litatusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi*)

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kama wenzangu walivyoanza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Karagwe nichukue nafasi hii kutoa rambirambi kwa familia ya Mzee Chifupa kwa kuondokewa na mpendwa wetu Amina Chifupa ambaye tulimzoea na tulimpenda sana. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwasilisha hotuba nzuri sana. Wanasema mwenye macho haambiwi tazama. Hotuba ni nzuri. Nitakuwa na machache tu ya kuongezea kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaendelea juzi ilitolewa taarifa kwamba nilikuwa sijisikii vizuri, wananchi wangu wa Karagwe wakapatwa na wasiwasi kwamba labda naumwa sana au nimelazwa. Kupitia nafasi hii niwaondoe wasiwasi kwamba naendelea vizuri, afya yangu ni njema, kidogo tu nilikuwa nasumbuliwa na uchovu na homa kidogo.

Mheshimiwa Spika, leo naomba nianzie kwenye kilimo hasa napenda niende moja kwa moja kwenye zao la kahawa. Katika hili namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa juhudi za makusudi ambazo amezionyesha za kutaka kuboresha zao hili. Nakumbuka mwaka jana Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwaita wadau wote wa kahawa Dar es Salaam katika Ukumbi wa Karimjee. Lengo lilikuwa kuzungumzia namna gani zao la kahawa linaweza likaongeza ufanisi katika kuchangia pato la Taifa hasa sehemu ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, napenda nimkumbushe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba katika yote ambayo tulizungumza, wadau walichangia mambo mbalimbali, zikiwemo mbinu za kuongeza zao la kahawa, na kwa sababu ya muda leo nitataja moja tu. Kubwa ambalo wadau waliliona kwamba ni tatizo linalokwamisha zao la kahawa kutoongezeka ni tatizo la bei. Bei ya kahawa imekuwa ikishuka kila kukicha lakini wakati huo huo gharama za uzalishaji zinaongezeka zaidi ya mara mbili/tatu hata mara nne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wananchi wangu kule Wilaya ya Karagwe, Mkoa wa Kagera, ni wakulima wazuri sana wa kahawa. Sisi tumesoma, wazazi wetu wamesoma kwa kutumia zao la kahawa. Lakini kadri miaka inavyokwenda wananchi wanakata tamaa kwa sababu bei inawakatisha tamaa sana. Mpaka sasa hivi utakuta wananchi wa Karagwe wameshindwa hata kumudu maisha yao. Wameshindwa kupeleka watoto shule; wameshindwa kujenga nyumba za kisasa; wameshindwa kupata maisha bora ambayo walitarajia.

Mheshimiwa Spika, kwa nini bei ya kahawa inashuka? Sababu kubwa ambayo inashusha bei ya kahawa, mojawapo ni bei katika soko la dunia ambayo sitaki kuisemea sana kwa leo. Lakini la pili, tatizo kubwa sana ni makato ambayo anakatwa mkulima kwa kila kilo moja ya kahawa. Kuna utitiri wa makato katika kahawa ya mkulima. (*Makofi*)

Mimi nitaomba nitoe mfano wa makato ambayo yako katika Chama cha Ushirika cha Karagwe *(KDCU).* Kwa haraka hapa nataja makato kwa kilo moja ya kahawa ya maganda. Kuna usafirishaji wa fedha shilingi 1.11, kusindikiza fedha senti 19, usafirishaji kahawa maganda shilingi 15, *collateral management* shilingi 4.50, upakiaji na upokeaji maganda shilingi 1.33, bima ya mazao shilingi 1.40, bima ya fedha shilingi 1.36, ushuru wa vyama vya msingi shilingi 20, ushuru wa *Union* shilingi 19, utengenezaji wa mizani senti 65, vitabu vya taarifa ya mazao shilingi 1.94, uhakiki wa kahawa vyamani senti 11, udhibiti wa kahawa mipakani senti 17, riba ya mkopo senti 20, gharama za kupata mkopo shilingi 2.75, gharama za benki shilingi 1, ushuru wa Halmashauri ya Wilaya shilingi 27.5.

Mheshimiwa Spika, huu utitiri wa makato mwisho wa siku unamfanya mkulima aishie kupata naweza nikasema *token* yaani kile kidogo sana ndiyo anapelekewa mkulima wa kahawa.

Juzi wakati anachangia Mheshimiwa Kapteni Komba, Mbunge wa Mbinga, aliipongeza Serikali kwa kuondoa huu ushuru na gharama hizi mpaka kilo moja ya kahawa kule Mbinga imefika shilingi 2000. Lakini kule kwangu Karagwe kilo moja ya kahawa ni kati ya shilingi 450 mpaka 550. Malipo haya anayopata mkulima hayamuwezesha hata kidogo kuwa na morali wa kuweza kuongeza uzalishaji wa kahawa hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa nasema kwamba wananchi wanapofikia kuona kwamba bei ya kahawa yao iko chini, basi wanakata tamaa na badala yake wanang'oa ile kahawa, wanaanza kupanda migomba ya ndizi, nyanya, mahindi na maharage ili angalau kuona kwamba wanaweza kupata faida kidogo. (*Makofi*)

Wakati mwenzangu anachangia hapa, Mheshimiwa Maige, alieleza kwamba kahawa ni zao la pili kuchangia pato la taifa hapa nchini. Kwa mwaka jana limeingiza dola milioni 37, hii siyo hela ndogo. Mimi nasema hivi kama Serikali inataka kuongeza pato la taifa tafadhali sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, zile juhudi ambazo umezianzisha za kuondoa huu utitiri wa ushuru, ninaomba kabisa mwaka huu zianze. Utakapoondoa ushuru wote huu Mheshimiwa Waziri Mkuu nakuhakikishia zao la kahawa hapa nchini litaongoza. Serikali itapata fedha nyingi sana za kigeni na fedha za kuweza kuendesha mambo yetu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kule kwangu Karagwe sasa hivi wananchi kwa makusudi mazima wanang'oa ile mikahawa kwa sababu haiwapi faida. Bei ni ya chini mno, sasa mimi utakaponihakikishia kwamba huu utitiri utaondoka, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuhakikishia kwamba nitakimbia huko vijijini, nitawahamasisha na watapanda kahawa ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba nihamie upande wa miundombinu kwa Mkoa wetu wa Kagera. Utakumbuka kwamba Mkoa wa Kagera ulipata msukosuko wa vita vya Idd Amin. Lakini kwa bahati mbaya sana pamoja na miundombinu kuharibiwa ule Mkoa haukuweza kupata fidia *(compensation)* angalau ya

upendeleo. Mkoa ule umeendelea kuandamwa na wimbi la Wakimbizi. Wakimbizi wamekuja pale na kuharibu mazingira, hatujawahi kupata fidia.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo sitaki kuleta uchungu hata hivyo, naomba niwakumbushe kuzama kwa meli ya *MV* Bukoba katika ziwa Victoria. Mtakumbuka ile meli ndiyo ilikuwa inatoa huduma ya usafiri kutoka Bukoba hadi Mwanza, lakini baada ya meli ile kuzama wananchi wa Kagera wamebaki wanahangaika na usafiri badala yake wakapewa meli ya *MV Victoria.* Sasa hivi ninavyozungumza *MV Victoria* ni mbovu, haifai na haitembei majini. Kwanza ni kuu kuu sana, inatakiwa iondolewe pale kwa usalama wa raia wetu. (*Makofi*)

Hiyo hiyo *MV Victoria* walivyoona kwamba haifanyi kazi vizuri tukaongezewa *MV* Serengeti. *MV* Serengeti ilikuwa *designed* kwa ajili ya mizigo. Sasa hiyo meli ndio inabeba abiria kutoka Mwanza kwenda Bukoba. Kiusalama hili jambo kweli siyo zuri Serikali iliangalie. Ninafahamu kwamba kununua meli ni gharama kubwa sana lakini ni vizuri Serikali ikaanza kujipanga vizuri, ikaanza taratibu angalau watu wa Mkoa wa Kagera waweze kupata usafiri wa uhakika. (*Makofi*)

Ukiachia hilo tu kuna usafiri wa anga ambao watu wa Kagera wanautumia kutoka Mwanza au kutoka Dar es Salaam, tunatumia ndege na tunashukuru watu wa *Precision Air* jinsi wanavyotusaidia. Lakini la kusikitisha ni kwamba ule Uwanja ndege wa Bukoba na kwa kuzingatia mvua nyingi zinazonyesha pale, wakati mvua inaponyesha inabidi ndege igeuzie huko huko angani. Kama ilitoka Mwanza basi inabidi irudi huko huko Mwanza. Kwa maana hiyo yule abiria ambaye alikusudia kufika Bukoba hataweza kufika kwa sababu ule uwanja unashindiliwa tu na kifusi. Nilikuwa naomba Serikali ijitahidi kutenga kiasi cha fedha tuujenge uwanja uwe wa kisasa na uweze kufikika kwa urahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini hapo hapo sikumbuki ni mwaka gani, wakati Mheshimiwa Mwandosya akiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, alitembelea jimboni kwetu Karagwe akafika akatembelea kiwanja cha ndege kidogo kilichopo Kata ya Ihanda. Akafika pale, akaahidi kwamba kijengwe ili kiweze kusaidiana na Uwanja wa Bukoba Mjini. Mpaka juzi natoka kule sijaona dalili zozote labda namsubiri Waziri wa Miundombinu katika bajeti yake nione kama Uwanja wa Ihanda uko mle ndani na unajengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli usafiri katika Mkoa wa Kagera umekuwa ni balaa na ni kero kubwa sana. Mtakumbuka ukitoka Bukoba Mjini kuelekea Karagwe ni lazima upite barabara ya vumbi kutoka Kyaka mpaka Benako, ile ni barabara iliyojaa majambazi; ni barabara yenye vurugu na siyo nzuri. Nakumbushia ahadi ya Rais, Serikali iangalie jambo hilo.

Lakini vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa tamko ambalo amelitoa hapa kuhusiana na ujenzi wa zahanati kila kijiji pamoja na vituo vya afya kila kata. Kwa kweli nimelipokea vizuri, nakuhakikishia Mheshimiwa Waziri Mkuu,

nitakwenda kulitangaza kule kwangu na wananchi wangu wako tayari kujitolea kufanya kazi kuhakikisha kila kijiji kinapata zahanati yake. (*Makofi*)

Ombi langu Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba Serikali inapogawa fedha hizi ninaomba izingatie umbali wa vifaa vya ujenzi vinavyotoka Dar es Salaam kuelekea kule kwangu Karagwe. Bei ya sementi kutoka Dar es salaam hupatikana kati ya shilingi 9,000 na 10,000, ikishafika kule Karagwe inafika shilingi 22,000 mpaka 25,000. Sasa mgao uzingatie umbali, kama mikoa ambayo inapatikana vifaa vya ujenzi inapewa milioni tatu, basi Karagwe angalau tupewe milioni tano/sita kuweza kufidia hizo gharama za ujenzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nigusie upande wa afya, shirika la *MSD*. Shirika la *MSD* limetuangusha sana hasa sisi watu wa mbali. Upande wa Halmashauri wanajitahidi, wanaleta orodha ya dawa ambazo zinatakiwa kule kwa watu wetu, lakini wanapofika kule *MSD* wanaambiwa nusu ya orodha ya madawa yanayotakiwa kwa wagonjwa hayapo na hawawezi kupewa fedha na *MSD* waende kununua kwenye duka jingine, au Halmashauri ipewe fedha hizo ikae nazo.

Sasa mimi nilikuwa nashauri kwamba fedha hizo badala ya kuzirundika *MSD* na wakati madawa hawana, zipelekwe kwenye Halmashauri zetu. Mimi watu wale nawaamini, Mkurugenzi wangu na timu yake naiamini, wakae na fedha waweze kununua madawa wao wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kero ya tembo. Kule kwangu imetokea kero ya tembo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuomba msaada sana. Kuna tembo wamezuka kwenye kata ya Nyakakika, Kata ya Nyakasimbi, na Kata ya Kihanga, kijiji cha Mlamba. Tembo sasa wamekuwa ni balaa, badala ya kuwa ni nyara za taifa wamekuwa ni kero kwa wananchi. Wamekwishashaua watu na hakuna fidia. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu unisaidie katika hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumzia posho za Waheshimiwa Madiwani, sitaki kurudia sana lakini jamani tuwe wakweli, hivi shilingi 60,000 za sasa hivi unampa Mheshimiwa Diwani, mwenye Kata ya vijiji vitano/sita kama kule kwangu Karagwe, Kata ya Kituntu, Kata ya Igurwa, Kata ya Ihanda, Kata ya Nyakakika, huyu mtu hana hata pikipiki, baiskeli, unampa shilingi 60,000 kweli zinatosha? Nafahamu pamoja na udogo wa sungura lakini na hawa Madiwani waongezewe. Kama Waheshimiwa Madiwani hawatendi kazi hata sisi Wabunge hatuwezi kuwepo humu. Hawa Madiwani ndiyo wamejenga hizo shule za sekondari tunazosema, ndiyo watakaojenga zahanati. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu muangalie katika hizo posho za Madiwani shilingi 60,000 kwa kweli kwa wakati huu ni ndogo sana, napendekeza angalau kwa kuanzia basi iwe shilingi 150,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kilio cha watu wa Karagwe cha siku zote ni kuhusu ujambazi. Huu umekuwa ni wimbo, tumeuimba kila tukilala tukiamka tunaimba kuhusiana na ujambazi. Kwa kweli tumefika mahali wananchi wa Karagwe, tumekosa mahali pa kwenda. Wananchi hawawezi kutembea kutoka Mjini Karagwe kwenda

Bukoba, lazima wawe na *escort* ya askari wawili/watatu. Askari wenyewe wakipambana na majambazi wanalala mbele, wanakimbia. (*Makofi*)

Juzi kuna gari ya mfanyabiashara mmoja anaitwa bwana Paulo Tinkasimile, haijapita wiki mbili, gari lake lilimiminiwa risasi zaidi ya 20. Sasa wananchi wanashindwa kwenda kufanya shughuli zao za biashara. Lakini vilevile kuna ujambazi wa mifugo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakupongeza kwa juhudi ambazo Serikali izifanya kuwahamisha wale wahamiaji haramu. Lakini nilitaka kusema kwamba suala la Karagwe naomba lipewe *special attention,* liwe la aina yake, lisiwe kama sehemu zingine kwa sababu Karagwe tuna bahati mbaya tuko mpakani na nchi jirani. Matatizo ya pale ni ya kudumu. Mimi mwenyewe nikiwa Mbunge wa Karagwe kwenda jimboni kwangu lazima nipate *escort*. Ninapotaka kwenda kulala nyumbani kijijini lazima niende kwa *OCD* nimwombe msaada nilale nimelindwa. Sasa kama Mbunge nalindwa je, huyu raia wa kawaida itakuwaje? Napendekeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Serikali iangalie kwa upana sana Karagwe tupewe *special attention* kuhusiana na suala la ujambazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo nataka kuchangia ni kuhusiana na *SACCOS* zetu zilizopo. Naishukuru sana Serikali kwa jinsi ambavyo imeweka utaratibu huu. Niliondoka mimi mwenyewe kwenda kuhamasisha *SACCOS*, karibu kata zangu zote nimekaa na madiwani wangu, wananchi wamepokea vizuri na karibu kila kata Jimboni kwangu Karagwe ninazo *SACCOS*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Kabla sijamwita msemaji anayefuata Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, nitamke wale wanaofuatia kwa sababu nilikuwa napata vikaratasi hapa. Niwatamka wanne wanaofuatia sasa. Baada ya Mheshimiwa Nkayamba ni Mheshimiwa Brig. General Hassan Ngwilizi, halafu Mheshimiwa Idd Azzan halafu Mheshimiwa Josephine Genzabuke na baada ya huyo Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. SIJAPATA FADHILI NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kigoma, napenda kutoa rambirambi zao kwa kifo cha Mheshimiwa Amina Mpakanjia ambaye alitutoka siku ya Jumatano. Namwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. Amin!

Mheshimiwa Spika, pili, napenda nitoe shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Manaibu wake. Kwa nini nitoe shukrani hizo? Katika bajeti iliyopita ya mwaka 2006 niliomba wawajengee bweni watoto wasioona na wenye mtindio wa akili waliopo katika Shule Maalumu ya Uvinza Kigoma. Hivi ninavyosema Mheshimiwa na kundi lake wameweka kutuma shilingi milioni 9 kwa ajili ya kuwajengea bweni. Kwa hiyo, nawashukuru sana. Wananchi wale wanasema Mungu awazidishie rehema ili muweze kurudi katika kipindi kingine. (*Makofi*)

Vilevile katika bajeti iliyopita niliweza kuzungumzia akina mama ambao wanaopigwa *station* wakati wa kuuza biashara zao ndogo ndogo waliopo Uvinza, Kazulamimba, Rwiche, pamoja na Nguruka. Wakati huo walikuwa wakiuza biashara zao wanakuja mgambo wanawapiga vibaya sana wanaambiwa wasiuze zile biashara na wakati mwingine wanawamwagia biashara hizo. Lakini kwa Awamu hii ya Nne yenye Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya hilo tatizo tena hawana, wanauza bila wasiwasi wowote. Kwa hiyo, wanajinafasi. Namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Uraia ameweza kupeleka mkono wake pale na wale mgambo wakaweza kuacha tabia yao mbaya, walikuwa wanawasumbua akina mama hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nahamia miundombinu. Sisi Mkoa wa Kigoma ni watu ambao tumesahaulika tangu Awamu ya Kwanza, Awamu ya Pili mpaka Awamu ya Tatu. Tumesahaulika kabisa! Barabara hazipitiki, ukienda barabara yoyote kuanzia Kibondo Kasulu mpaka Kigoma ni balaa tupu hasa wakati wa masika. Ukienda barabara ya kutoka Mwandiga kwenda Kalinzi, wakati wa masika bei inaongezeka inakuwa shilingi 10,000 kwa mtu mmoja usafiri.

Naiomba Serikali kwa kupitia awamu hii yenye Ari Mpya, Nguvu na Kasi Mpya, iweze kutujengea barabara hizo kwa kiwango cha lami kutoka Nyakanasi, Kibondo mpaka Kigoma ili tuweze kusafiri kama wanavyosafiri watu wa kutoka Dodoma mpaka Dar es Salaam kwa saa mbili. Lakini sisi tumekuwa tukisafiri kwa siku tatu tunalala njiani kwa sababu ya hiyo barabara mbovu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itutengenezee barabara ya kutoka Tabora hadi Kigoma kwa kiwango cha lami ili wafanyakazi wanaouza samaki wabichi na dagaa wabichi na waweze kuwapeleka Tabora mpaka Dodoma. Nadhani wananchi wa Dodoma watafurahia kula Migebuka ya huko. Naiomba Serikali kwa muono huu ilio nao wa *speed and standard* waweze kutekeleza yale yaliyosemwa wakati wa kampeni mwaka 2005 katika Ilani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ajali barabara, zimekuwa zikitokea mara kwa mara, kama hizi za juzi kwa kweli zimetusikitisha sana hasa hizi zilizotokea Singida. Sasa mimi naomba kuiuliza Serikali katika miaka iliyopita, miaka ya nyuma kidogo Serikali iliweza kuweka *speed governor* kwa magari yote yaendayo katika mikoa mbalimbali na yale yaendayo mjini; lakini nashangaa sasa hivi *speed governor* hazisemwi; je, huo mradi ulikuwa ni wa mtu binafsi au ulikuwa wa Serikali? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Afya, watumishi wa Idara ya Afya hasa waliopo vijijini wamekuwa wakifanya kazi kwa muda mrefu bila kupumzika. Wamekuwa wakifanya kazi zao kuanzia saa mbili mpaka saa tisa, wanapokuwa wamekwenda nyumbani kupumzika wanaitwa tena kwenda kufanya kazi.

Watumishi hao wamekuwa hawapumziki, hata usiku wanaitwa kwenda kufanya kazi hizo ukizingatia kwamba kila zahanati ina watumishi wawili au watatu. Hata wakati wa kipundupindu, wamekuwa hawapumziki; wamekuwa wakifanya kazi ngumu sana, kitu ambacho ni hatari kwa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, naomba watu hao hasa wale walioko vijijini walipwe *on call allowance*. Lakini katika majibu ya Naibu Waziri, alisema kuwa hiyo *on call allowance* imewekwa kwenye mishahara yao. Lakini nimefuatilia wale watumishi wamesema hakuna.

Mheshimiwa Spika, watumishi hao hao wamekuwa wakifanya kazi ngumu sana hasa wale wanaowazalisha wazazi. Unaweza ukikaa vibaya ukashtukia yule mzazi amekupiga teke mdomoni au wakati mwingine hujamwambia sukuma, yeye anasukuma tu! Unakuta yale maji yanakudondokea mdomoni. Huoni kama hayo ni madhara! Nilikuwa naiomba Serikali iwalipe *disturbance allowance* watumishi hao ili na wao wafanye kazi zao kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Madiwani wao wamekuwa wakifanya kazi katika Halmashauri zao na ndiyo washauri wakuu, bila wao hata sisi hatuwezi tukafanya kazi. Hiki kiwango cha posho ya sh. 60,000 kwa kweli hakiwafai, yaani katika kata zao wananchi wamekuwa wakiamka asubuhi kwenda kuwaomba fedha wakiwatolea matatizo yao mbalimbali, "nina mtoto mgonjwa, nina mtoto anataka kwenda shule!"

Gharama za Shule ni sh. 30,000 au sh.60,000 hiyo hiyo na wakati Diwani huyo huyo na yeye anataka kusomesha, ana mtoto wake yuko Sekondari, kwenye shilingi 60,000 na familia yake nayo inataka ile, awape matibabu watoto wake, hivi shilingi 60,000 zitawatosha? Jamani na wenyewe muwaangalie kama ni binadamu, kwa kweli shilingi 60,000 haziwatoshi. Kwa hiyo, naiomba Serikali kuangalia iangalie upya kiwango hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Madiwani wamekuwa wakifanya kazi nyingi sana, wanakwenda kwenye mikutano na kwenye Kata zao. Wengine wana wana vijiji vitatu mfululizo, unakuta kijiji kimoja kiko hapa kingine kiko Kibaigwa.

Madiwani hao wamekuwa wakitembea kwa miguu mpaka mimi mwenyewe nawaonea huruma. Mpaka siku mmoja Diwani mmoja nikamtania, nikamwambia kuwa Mheshimiwa, miguu itakurudi tumboni kwa kutembea muda mrefu.

Sasa naiomba Serikali iwakopeshe pikipiki. Kwa kuwa wameongezwa hizo shilingi 30,000 basi hizo 30,000 waweze kukatwa ili waweze kununuliwa pikipiki hizo na kama itakuwa hazikutosha waweze kukatwa wakati wa kiinua mgongo chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika kuhusu maji katika Mkoa wa Kigoma, jimbo la Kigoma Kaskazini kuna akina mama ambao wanapata shida sana. Kuna chanzo kimoja cha maji ambacho kilitegwa katika Mto wa Mkongoro kinachohudumia Bitale, Kiganza pamoja na Mwandiga. Yaani akina mama hao wamekuwa wakipata shida sana. Hakuna cha masika wala kiangazi, yaani wamekuwa wakiamka mapema sana.

Kile kipindi cha kombora cha asubuhi, wakati ndiyo mtu unapata usingizi mzito, wao wamekuwa wakiamka asubuhi kwenda kuchota maji kuyatafuta kwenye mto mmoja unaoitwa Mungonya, wanatembea karibu saa nne, tano kwenda kutafuta hayo maji. Sasa hivi ukiwaangalia karibu wanaota vipara. Mwanamke hana asili ya kuota kipara, wanaoota vipara ni wanaume.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa niongelee Walimu. Sote tunafahamu kuwa bila walimu tusingekuwa hapa. Naiomba Serikali iwajengee nyumba iwakopeshe. Maana yake wakati wa kustaafu kazi, utakuta mwalimu anahangaikia mahali pa kuishi. Ukimwuliza wewe si ulikuwa mtumishi, anasema bwana mshahara ulikuwa hautoshi na kweli mshahara hautoshi. Kwa hiyo, naiomba Serikali iwajengee nyumba ili Serikali yenyewe iweze kuwakata kidogo kidogo. Watakapokuwa wamestaafu wasiwe na matatizo ya mahali pa kwenda kuishi. Kwa kweli mimi nawaonea huruma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kilimo, katika Mkoa wa Kigoma katika kijiji cha Kalinzi na Manyovu wanalima kahawa. Kahawa hiyo ni kahawa ambayo ni nzuri sana inazidi hata ile ya Bukoba, Arusha na Moshi. Wanasema ile ina ladha nzuri sana, ni kahawa ambayo inapendwa mno. Lakini sasa wananchi hawana mahali pa kwenda kuiuza. Unakuta wanapokuwa wanauza kahawa hiyo wanauza kwa bei ndogo sana. Kwa hiyo, namwomba Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika awaone hawa wana-Kigoma wanaosumbuka na kahawa yao. Naomba wasaidiwe, wawatafutie soko.

Katika Halmashauri ya Kigoma wamenyimwa pesa za ruzuku ya maendeleo. Waheshimiwa Madiwani walikaa wakaliona hilo kabla ya kunyimwa ruzuku hiyo, wakawa wameandika barua ya kuwasimamisha baadhi ya watumishi. Wakapeleka Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Walivyokuwa wamewasimamisha baada ya siku mbili, tatu au mwezi mmoja wakawa wamerudishwa kazini. Wakasema msipowataka hawa watumishi basi mtanyimwa ruzuku. Sasa mbona wamenyimwa ruzuku? Ina maana hizo pesa zimechukuliwa na mashetani? Kama zimechukuliwa na mashetani tunataka leo hii hii tujue.

Waheshimiwa Madiwani waliamua kuandika barua ya kuwasimamisha kazi kwa sababu waliona wale watumishi waliokuwa wakifanya kazi pale ndiyo wanaowahujumu pesa hiyo. Lakini Serikali Kuu iliamua kuwarudisha kazini. Papo hapo *PCB* ikafanya kazi kwenda kuchunguza benki kama kweli wanaweza kuwa na hela nyingi za kuweza kuhujumu Halmashauri. Mmoja walikuta ana shilingi milioni 200, wengine wana shilingi milioni 40 na wengine shilingi milioni 80. Lakini Serikali haikuweza kuchukua hatua yoyote ile. Mpaka sasa waliwachukua wale watumishi wakawahamisha kutoka Kigoma kuwapeleka sijui Arusha au Morogoro. Kwa kweli hawakutenda haki, inatakiwa mkono wa Sheria ufanye kazi, uwafuate huko huko mahali walipo, wachukuliwe hatua. Zile hela ambazo zilikuwa zimepatikana benki ambazo zilikuwa zimezidi uwezo wao naomba wazirudishe Halmashauri. Ndugu yangu Pinda, mtani wetu, tunaomba hili ulifanyie kazi. Tunaomba kabisa ulifanyie kazi. Hatuwezi kuhujumiwa hivi hivi tunaona! Watumishi watolewe Kigoma wakapelekwe sehemu nyingine wakati wametuhujumu haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naiunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. BRG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge katika kuomboleza kifo cha ndugu yetu, Mheshimiwa Mbunge mwenzetu , Amina Chifupa, Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake aliyowasilisha hapa ni nzuri, sina matatizo nayo. Kwa vyovyote vile bajeti tumekwishaipitisha, labda nianze kwa kusema kwamba nadhani hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kielelezo cha ubora wa CCM. *(Makofi)*

CCM ni chama kikongwe, kila mtu anakihusudu katika Afrika hii. Bahati mbaya kwamba kuna wenzetu wengine wanaona kwamba chama hiki hakijafanya chochote. Lakini CCM ni mwalimu na daima ukimkuta mwanafunzi anamlaumu mwalimu ujue basi huyo masomo kwake yatakuwa magumu sana. Wenzetu wajifunze kusoma kutoka CCM. *(Makofi)*

Lakini vilevile Mheshimiwa Spika, niwapongeze ndugu zangu, viongozi wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Lushoto kwa kazi nzuri waliyoifanya. Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Lushoto kina nguvu, na pale wapinzani hawaoni ndani. Sio kwa miaka iliyopita tu hata mwaka 2010 hawataona ndani. Wananchi wa Lushoto ni wachapa kazi, wananchi wa Lushoto wanapenda maendeleo, isipokuwa wananchi wa Jimbo la Mlalo wanawaomba viongozi wao wa kitaifa wafike Mlalo, kwamba ukifika Lushoto bado hujafika Mlalo, jimbo la Mlalo liko kilomita 20 Kaskazini Magharibi ya Lushoto. Bahati mbaya kwamba viongozi wengi hawajafika huko, lakini ni sehemu nzuri sana, ina wananchi wazuri sana wachapa kazi. Shughuli zote za kimaendeleo ambazo zimeagizwa kitaifa zimetekelezwa vizuri sana , shule tumejenga, kuna Kata zingine wamejenga sio *secondary school* moja tu, wamejenga mpaka tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wa Mlalo ni watu ambao wanajitengenezea barabara zao kwa nguvu zao wenyewe isipokuwa pale ufundi unapowazidi; ni watu ambao pia wamejijengea zahanati zao. Kwa hiyo, ndugu zangu mtakaopata nafasi ya kutembelea kule karibuni, hamtapata matatizo. Hata hivyo, kama ilivyo kawaida kila penye neema vilevile pana matatizo. Yapo matatizo katika Jimbo la Mlalo na leo hii Mheshimiwa Waziri Mkuu ungetembelea jimbo lile wananchi wangekuambia vilio vyao vifuatavyo:-

Kilio cha kwanza ipo barabara moja ambayo inatoka Kata ya Mbaramo kwenda Mlalo ili kuunganisha kwenda Makao Makuu ya Wilaya ya Lushoto. Barabara hii ni kitendawili. Kwa sababu Kata ya Mbaramo kwa bahati mbaya ni moja ya Kata za Jimbo lile ambazo hazina usafiri. Ukitaka kwenda Mbaramo ni lazima upitie Mnazi, upande mlima kilomita 16, barabara ile inapandwa na magari ya *four wheel drive.* Kwa hiyo, mizigo yote mizito inabidi wananchi waipandishe kwa vichwa. Mbaramo pana maendeleo wamejijengea shule, wana nyumba bora kama walivyo watu wote wa Mlalo. Sisi kule hatuna haja ya kuwaambia watu wajenge nyumba bora, nyumba nzuri kabisa.

Lakini tatizo ni usafiri. Lakini *solution* ya tatizo la Mbaramo ni kujenga barabara kutoka Mbaramo kuja Mlalo. Bahati mbaya barabara hii inapita kwenye msitu wa asili unaitwa Shaghayu. Barabara hii zamani enzi za Ujerumani ilikuwa inapitika kwa magari

ya farasi. Lakini baadaye usafiri huo ulikuja kuachwa na msitu umerudia imebakia njia ya miguu. Wananchi walijitolea kuchimba barabara hii, walianza Mbaramo kuchimba mpaka wakafika kwenye mpaka wa msitu na upande wa Mlalo wakachimba mpaka kwenye mpaka wa msitu.

Baada ya hapo Halmashauri yao ya Wilaya ikaomba kibali kutoka Serikalini ili barabara ile ijengwe. Bahati mbaya jibu lililokuja kutoka Serikalini ikawa ati vyanzo vya maji vitaharibiwa. Lakini kitendawili kinaongezeka kwa sababu Serikali ilikwishaidhinisha fedha ya ruzuku ya *road fund* ili barabara ile Serikali iunge mkono nguvu za wananchi. Zilitolewa shilingi milioni 66.

Fedha zile zilishindikana kutumika kwa sababu kile kibali cha barabara ile kimeshindikana kupatikana. Bahati nzuri hili nimelizungumza na Waziri mhusika wa sasa na amelielewa na ndugu zangu wa Mlalo kama wanasikiliza huko naamini kwamba jibu zuri litatokea hivi karibuni, wavute subira barabara ile itajengwa.

Tatizo la pili, Mheshimiwa Spika, ambalo watu wa Mlalo wataweza kuieleza Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu, lipo eneo la umwagiliaji la Kitivo. Mradi huu ulikuwa ni mkubwa sana. Ulikuwa ni mkubwa kuliko wa *Lower Moshi* lakini kwa bahati mbaya mradi ule pamoja na vifaa vyote na fedha zilizotumika, zile mvua za *Elnino* ziliponyesha zilibomoa bwawa, matokeo yake mradi ule umetelekezwa. Kilichofuatia, taratibu ni kuanza kuondolewa kwa vifaa, na hatujui vilikopelekwa.

Lakini matokeo yake ni kwamba wananchi sasa waliokuwa wanalima wanapata shida hawawezi kuzalisha kama walivyokuwa wanazalisha. Na ni tegemeo kwamba Wizara ya Kilimo upande wa umwagiliaji wataliangalia tatizo hilo. Jimbo la Mlalo lina maeneo mengine kama Lunguza na Mnazi ambayo yanafaa kwa umwagiliaji na yanaweza yakatuongezea mapato na vilevile chakula.

Kuna tatizo lingine la umeme katika Jimbo la Mlalo. Umeme umefika Mlalo, lakini mradi ule haujakamilika. Kuna tarafa ya Mtae ilikuwa upelekwe kule. Wananchi kule walihamasishwa wamekwishaweka nyaya katika nyumba zao. Tangu wameweka nyaya karibu miaka 6 sasa lakini umeme umekuwa ni kitendawili. Hilo nalo ni tatizo ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu atalipata akitembelea Mlalo. Tatizo lingine ni maji. Maji tunayo kule lakini ni maji ya vilimani, yakishatoka kwenye chanzo yanatiririka kwenda mabondeni. Sisi Wasambaa tunakaa juu ya milima kwa hiyo ukiyataka ni lazima uteremke chini. Kinachotakiwa ni matengenezo ya *intakes,* tumekwishatengeneza miradi ya *scheme* na programu zile na kukabidhi Wizara ya Maji lakini mpaka sasa hivi hatujapewa taarifa. Tunategemea kwamba katika mwaka huu wa fedha huenda tutapatiwa jibu ili wananchi wale waweze kupata maji ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia haya ya Jimbo la Mlalo, sasa nizungumze ya jumla kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Na mimi ningependa kujikita kwenye suala la ajali la vyombo vya usafiri. Mara nyingi tumezungumza hapa kwamba vyombo hivi vimeua Watanzania wengi sana. Juzi bahati nzuri, wiki iliyopita, Wizara ya Miundombinu ilitoa takwimu hapa kwamba ajali za barabarani peke yake mwaka 2005 kwa mfano, zilikuwa 16,300 na vifo vilikuwa 2,430,

kwa mwaka mmoja tu! Suala hili ni zito kweli kweli, wakati Mheshimiwa Mkuchika anachangia hapa jana alisema hii ni vita.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa mfano vita vyetu na majeshi ya Iddi Amin, Uganda, askari waliokufa hawakuzidi 300. Hivi sasa Marekani kule Iraq, toka mwaka 2003 mpaka tarehe 20 Juni, 2007 askari wao waliokufa ni 3,563. Sisi magari peke yake kwenye mwaka mmoja watu 2,400 na ushehe. Tuna vita gani hapa Tanzania! Kinachonisikitisha zaidi ni kwamba, juzi nilikuwa nasikiliza madereva wa mabasi wanalalamika kwamba siyo makosa yao. Wanataka waandamane kwa sababu wanadhania wana haki ya kuendelea kuwaua Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mlezi ndiye anayembeba mtoto na mbeleko. Mbeleko ikifunguka akianguka wa kulaumiwa ni mlezi sio mtoto. Madereva wao ndio wanastahili kulaumiwa kwa vifo hivi, kama waliona magari yana kasoro kwa nini walikubali kuyaendesha, waache kuendesha! *(Makofi)*

Kwa hiyo, visingizio wanavyovitoa sisi hatuwezi kukubaliana navyo hata kidogo. Watu hawa waliokufa mbali ya upande wa madereva tunao upande wa pili. Mashirika ya bima watu wanakufa, wanajeruhiwa, lakini hawapati fidia na sisi viongozi wa siasa tunaona hiyo ni sawa kabisa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tukatae. Mashirika ya bima lazima yawalipe watu wale. Napenda kuishauri Serikali ilivalie bango suala hili mpaka kieleweke, walioumia kwa nini hawajalipwa? Hatuwezi kuendelea kuachia Watanzania wanauawa na tukaona kwamba hao waliowaua wana haki ya kuua na mashirika ya Bima yana haki ya kupata faida, hapana! Tumechaguliwa na Watanzania ili tutetee haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nizungumzie suala la miundombinu kwa sababu inawezekana sitapata nafasi wakati Wizara hiyo ikizungumzwa. Katika hili nataka kuzungumzia usafiri wetu wa reli. Mpaka sasa hivi tunaelezwa kwamba tuna mkataba, kuna huyu mwekezaji, kuna mwendeshaji, tunamkabidhi reli. Lakini mimi kila nilivyosikiliza maelezo yaliyotolewa, kitakachofanyika hapa ni yeye atajenga reli mpya, injini mpya, na ataleta mabehewa mapya. Lakini kuna mambo *much more critical* kwa ajili ya maendeleo ya reli sikuyasikia.

Geji tunayotumia hapa Tanzania na *East Africa* ni *narrow gauge* huyu anayekuja atatuwekea *wide gauge i*li kuhakikisha kwamba matreni yetu yanakwenda kwa *speed* zaidi? Hicho bado hakieleweki. Lakini tunajua vilevile kwamba treni za siku hizi afadhali ziwe zinatumia umeme. Hili suala limefikiriwa katika kipindi hiki atakachokuwa anaendesha reli hiyo? Mimi nilidhani kwa vile kuna wateja wetu Magharibi sasa kuwa na *railway line* moja haitoshi. Tungekuwa na *railway line* mbili, moja kupeleka tu mizigo na mabehewa kuelekea magharibi na nyingine ya kuteremshia. Nia ikiwa ni ili tuweze kupeleka mizigo kutoka Dar es Salaam-Kigoma *in twenty four hours,* lakini kulingana na mipango nilivyoisikiliza ni kwamba tutaendelea na utaratibu tuliozoea wa kutengeneza reli itusafirishie kama tulivyozoea. Namna hiyo hatuta-*capture* biashara ile ya wenzetu wa nchi tunazopakana nazo.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa najiuliza, hivi wakati tunazungumzia mikataba hii wadau wa reli walihusika wapi katika kupendekeza? Ama tuliwaachia wataalam tu wakae wapige nadhiria zao kama wanavyoona bila kufikiria *political leadership* inasema nini. Hilo nadhani nalo ni lazima tuliangalie.

Mheshimiwa Spika, bado tuna matatizo pia kwa upande wa wanafunzi Wizara ya Elimu, bado tuna wanafunzi wanafukuzwa shule. Wakati Serikali inataka kila mtoto aende shule lakini bado unakuta mtoto anaambiwa hana karo, hana *uniform,* anarudishwa.

Hivi na utu uzima wetu huu hatujui kwamba ni nani anastahili kulipa hiyo karo? Kuna mtoto ambaye anajilipia karo? Kuna mtoto ambaye anajishonea nguo? Ni mzazi.

Kwa nini tusishughulike na wazazi ili tuhakikishe kwamba watoto hawa wanapata haki yao ya kusoma. Nadhani hili ni suala ambalo ni la muhimu, ni lazima tulitilie maanani sana.

Wiki mbili zilizopita Halmashauri ya Wilaya ya Ilala imezungumzia suala la kuwaagiza wenye mabaa waache kupiga muziki kwa makelele. Zikaanza kutoka hoja hapa, haiwezekani mpaka tufuate sheria.

Mheshimiwa Spika, wanaobughudhiwa ni Watanzania. Hebu turudi kwenye sheria, tuziwezeshe Serikali za Mitaa kwamba hakuna mtu anatakiwa kufungua baa kwenye mtaa kama wakazi wa mtaa ule hawajahusishwa na mimi naamini kwamba watu wa mitaa ile wakihusishwa watakataa mabaa na ma-*grocery* yafunguliwe ovyo. Tusiwape watu ambao wana uchu wa fedha tukasahau haki za wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na mimi kupata nafasi hii kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kinondoni, nami niungane na wenzangu kutoa pole kwa wenzetu wote ambao walipata ajali wakati tukiwa hapa Bungeni na takriban watu zaidi ya 50 walifariki katika ajali mbalimbali zilizotokea katika Mikoa ya Singida, Arusha na mingine.

Lakini pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kinondoni ninachukua nafasi hii kukupa pole Mheshimiwa Spika, wewe binafsi lakini pamoja na familia ya Mheshimiwa Amina Chifupa, kwa msiba ambao umetukuta hivi juzi na nimtakie tu Mwenyezi Mungu ailaje mahali pema roho ya marehemu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nichukue nafasi hii tena kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza kwa hotuba yake nzuri ambayo imesheheni mambo mbalimbali kwa kutuletea maendeleo katika Taifa letu. Lakini kubwa, hotuba yake ile imeelekea ama imeegemea kabisa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliizungumza Dar es Salaam na alionyesha ni jinsi gani Dar es Salaam inahitajika ipate ama kipaumbele au ipate msaada mkubwa sana kutoka Serikalini kutokana na Jiji lile linavyokuwa kwa kasi kubwa mno. Watanzania wengi ama wanapenda kuishi Dar es Salaam au wanapenda kutembelea Dar es Salaam. Kwa maana hiyo basi jiji lile linakuwa wakati wote na kuna msongamano mkubwa wa watu na vyombo vya usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Serikali haitaelekeza nguvu za dhati kabisa kuhakikisha kuwa Dar es Salaam inapewa kipaumbele, nina hakika jiji letu kwa kweli litakuwa na matatizo makubwa sana. Labda nianze na huduma za afya na napenda nizungumzie suala la hospitali ya Mwananyamala. Kwa kuwa wenzangu wote mnaifahamu, ama mnaisikia kwamba kila mara imekuwa ikilalamikiwa kwa huduma mbovu na mambo mbalimbali, lakini niseme tu wakati hospitali ile inajengwa ilikuwa inategemewa labda kuhudumia watu kati ya 150 na 300, lakini hivi sasa inahudumia kati ya watu 900 mpaka 1300 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaona ni jinsi gani hospitali ile ilivyozidiwa na mzigo wa wagonjwa. Kwa sababu hiyo, niiombe Serikali pamoja na mipango mizuri ambayo juzi tu Mheshimiwa Waziri wa Afya aliieleza ya kujenga hospitali ya Mkoa pale Dar es Salaam lakini wakati tunasubiri hiyo ya mkoa ijengwe basi ni vyema Serikali ikajaribu kuangalia ni jinsi gani itaweza kusaidia hospitali ile ili iweze kupata madaktari wa kutosha, wauguzi pamoja na vifaa ili iweze kukidhi haja kulingana na jinsi wananchi wanavyoitegemea sana.

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam tulikumbukwa na ugonjwa wa kipindupindu, na napenda pia nimshukuru na nimpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu naye aliuvalia njuga ugonjwa huu pamoja na Mkuu wetu wa Mkoa, Mzee wangu Abbas Kandoro, na kweli hivi sasa haupo. Lakini si haupo kwa maana umeondoka kabisa,

upo jirani jirani kutokana na hali halisi ilivyo Dar es Salaam. Ugonjwa wa kipindu pindu unasababishwa na uchafu. Yapo maeneo ambayo kwa kweli kama hatukuweza kuyatengeneza basi nina uhakika ugonjwa ule unaweza ukarudi tena baadaye. Nazungumzia mifereji ya maji machafu, mifereji ya maji ya mvua, na ndiyo maana Dar es Salaam mvua ikinyesha kunakuwa na mafuriko.

Mifereji ya kuondoa yale maji kwa kweli ama haipo kabisa au ni michache sana. Nina hakika Halmashauri ya Kinondoni inajitahidi sana kufanya hizo kazi ili kuweza kuweka mifereji. Lakini tatizo linakuwa ni kwenye upatikanaji wa pesa. Bado mapato yetu ni madogo. Mahitaji ni mengi sana, hivyo, inawezekana tukawa tunashindwa. Kwa hiyo, kwa sababu Kinondoni ni eneo ambalo lina msongamano mkubwa sana wa watu, naiomba Serikali iangalie jinsi ya kuwasaidia wananchi wa Kinondoni ili waweze kutengeneza mifereji ya kuondoa maji haya ya mvua.

Lakini si maji ya mvua tu, tuna majitaka. Maeneo ya kama *Kinondoni Block 41,* Kinondoni Shamba, hata wale wanaotumia vyoo wakichimba yale makaro, *water table* iko juu, mvua ikinyesha kidogo maji yanafurika. Kwa hiyo, ni vema tukaona ni jinsi gani tutaweka miundombinu ya kuondoa majitaka. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, na bahati nzuri Kinondoni unaijua vizuri, basi ujaribu kutusaidia kwenye hilo, na nina hakika Waziri Mkuu atakaposema basi! mambo yatafanyika kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona barabara ya Shekilango ilivyokuwa mbaya lakini pale Waziri Mkuu alipokwenda na akasema kwamba barabara hii inatakiwa ijengwe, imejengwa na hivi sasa inapitika vizuri kabisa. Lakini si hilo tu mambo mengi ambayo Waziri Mkuu amejaribu kuyazungumza kwa Dar es Salaam yanafanyika vizuri. Nikupe tu mfano kidogo juzi tu hapa Dar es Salaam tuna msongamano mkubwa sana wa magari lakini ubunifu wake na usimamizi wake mzuri ameweza kuuondoa msongamano ule kwa kitu kidogo tu kwamba badala ya kutumia njia mbili, asubuhi tutumie njia tatu, kitu ambacho kimeleta faida kubwa sana. Msongamano umeondoka, ingawaje mwanzoni kulikuwa na matatizo kidogo watu hawajazoea, lakini kwa kweli hivi sasa hali inakwenda vizuri mno. Niwaombe wale watendaji ambao wanamsaidia Waziri Mkuu ndugu zangu wa usalama wa raia, wajitahidi basi kusimamia vizuri zoezi hili ili mambo yaendelee kuwa mazuri na nina hakika kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyosema kwamba zoezi hili ni la muda lakini pale ambapo mabasi ya kasi yatakapoanza litakuwa limekwisha. Lakini kipindi ambacho tunaelekea huko basi usimamizi uwe nzuri, wapo madereva ambao ni wakorofi na hasa wa Daladala. Ndugu zangu wa usalama ni vyema tukawa makini sana na hawa madereva wa Daladala mara nyingi wamekuwa wakikiuka zile taratibu zilizowekwa. Tumeambiwa kwamba ni muda gani barabara tatu zitatumika, lakini wao wanaweza kuamua wanavyotaka wao tu, wakati wote tu! Hata ule muda ambao hauruhusiwi ilimradi dreva wa Daladala ana haraka sana yeye anaamua kupita hiyo njia ya tatu. Kwa hiyo, naomba wenzangu wa usalama tumsaidie Waziri Mkuu kwenye hili ili mambo yazidi kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo lingine Dar es Salaam katika kuondoa msongamano. Nimeona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza hapa barabara ambazo zitatengenezwa kwanza kwanza kwa kiwango cha changarawe lakini

baadaye kwa kiwango cha lami. Nina hakika hiyo itakuwa njia pekee ya kuondoa msongamano Dar es Salaam. Zipo njia nyingi za pembeni, wamezungumzia hapa barabara ya Kigogo mpaka Ubungo Maziwa, Kigogo kwenda Tabata. Ni kweli kabisa ni njia ambazo zikitengenezwa kwa kweli zitaondoa sana msongamano. Lakini ipo njia nyingine ambayo kama itatengenezwa inaweza kuondoa msongamano mkubwa sana katika barabara ya Ali Hassan Mwinyi. Barabara ambayo inakatiza nyuma ya Ubalozi wa Ufaransa, kuna njia ambayo inapita pale inatokea *Tazara Club* unapita Kinondoni shamba unatokea Biafra, unapita Mwananyamala Hospitali, Kijitonyamala na Polisi Kijitonyama Mabatini pale, unatokea Afrika Sana mpaka Mwenge. Hii njia nayo ikishughulikiwa kwa maana ya kutengenezwa vizuri itaondoa sana msongamano. Niombe tu Serikali ijaribu kutusaidia kuzitengeneza hizi njia ili kuweza kuondoa msongamano ambao unatusumbua. Nikukubaliane na hotuba ya Waziri Mkuu kwamba barabara hizi ambazo zinatengenezwa ni kwa kiwango cha changarawe lakini azma kubwa ni kuziweka lami. *(Makofi)*

Hili la lami ndio la msingi, kwa sababu hizi za changarawe tukizitengeneza hazichukui muda, pesa zinatumika nyingi lakini barabara huchakaa haraka kutokana na uwingi wa magari na wanaotumia barabara hizo. Kwa hiyo, ni vema tukajielekeza sana kwenye huo mpango wetu wa kuweka lami nafikiri ndio litakuwa suluhisho kubwa la kuondoa tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, nichukue tena nafasi hii kumpongeza tena Waziri wa Maji na Naibu wake kwa kazi nzuri waliyoifanya. Hivi sasa Kinondoni maji angalau yanapatikana katika baadhi ya maeneo na niseme tu kama ambavyo wenyewe waliahidi kwamba itakapofika 2008 basi asilimia kubwa ya wananchi wa Kinondoni na Dar es Salaam kwa ujumla watapata maji. Kwa kweli dalili zimekwishaonekana. Kazi nzuri sana imefanywa, maji kwa kweli yameanza kupatikana, nawapongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu ulikuja kutembelea katika Jimbo la Kinondoni ingawaje ulikuja mara tu ukaondoka hukulala kama ambavyo unakwenda kwa wengine, lakini nikushukuru sana kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie tena suala la maeneo ya wazi, maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya michezo. Maeneo mengi yamevamiwa lakini yapo ambayo kwa kweli bado tunaweza tukayachukua na vijana wetu wakapata kufanya michezo. Nazungumzia eneo la Jangwani, eneo la Jangwani ni viwanja ambavyo wakati ule Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere alikuwa amelitenga vizuri mno kwa ajili ya michezo na kweli ulikuwa ukienda jioni pale unafurahi unavyoona timu zote zinafanya mazoezi, vijana wanacheza pale. Lakini hivi sasa eneo lile limevamia, kwa hiyo, niiombe Serikali kwa kusaidia na hizi Halmashauri waone ni jinsi gani eneo lile litarudishwa ili libakie kuwa la michezo kama ambavyo limepangwa.

Mheshimiwa Spika, ningependa tena nimalizie hotuba yangu kwa kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja, na kweli haya ambayo yameainishwa katika hotuba yake yakitekelezwa kwa dhati kabisa, nina hakika kuwa kero nyingi zitaondoka kama ambavyo Baba wa Taifa alivyosema kuwa "inawezekana

timiza wajibu wako." Basi nina hakika kabisa watendaji wetu watatimiza wajibu wao ili kuona kwamba haya ambayo tumeyaahidi tunayatekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho, Mheshimiwa Waziri Mkuu wakumbushe watendaji wako hasa Halmashauri kukusanya mapato, *proper tax* Dar es Salaam tunachelewa ama tunapata hela kidogo sana. Tungeweza kupata pesa nyingi lakini watendaji hawafanyi kazi nzuri, kwa hiyo, wakumbushe ili waweze kukusanya mapato vizuri ili kuweza kuondoa hizi kero. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono asilimia mia moja, asante sana. (*Makofi*)

**MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi naungana na wenzangu kwa kutoa rambirambi kwa Marehemu Amina Chifupa. Marehemu Amina alikuwa ni jasiri nami nilijifunza mengi kutoka kwake, naomba Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema roho yake peponi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri lakini vilevile nawapongeza Mawaziri ambao wako katika Wizara yake pamoja na watalaam kwa kuweza kusaidiana naye kutengeneza hotuba nzuri inayoeleweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ya kwangu ni machache. Kwa kupitia Bunge hili, kwanza kabisa napenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuweza kuja mkoani Kigoma kututembelea. Mheshimiwa Rais alipotembelea katika mkoa wa Kigoma aliweza kufika katika Wilaya zote za Mkoa wa Kigoma, na alipopita katika Wilaya zile aliweza kuzungumza na wananchi katika mikutano ya hadhara. Napenda nimshukuru kwa ahadi zake kusema kwamba atatutengenezea barabara. Nina imani kabisa kwa sababu wakati anapita akiomba kura aliahidi kututengenezea barabara, na baada ya kuwa ameanza kazi, amerudi tena kutuahidi kututengenezea barabara, ninaimani barabara ya Kigoma-Tabora-Manyoni itatengenezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge la Bajeti la mwaka jana Waziri Mkuu alifuatana na Waziri wa Miundombinu na Waziri wa Kilimo pamoja na Naibu Waziri wa Elimu, wakati wa ziara ile naye aliweza kujionea hali halisi ya barabara yetu ya Kigoma. Sasa naimani kwa vile Mheshimiwa Rais ameona Waziri Mkuu alijionea hali halisi na kwa sababu Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu barabara yetu ya Kigoma itatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, ombi kwa Miundombinu: Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, tunakuomba mara mtakapopata pesa uzingatie kutekeleza ahadi ambayo Rais ameiahidi. Tunaomba kabisa chonde chonde najua pesa zitapatikana, tunaomba mtutengenezee barabara yetu ya Kigoma, ninajua mkishapata pesa mkafungua barabara yetu ya Kigoma mtakuwa mmefungua uchumi wa nchi hii. (*Makofi*)

Vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuweza kutupatia mfadhili wa kututengenezea daraja letu la Malagalasi, likishakuwa tayari mkoa wetu vilevile utakuwa umefunguka. Wananchi wa Kigoma sisi sio wavivu, miundombinu tu ndio inayotufanya sisi tuonekane maskini, lakini tukipata miundombinu tutaweza kujitegemea kwa kasi ya ajabu, kwa sababu mkoa wetu kwanza hatuna njaa, chakula kinastawi, tuna imani miundombinu hiyo yote itakapokamilika sisi tutaweza kupiga hatua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Elimu, kwa kupitia mpango wa MMEM na MMES, Mkoa wa Kigoma tumeweza kupata maendeleo katika elimu. Tumeweza kupata shule 52 za kata na tuko mbioni kuongeza shule nyingine. Pamoja na mafanikio hayo matatizo madogo madogo hayakosi, tuna tatizo la nyumba za walimu, tatizo la maabara katika shule zilizofunguliwa.

Lakini la pili, tuna tatizo la hosteli, tunaomba Serikali iweze kutusaidia katika mambo hayo yanayotusibu. Niwaombe walimu wanaopangiwa kuja mkoa wa Kigoma waje kwa sababu wakati wanajaza mkataba huwa hawachagui ni sehemu gani wataenda kufanya kazi. Tunawaomba walimu kupitia Bunge lako Tukufu wanapopangiwa kuja mkoani kwetu waje, sidhani kama kuna sheria inayosema kwamba mwalimu achague sehemu ya kwenda. Kwa hiyo, wanapopangiwa sehemu ya kufanyia kazi Kigoma tunawaomba waje, la sivyo kule watakakokuwa wamekimbilia wasiajiriwe kwa sababu ili tumkomboe mwanafunzi na ili tukomboe elimu yetu ni lazima tuwe na walimu. Sasa kama walimu watakuwa wanachagua ni sehemu gani wakafanye kazi, sisi tunaoishi kwenye sehemu ambazo miundombinu ni ya kubahatisha, ina maana walimu tutakuwa hatupati. Tunaomba Wizara ya Elimu iliangalie suala hili ili iweze kutusaidia, walimu wasichague maeneo ya kwenda hata Kigoma waje! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, umeme wa Kigoma ni wa majenereta, sisi tunatumia jenereta, tunaomba Serikali ituunganishe kwenye mtandao na sisi tuweze kuwekwa kwenye gridi ya taifa. Mkitupatia umeme na sisi tutaweza kuufungua mkoa wetu kwa kuwaita wawekezaji kuja kuwekeza katika mkoa wetu. Hatuwezi kuwaita wawekezaji sasa hivi au hakuna mwekezaji anayeweza kuja Kigoma kwa sababu umeme hauaminiki. Tunaomba mtusaidie jamani, sisi tumesahaulika muda mrefu. Serikali ya CCM ninajua kabisa ina nia nzuri na Mkoa wa Kigoma lakini tunaomba ifanye haraka. Maji nayo ni tatizo, kwa mfano, vijiji vya milimani ambavyo viko nyanda za juu kwa kweli maji ni shida, ukienda Manyovu maji ni ya tatizo, ukienda vijiji vya Shunga maji ni tatizo na sababu kubwa pamoja na matatizo mengine yote, ile milima nayo ilioko kule kwetu inachangia. Tunaomba basi Serikali itusaidie kutupatia hata visima vya muda.

Mheshimiwa Spika, barabara za vijijini nafikiri tutakubaliana wote hapa kwamba hatuwezi kuondoa umaskini kama miundombinu sio mizuri, kwa ajili hiyo tunaomba barabara za vijijini, mfuko ule wa *road fund* uongezewe pesa ili barabara za vijijini ziweze kufunguka. Tukifungua barabara za vijijini wananchi watapata fursa ya kwenda kuuza biashara zao katika makao makuu ya Wilaya kufanya shughuli zao mbalimbali katika Makao makuu ya wilaya lakini kama barabara hazipitiki kwa kweli litaendelea kuwa ni tatizo. Barabara hizi zinasababisha watu waendelee kupata shida kwa sababu ukikuta barabara za kule vijijini kwa kweli hazipitiki, ni mbaya. Kwa mfano, kuna

barabara ya Nanila, Mwayaya, Buhinda mpaka Lusaba haipitiki. Ukiendelea mbele tena kuna barabara ya Hedu Juu mpaka Malumba kupitia Mkundusi haipitiki. Barabara ya Makele kwenda Kitanga, Kitema, Nyenge , haipitiki na barabara nyingine nyingi ambazo ziko katika Mkoa wa Kigoma ambazo ziko vijijini hazipitiki kwa sababu pesa inayotolewa haitoshi. Naiomba Serikali ituongezee pesa kwenye mfuko wa *road fund* ili barabara zetu za vijijini ziweze kutengenezwa, ziweze kufungua mawasiliano ya vijiji na wilaya.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye afya, na yenyewe ni tatizo. Nashukuru zahanati zimejengwa lakini waganga hawatoshi, tunaomba tuongozewe waganga kwenye vile vituo ambavyo viko tayari. Kuna vijiji vingine navyo waganga wakipangiwa hawaendi, wanakataa kwenda. Kwa mfano, ipo hospitali moja katika wilaya yetu mkoani Kigoma aliwahi kupelekwa mfanyakazi kule, bahati mbaya yule mfanyakazi akawa amekufa ameuawa, na tangu wakati huo zahanati ile ina miaka miwili haina mfanyakazi, kila anayepelekwa kule anaogopa. Naiomba Serikali iweze kuliangalia suala hili ili wale wananchi wasiendelee kupata shida kwa sababu ya ukosefu wa waganga.

Lakini pia kuna zahanati nyingine ambazo ziko mbali na makao makuu ya wilaya, wahudumu wanapokwenda kufuata mishahara hospitali zile zinafungwa, wananchi wakienda kupata huduma wanakuta waganga hawapo. Naiomba Serikali kupitia Bunge lako Tukufu waganga wawe wanabadilishwa kwa zamu, wanapokwenda kufuata mishahara yao watafute utaratibu wa jinsi ya kufanya ili wananchi wasiendelee kupata shida.

Mheshimiwa Spika, miundombinu nayo vilevile inasababisha hospitali nyingine kuweza kukosa huduma, kwa mganga akipelekwa sehemu ambayo hakuna barabara anabebwa kwa baiskeli, na wakati mwingine kama ni mnene kama mimi baiskeli hawezi kupanda, anakataa kabisa anasema siwezi kwenda. Kwa sababu hiyo, utakuta mama amejifungua, anatembea kwa mguu. Amemaliza kujifungua anatembea kwa miguu, kwa sababu barabara zile hazipitiki, na hata baiskeli nazo utakuta njia ni za makorongo. Kwa hiyo, barabara nazo zinachangia sehemu nyingine kuweza kukosa huduma.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, ninaomba pia kilimo kitupiwe jicho. Tunaomba wataalamu wapelekwe kwenye maeneo ili waweze kutufundisha kilimo na vilevile pembejeo ziweze kuwafikia wananchi mapema kabla ya msimu. Wananchi wana moyo wa kujituma, lakini wakati mwingine ucheleweshaji wa mbolea unawakatisha tamaa. Sasa wanapopanda bila mbolea hawawezi kupata mafanikio. Kwa hiyo, tunaomba Wizara ya Kilimo itufikishie mbolea vijijini mapema ili wananchi waweze kupata pembejeo hizo mapema kwa ajili ya msimu unaokuwepo wakati huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezeshwaji, tunaomba Serikali iwaangalie wananchi wale wanaoishi vijijini, isiwaangalie wale wananchi wanaoishi mjini. Wananchi wanaoishi vijijini wanaweza kuwezeshwa kwa njia mbalimbali, tukiwakopesha mbolea tukawapa muda wa kutosha wa kuweza kulipa taratibu wananchi wale wanaweza kujiinua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali iliangalie jambo hili ili wananchi nao wasikatishwe tamaa wawezeshwe kutokana na jinsi walivyo. Kwa sababu tulisipowasadia wale wananchi ambao wako vijijini tutawakatisha tamaa. Kwa hiyo, tuombe tu kwa kupitia *SACCOS, NMB* ziwasikie hata wale wanaotokea vijijini na si wa mjini tu. Nina imani kwa kupitia kwenye *SACCOS* wananchi watazidi tu kujiunga kwenye *SACCOS*, tunaomba basi pesa zile zinapotolewa na wale wanaoishi vijijini nao ziweze kuwafikia. Pengine itaonekana labda wenyewe wamechangia kidogo, lakini katika kidogo kile kile tusiwakatishe tamaa na wao tuwapatie kutokana na mafungu yao.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi mwitikio wa *SACCOS,* wameupokea na ninajua kwamba wataendelea kujiunga kwenye *SACCOS.* Tuombe sasa tusiwakatishe tamaa, tuwatie moyo na wao. Nina imani kabisa kuwa wataweza kujiunga kwenye *SACCOS* na niombe *NMB* na *CRDB* ziweze kubadili utaratibu waliokuwa wameweka ili wananchi wetu wasiweze kukata tamaa. (*Makofi*)

Lakini pia niombe Halmashauri zetu kwa kupitia watu wa ushirikisha waweze kwenda vijijini kuwahamasisha wananchi waweze kuendelea kujiunga katika *SACCOS*. Wananchi wengi elimu haijawafikia kwa hiyo, tunaomba hata Halmashauri nazo ziweze kutusaidia kuendelea kupeleka mafunzo kule vijijini kwa kupitia maafisa wa ushirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukifanya hayo tutaweza kupiga hatua lakini kama Halmashauri wataendelea kuwaachia labda Waheshimiwa Wabunge bila wao kutusaidia, sisi hatutaweza. Sisi hatutaweza bila wao, kwa sababu Halmashauri ndizo zilizo karibu na wananchi. Ndio maana kilio chetu kikubwa ni kuwawezesha madiwani kwa sababu wako karibu kabisa na wananchi, kazi hii ya kuwaelimisha wananchi wataifanya vizuri kabisa.
Kwa hiyo, tunaomba Serikali iwawezeshe madiwani ili nao waendelee kupeleka elimu kwa wananchi wetu wanaoishi vijijini, tukifanya hivyo wananchi wataweza kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, mimi ya kwangu yalikuwa ni hayo naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, asante. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku hii ya leo na mimi nimeweza kupata nafasi ili kuchangia machache niliyonayo. Pamoja na hayo napenda nitumie nafasi hii kwanza kwa majonzi makubwa kabisa na masikitiko kwa kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Amina Chifupa na ninaiombea faraja kwa Mwenyezi Mungu, tukisema kwamba Bwana alitoa na yeye ametwaa, jina la Bwana libarikiwe.

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Singida kwa upendo na umoja wao kwa kujitoa kwa dhati kabisa hasa wakati ule wa ajali ya basi la *Mohamed Trans* iliyotokea na kuua watu 26. Nawashukuru sana kwa moyo wao wa upendo kwa kujitoa kwa mashirika mbalimbali, madhehebu mbalimbali ya dini, wafanyabiashara, madaktari na wauguzi wote wa mkoa wa Singida.

Lakini pia nisiwasahau wale wamiliki wa mabasi makubwa pamoja na mabasi madogo yaani *minibus* na *taxi* ambao walijitolea kwenda kuwasaidia wale majeruhi bila ya malipo yoyote.

Lakini pia nimshukuru sana Mkuu wetu wa Mkoa, Jeshi la Polisi pamoja na Mkuu wa Wilaya, kwa umoja na upendo na huruma na kufanikisha mazishi yale, ninasema Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri ambayo imejitosheleza na hii inaashiria ni wapi tunapokwenda. Lakini niwaombe tu watendaji wasimwangushe, hotuba ni nzuri imejitosheleza, wazingatie yale yote ambayo yameainishwa ili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, yangu mimi ni machache ambayo napenda kuchangia, nataka nizungumzie hali halisi ya mkoa wa Singida. Mheshimiwa Waziri Mkuu , hivi karibuni ninamshukuru sana, alitembelea Mkoa wa Singida na yeye mwenyewe amedhihirisha kuwa Mkoa wa Singida ni wa mwisho kiuchumi. Hii inasikitisha sana lakini ndio ukweli.

Sasa basi maoni yangu, kwanza, napenda kuwaambia kwamba wananchi wa Mkoa wa Singida ni wachapa kazi, na Mkoa wa Singida una rasilimali nyingi ambazo zinaweza zikaufanya mkoa ule ukawa si wa mwisho tena bali ukawa wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie upande wa Kilimo. Mkoa wa Singida ambao unarutuba, una maeneo mengi ambayo yanaweza yakalimwa mazao ya biashara na chakula, kwa mfano zao la alizeti linastawi sana katika Mkoa wa Singida lakini wananchi wake wamekuwa wakikata tamaa kulima zao hilo kutokana na miundombinu na viwezeshi. Sasa basi niiombe Serikali ianzie kwenye kilimo kuuinua uchumi wa Mkoa wa Singida, kuufanya mkoa huo uweze kujitegemea wenyewe. Kuna Maafisa Kilimo ambao wanatoka *SUA* , na nimesikia kuwa karibu watapata ajira baada ya kumaliza masomo yao. Serikali inatazamia kuajiri maafisa kilimo wengi sana, sasa niiombe Serikali kwa kuusaidia Mkoa wa Singida maafisa Kilimo hawa wawaajiri na kuwaleta wengi sana katika Mkoa wa Singida hasa kila Kata kuwe na afisa kilimo kuweza kusaidia uchumi kwa kila Kata.

Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, na kwa sababu ulifika Singida, umeona mwenyewe hali ilivyo, sisi tuko tayari tunataka tuanzie kwenye kilimo. Naomba sana utusaidie kila kata iweze kupata Afisa Kilimo. Lakini pamoja na hayo haitatosha kupata Afisa Kilimo tukaishia hapo, kwa sababu wananchi wataitikia kama nilivyosema ni wachapa kazi, wataitikia , watalima vizuri na mazao yatastawi Mungu atawajalia lakini miundombinu ya vijijini ni lazima iboreshwe. Kwa hiyo, naiomba Serikali iuangalie Mkoa wa Singida kwa jicho la huruma, ili miundombinu kutoka vijijini iweze kusafirisha mazao yatakayokuwa yamepatikana.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na miundombinu, Mkoa wa Singida unajiandaa kuanzisha chama cha ushirika lakini ni katika hali ngumu sana kutokana na

hali ya kiuchumi hasa tukizungumzia masuala ya pesa. Hivyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuomba sana kwa kupitia Wizara ya Kilimo kuuwezesha Mkoa huu uweze kuanzisha chama cha ushirika ili kuweza kuwakomboa wakulima wa Mkoa wa Singida na kuinua uchumi wa Mkoa huu. Aidha, jitihada zifanyike kutenga fungu la kutosha, kuupa Mkoa wa Singida fedha za kutosha kuweza kuanzisha chama cha ushirika ambacho kitakuwa ni mkombozi kwa mkulima wa Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, lakini pia pamoja na uanzishwaji wa chama cha ushirika bado tunavyo viwanda vidogo vidogo ambavyo vinakamua mafuta ya alizeti, viwanda hivyo vina uwezo wa kufanya kazi saa ishirini na nne, lakini wale wamiliki wa vile viwanda bado Serikali haijawawezesha vya kutosha, wale ni wakombozi wa wananchi. Tunaiomba sana Serikali kupitia mabenki, maana huwa wanasumbuliwa sana kwenye benki zetu, iwasaidie ili waweze kukopeshwa waweze kununua mazao kutoka kwa wananchi. (*Makofi*)

Tunacho kiwanda Shelui, Ndago, Iguguno, Singida Mjini na sehemu nyingine mbalimbali za mkoa wa Singida, tunaomba sana wawekezaji hao wa viwanda hivi vidogo vidogo na wenyewe wawezeshwe. Lakini bado tunaiomba Serikali iweke mikakati basi ya kutusaidia ili tuweze kupata hata soko kwa ajili ya mifugo iliyopo katika Mkoa wa Singida. Huku kung'ang'ana na matenga kila siku Singida- Dar es Salaam, Singida-Arusha; kwa nini kuku hawa, kwa nini mifugo hii isiuziwe pale pale Singida? Kwa hiyo, tunaiomba sana itusaidie ili tupate mwekezaji ambaye anaweza akatusaidia kutupatia soko la mifugo yetu ili kuku waweze kuuzwa katika Mkoa wa Singida na watu watafuga kwa wingi sana na kuondoka na hii hali ambayo tumeisema.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumze kwa watu binafsi. Mkoa wa Singida pia katika utalii ukienda kwa Waziri wa Maliasili na Utalii yeye anaelewa vizuri zaidi, kwa hiyo, ninaomba sana watu binafsi, watu mbalimbali, wafanyabiashara wadogo wadogo wawezeshwe ili waweze kuinua sekta hii ya utalii katika Mkoa wa Singida ili uweze kuwa na hali ya kuvutia tupate wawekezaji zaidi na watu watakaotembelea Mkoa wa Singida. Ikumbukwe pia tuna madini, hivyo, tunaomba hata sekta ya madini iuangalie Mkoa wa Singida kwa jicho la huruma kuwawezesha hata wachimbaji wadogo wadogo kuleta wakezaji pia ili mkoa wetu uweze kuinuka.

Lakini labda nizungumzie tatizo lingine linalofanya Mkoa wa Singida uweze kusuasua na hatimaye kuwa wa mwisho. Mkoa wa Singida ni mkubwa sana, ukichukua wilaya zake jinsi zilivyokaa, jiografia ya Mkoa wa Singida ni matatizo. Tuchukue mfano wilaya ya Manyoni, ina ukubwa usiopungua *square* kilomita 28,000, sasa hii ni sawa na Mkoa wa Kilimanjaro wenye wilaya sita, au Halmashauri sita. Kwa hiyo, ukimchukua *DC* wa Wilaya ya Manyoni anayehudumia wilaya nzima, *DC* mmoja ni sawa na Wakuu wa Wilaya sita wa Kilimanjaro. Ukichukua Mkurugenzi wa Wilaya ya Manyoni ni sawa na Wakurugenzi sita wa Mkoa wa Kilimanjaro. Najua utasema habari ya idadi ya watu, lakini bado kuna mikoa mingine imepewa wilaya zina watu laki mbili. Kwa hiyo, tafadhali ninaomba sana kuugawa Mkoa wa Singida katika Wilaya zitakazotosheleza au

Halmashauri ili kuweza kusaidia kuinua uchumi wa Mkoa wa Singida. Tafadhali sana Waziri Mkuu ninakuomba hilo.

Lingine nizungumzie na upande wa Afya. Upande wa Afya imekuwa ni tatizo. Nimepata habari kwamba Daktari Bingwa wa magonjwa ya wanawake (uzazi) ameripoti juzi. Sina hakika, lakini Mheshimiwa Waziri naomba niwe mkweli, kwa sababu mwaka jana niliongelea kuhusu angalau kuwe na daktari mmoja atakayeokoa maisha ya kinamama wakati wa uzazi, lakini mwaka mzima umekwisha hakuna kilichofanyika, kana kwamba Singida haipo Tanzania! Mimi nilipanga kwenye hotuba ya Wizara ya Afya nikawakusanye wale wanawake wajawazito wote waje wakae kwenye *gallery* huku ili Waziri wa Afya awahakikishie usalama wa maisha yao wakati wa kujifungua, wanapata tabu sana. Nina mdogo wangu ni mjamzito, sasa hivi ni taabu mzigo ule umekuwa ni wa kwangu, inabidi kumpeleka Itigi, kuhangaika. Kwa hiyo, tafadhali naomba kama daktari huyo amesharipoti basi afike kwa muda muafaka na sisi tuko tayari kumpokea, na tunalishukuru hilo kama Serikali imefanya hivyo ahsante sana.

Pia naomba nizungumze kuhusu Barabara ya Manyoni – Isuna. Sielewi kama kulikuwa na *tender* au zabuni, sasa naomba niambiwe Barabara hii inashughulikiwa vipi maana yake kile kipande kisije kikasahaulika, tunaomba tuhakikishiwe Barabara hiyo kama ni *tender* au zabuni imefikiwa wapi na itaanza lini? Ni vizuri kumpa mtu ambaye sasa hivi yuko kwenye *site,* usije ukampa mtu ambaye yuko maili kama 2000 au 3000. Mpeni mtu ambaye yupo kwenye *site* kama KONOIKE ili waendelee kwa sababu wapo pale ili Barabara ile iweze kwisha mapema. Lakini namshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia kuitangaza Tanzania katika ukurasa wa 64, kwa kuwataka Watanzania walioko nje wafanye hivyo. Mimi nafurahi sana kwamba hilo Waziri Mkuu ameliona lakini naomba kwamba Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje iangalie yale majengo yaliyopo katika Balozi zetu, kuna Balozi nyingine zinatia aibu haziitangazi Tanzania jinsi ilivyo. Majengo mengine ni mabovu kwa hiyo yakakarabatiwe ili sura ya nchi yetu isije ikaonekana ya ajabuajabu. Ukienda ubalozi wa Ufaransa wao wamepanga kwenye Jumba la Ubalozi wa Uganda, sasa wenyewe wamejibanza tu pale, hiyo sura ya nchi yetu kidogo inakuwa si nzuri. Kwa hiyo, ninaomba pia ili kuitangaza nchi yetu vizuri basi Balozi zetu, watu wetu na nyumba zao wanakoishi ziboreshwe ili tuweze kuitangaza nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kabisa, kuhusu suala la maji, sitazungumza bali ninaomba nimwalike Mheshimiwa Dr. Jumanne Shukuru Kawambwa niongozane naye kwenda Singida ili akajionee mwenyewe, tuanzie Mpapa twende Ndago na maeneo ambayo ninayajua kwamba yana ukame ili yeye aweze kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza, pia naomba nizungumzie kuhusu Bodi ya Mikopo juu ya kuzuiwa kwa wanafunzi kufanya mitihani. Bodi hii inafanya kazi vizuri lakini Wizara iongezewe pesa, kwa sababu ile 40% inatesa sana wanafunzi. Sasa naomba sana Serikali iangalie Wizara ya Elimu ya Juu kwa sababu maendeleo ni elimu, wanafunzi wanapoingia darasani wameshalipiwa 60% halafu baadaye hawatakiwi tena kufanya mitihani kwa sababu ya 40%, hii inakuwa ni matatizo.

Mheshimiwa Spika, mimi sina zaidi, ninaomba kuunga mkono asilimia mia moja hotuba hii ya Waziri Mkuu.  Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumza na kuchangia mchango wangu katika hotuba ya Waziri Mkuu ambayo inaelezea taarifa ya utekelezaji wa kazi za Serikali.

Kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kigoma Kaskazini na kwa kuwa mimi ni miongoni mwa Wabunge vijana, kwa niaba ya vijana wote wa *Tanzania Across Political Parties,* napenda nitoe rambirambi zangu za dhati kwa msiba uliotupata wa Marehemu Amina Chifupa na ninaamini kabisa kwamba Mwenyezi Mungu atamuweka Mahali Pema Peponi, Amin!

Mheshimiwa Spika, nina masuala kama matano ambayo napenda kuyazungumzia kuhusiana na hotuba ya Waziri Mkuu. Mawili ni masuala ya Jimbo na yaliyosalia ni masuala ya kitaifa kwa ujumla wake na moja ni suala la Mambo ya Nje ambayo naamini kwamba nikifikisha kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu anaweza akayafayia kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza la kijimbo ambalo ningependa kulizungumzia, ni shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Alifanya ziara mwaka jana katika Mkoa wa Kigoma na akapita jimboni kwangu na nikampeleka katika kinu chetu cha kukoboa kahawa kule Matyazo. Tulikuwa na tatizo la *re–fund* ya *VAT* ambayo wananchi walikuwa wamenunua mtambo wakawa wametozwa *VAT,* Waziri Mkuu akaahidi kulitekeleza na napenda kumthibitishia kwamba agizo lake lilitekelezwa na tayari ile pesa imerudishwa kwa hiyo tunakushukuru sana kwa hilo. (*Makofi*)

Kwa taarifa tu zaidi ni kwamba inawezekana safari yako ilifungua mambo mengi zaidi kwani sasa hivi wakulima wa kahawa ukanda wote wa juu wa wilaya zote yaani Kasulu na Wilaya ya Kigoma kwa maana ya Jimbo la Kigoma Kaskazini yaani Kasulu Magharibi na Kasulu Mashariki soko la kahawa kwa sasa hivi siyo tatizo. Mwaka jana tumepata bei nzuri zaidi kuliko wakulima wote wa kahawa Tanzania na tumepata mradi mkubwa sana ambao unafadhiliwa na Shirika la *Sustainable Harvest* la Marekeni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunazalisha kahawa iliyo bora ambayo itakuwa na bei nzuri na tutai–*plant* kwa kuiita **Kahawa ya Gombe**. Kwa hiyo, naomba Serikali iendelee kutoa ushirikiano wa karibu kwa wakulima wa kahawa wa Mkoa wa Kigoma ili tuweze kwa kweli kuhakikisha kwamba tunaondoa umaskini kutokana na zao hili la kahawa.

Pia napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba alipita katika Kijiji cha Mahembe ambacho mwaka jana kulikuwa na tatizo la shule ya Sekondari, akaahidi kuchangia na Mheshimiwa Waziri Mkuu ule mchango ulifika, shule imekwisha na sasa hivi watoto wanasoma. Kwa hiyo, na hilo nalo napenda nitoe shukrani zangu za dhati.

Mheshimiwa Spika, kuna hili suala la maji ambalo kuna mzungumzaji mmoja amelizungumzia. Ni kweli kabisa kwamba kuna tatizo la maji Kigoma lakini kwa kushirikiana na Halmashauri, Serikali na nchi za Jumuiya za Ulaya kupitia mradi wa *EU Water Facility* tumejitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kuhakikisha kwamba suala hili linapungua.

Tatizo kubwa lililopo ni pale Mwandiga ambapo wananchi bado hawajapata maji kwa sababu Mradi wa Maji wa Mkongoro bado ni mdogo, unahitaji kupanuliwa lakini mwaka huu tulipata ziara ya Balozi wa Marekani ambaye alitembelea katika Jimbo la Kigoma Kaskazini na tumekubaliana na Serikali ya Kijiji kuweza kupanua ule mradi kwa msaada wa Serikali ya Marekani ili kuhakikisha tatizo hili la maji pale Mwandiga linakamilika. Haya yote yanawezekana kwa sababu ya mahusiano yetu mazuri kati ya nchi yetu na nchi nyingine kiasi kwamba Mabalozi wa nchi marafiki wanaweza wakatusidia katika masuala mbalimbali. Hayo ni masuala ya kijimbo.

Mheshimiwa Spika, masuala ya kitaifa. Suala la kwanza ambalo napenda kulizungumzia ni suala la Wanafunzi wa *UKRAINE*. Mtakumbuka kwamba katika Bunge hili, Mheshimiwa Halima J. Mdee alileta swali na.52 hapa Bungeni kama nakumbuka vizuri, na tukapata majibu kutoka Serikalini ambayo kwa kweli sidhani kama yanakidhi haja kwa sababu katika majibu yao Naibu Waziri na Waziri walionekana kupingana kwa sababu Naibu Waziri alisema kwamba Serikali katika mwaka 2006/7 haimkufadhili mtu yeyote nje na Waziri akasema kwamba walipata ufadhili, majibu yote haya yapo kwenye *Hansard* ya tarehe 20 Juni.

Mheshimiwa Spika, naona kuna tatizo kubwa sana nitaliongelea hili pia. Kuna tatizo kubwa sana la uratibu katika Serikali na nimeona niliongee hili kwa sababu Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo yenye jukumu la kuratibu Wizara zote. Inapotokea Waziri na Naibu Waziri wanatoa majibu ambayo yanapingana ina maana kwamba huo uratibu unakwenda kwenye ngazi ya Wizara.

Kwa kweli kufuatana na majibu ambayo Waziri wa Elimu ya Juu aliyatoa inaonyesha dhahiri kabisa kwamba alimpotosha Rais na ndiyo maana Rais alipokuwa anazungumza na Waandishi wa Habari pale Dar es Salaam majibu aliyoyatoa ni kama jinsi ambavyo Waziri alivyozungumza.

Kwa hiyo, kuna vitu ambavyo Wizara ya Elimu ya Juu haikumfahamisha Rais kuhusiana na suala zima la Wanafunzi wa *UKRAINE* kwa sababu wale wanafunzi walipewa mkopo na waliingizwa kwenye mikopo lakini ile mikopo haikupelekwa na kulikuwa kuna mawasiliano kati ya Serikali ya Tanzania na chuo ambacho wale wanafunzi walikuwa wanasoma, mawasiliano amabayo sasa hivi Serikali inayakataa.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nasononeka sana kwa sababu nafahamu kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mtu ambaye anataka kuhakikisha kwamba Mtanzania hapati tatizo lolote. Lakini kwa kuwa yeye anafanya kazi kufuatana na mfumo wa Serikali anachotaarifiwa na Wasaidizi wake ndicho hicho ambacho anakizungumza.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba pitia majibu ambayo Naibu Waziri aliyatoa kwa msaada wa Wataalamu; pitia majibu ambayo Waziri wa Elimu ya Juu aliyatoa kufanya *reference* na taarifa ambayo Rais aliizungumza na Waandishi wa Habari, utagundua kabisa kwamba kuna tatizo katika Wizara ya Elimu ya Juu na kwa vyovyote vile mimi ningekushauri tu Mheshimiwa Waziri Mkuu uangalie ni jinsi gani ya kuweza kutatua tatizo hili kwa sababu limepelekea hata matatizo mbalimbali ambayo sasa hivi

tunayapata kutokana na migomo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu. Kutokana na rekodi zilizopo, Wizara kwa sasa imepata matatizo mengi sana ya migomo kwa sababu ya maamuzi ambayo si sahihi na maamuzi ambayo pia hayazingatii ushauri mbalimbali ambao wadau mbalimbali wa elimu ya juu wamekuwa wakiyatoa.Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hili suala la watoto wa *UKRAINE* tuliangalie upya kwa sababu inawezekana kabisa fedha ambazo Serikali ilitenga kwa ajili ya kulipia watoto hawa zimeliwa, inawezekana kabisa. Naomba Ofisi ya Waziri Mkuu iweze kuliangalia na watu wanaohusika na Wizara ya Elimu ya Juu waweze kutoa masuala yanayotakiwa.

Suala la pili la Kitaifa ambalo nataka kulizungumzia ni suala la Madini. Nilikuwa napitia hapa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu akizungumzia maendeleo mbalimbali ambayo tumeyapata kutokana na migodi ya madini likiwemo suala zima la kufanya migodi hii ianze kulipa kodi mapema kwa kulegeza baadhi ya vipengele vya mikataba likiwemo suala la Halmashauri za Wilaya ambazo ndani yake kuna migodi kuweza kulipwa dola 200,000/= kila mwaka. Likiwemo pia suala la Kampuni ya *Barrick* kuanza kulipa kwa hiari dola milioni 7 na vilevile Kampuni ya *Resolute Tanzania Limited* kuanza kulipa dola milioni 2 kwa halali.

Ukiangalia maelezo haya ambayo Waziri Mkuu ameyasoma, utagundua kabisa kwamba tuna tatizo la kuonekana kwamba sisi ni watu wa kuhurumiwa siyo watu ambao tuna haki zetu ambazo tunapaswa kuzipata, nitatoa mfano: Makampuni haya ya Madini wamekubaliana na Serikali kuanza kulipa dola 200,000/= kila mwaka kwenye zile Halmashauri ambazo zina migodi. Lakini swali ambalo ni la msingi sana la kujiuliza ni kwamba ni *formula* gani ilitumika, yaani tulitumia *formula* gani kuweza kuhakikisha kwamba hizi dola 200,000/= zinalipwa kwa sababu bei ya madini inabadilika katika soko la dunia. Mfano, sasa hivi bei ya dhahabu iko juu sana na hizi dola 200,000/= ni mikataba ya zamani kwa hiyo hakuna *base* yoyote. Kwa hiyo, utakuta kwamba kama tungeweza ku *–pack a certain formula* kwa ajili ya hizi Halmashauri kufaidika na ile migodi ambayo ipo katika maeneo yao wangeweza kupata zaidi ya dola 200,000/=.

Kwa hiyo, naomba ili lisionekane kama ni mafanikio kwa sababu inaonekana kama tunawaomba hawa watu wenye migodi ninashauri kwamba suala hili liangaliwa upya ili tuweze kuwa na *formula* ambayo itaendana na mauzo ya madini yanavyokwenda katika soko la dunia. Kama mauzo yakishuka tupate kidogo lakini kama mauzo yakiwa makubwa zaidi tuweze kupata kutokana na thamani ya dhahabu katika soko la dunia. Hata hili suala la kampuni ya *Barrick* kujitolea kulipa dola milioni 7 kila mwaka, hapa tuna tatizo kwa sababu mara baada ya Serikali kukubaliana na migodi kuhusiana na suala la kulipa hizi dola milioni 7 kila mwaka ilichokifanya Kampuni ya *Barrick* ni kuunganisha migodi yake yote mitatu iliyopo nchini kuiweka chini ya Kampuni moja. Kwa hiyo, mgodi wa Tulawaka, Bulyankhulu na Mgodi wa *North Mara* ambao waliununua kutoka kwa *East African Gold Mining* na sasa hivi wana mgodi mpya wa Buzwagi wataendelea kutoa hizo hizo dola milioni 7 hata wakipata mgodi mwingine. Kwa hiyo, ndiyo *trick* ambayo Serikali nadhani haikuiona kwa sababu ilitakiwa hawa watu wa migodi walipe kutokana na migodi siyo……!

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu!

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa kulisaidia tu Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla, hayo anayoyasema Mheshimiwa Kabwe ni kweli Kampuni ya *Barrick* imezinunua hizi *North Mara, Plesedom* na hii ya Tulawaka.

Lakini kwa makusudi ya ulipaji wa kodi kwa mujibu wa Sheria kuanzia madini yenyewe lakini pia kwa Sheria ya Mapato ya kodi ya Tanzania, kodi inalipwa kwa kila mgodi hakuna *consolidation,* ni vizuri tu hilo likaeleweka ili wote tumsikilize vizuri anayechangia ili tumwelewe.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante kwa taarifa hiyo, kwa kuwa ni taarifa Mheshimiwa Zitto endelea!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, naendelea lakini Mheshimiwa Waziri hakunisikia vizuri. Sijajenga hoja yoyote kwenye kodi, suala la kodi sijalizungumzia kabisa, nimezungumzia suala la michango inayoitwa ya hiari ya dola milioni 7 kwa makampuni ya Madini.

Katika hali ya kawaida wakati Serikali inafanya *negotiations* za mwanzo ilikuwa ni dola milioni 5 kwa kila mgodi, kwa hiyo, kwa kampuni ya *Barrick* peke yake tungepata dola milioni 5 kutoka Bulyankhulu, North Mara na Tulawaka.

Lakini wakati mazungumzo yanaendelea *Barrick* wakakusanya migodi yao yote wakaiweka chini ya Kampuni moja na wakitoa taarifa yao ya Mapato na Matumizi yaani *Book Keeping and Accounts* zozote zile. *Financial Statements* zao wakizitoa siyo za kila mgodi, wanatoa *Financial Statement* ya kampuni moja na wana mgodi mpya wa Buzwagi. Kwa hiyo, tunaendelea kupoteza dola milioni 5 tukichukulia kwamba makubaliano yale ya Serikali yangeweza kuwepo. Kuna tatizo! Mimi ninachoiomba tu Serikali isikimbilie kutujibu, ilifanyie kazi, kuna tatizo katika eneo hilo. (*Makofi*)

Masuala mawili ya mwisho. Kwanza, ni suala la ushauri kuhusiana na ubalozi wetu wa *Brussels*. Ubalozi wa *Brussels* una kazi nyingi sana, unahudumia zaidi ya nchi tatu lakini pia Ubalozi huo unashughulikia *European Commission,* Tume ya Ulaya. Kwa hiyo unakuta Balozi ana wasaidizi wawili, anakuwa na mzigo mkubwa sana. Sasa nashauri kuwa Serikali ijaribu kuangalia kama tutakuwa na *special representative* katika *European Commission* kwa sababu tuna miradi mingi sana ambayo tunaipata kutoka *European Commission.*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni suala la *BoT*. Suala hili limeleta *debate* kubwa sana hapa Bungeni kiasi kwamba ikapelekea hata kuhamisha mazungumzo yaani *debate* ya kina kwenye ofisi ambayo inachangiwa na jamii nzima, sasa hivi inakuwa ikisikiliza tu suala hili la *BoT* na imepelekea hata baadhi ya Wabunge kuanza kujibishana.

Tatizo lililopo ni kwamba taarifa zinasambaa kuhusiana na ubadhirifu, taarifa hizi Serikali inazipata, kinachoniumiza mimi ni kwa nini Serikali haichukui hatua za haraka

kuweza kushughulikia masuala haya mpaka yanazungumzwa Bungeni yanakuwa ni *public.* Ukweli ni kwamba masuala kama haya yana-*tarnish image* ya nchi, yana *tarnish* sana *image* yaani kuna *problem* ya *communication* katika Serikali. Kwa hiyo, mimi naiomba …….!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu!

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Spika, naomba tu kutoa taarifa kwamba si kweli kwamba hakuna hatua zilizochukuliwa kabla ya kuja kujadiliwa hapa Bungeni na wewe ni shahidi, wakati Mheshimiwa Rais alipoitisha Mkutano wa Viongozi wote Wakuu na wewe ulikuwepo katika mkutano huo. Lakini pia taarifa mbalimbali na mikutano mbalimbali ilifanyika katika ngazi mbalimbali kuonyesha umuhimu wa kuwa na utaratibu mzuri na kurekebisha hali iliyokuwepo na *CAG* amechukua hatua kabla ya kikao hicho kwa wale wote waliokuwa wanahusika na hatua zaidi zitaendelea kuchukuliwa. Naomba kutoa taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabwe umeipata hiyo taarifa?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi naomba watu wa *front bench* ya upande wa pili wasiwe wanajiandaa kuwajibu Wabunge kwa sababu *Chief Whip* yupo upande wa pili hata alikuwa hajui nitakachozungumza yaani kitakachofuata ni nini. Ingewezekana kabisa kikawa kinaisaidia Serikali katika suala hili ambalo linaendelea. Kwa hiyo, nadhani tujenge tu utamaduni wa kusikiliza zaidi na kwa sababu kuna muda wa kuweza kujibu hizo hoja basi waweze kuzijibu.

Mheshimiwa Spika, lakini nilichokuwa nataka kukizungumza ni kwamba hali ilivyo sasa hivi, *public opinion* ilivyo ni kwamba Benki Kuu kuna tatizo. Inawezekana hakuna tatizo; inawezekana kabisa kwamba tuhuma ambazo zilisambazwa katika mtandao na zikazungumzwa hapa Bungeni kwa nia njema kabisa na Msemaji wa Upinzani kwa upande wa Ofisi ya Waziri zilikuwa ni tuhuma ambazo Serikali ingeweza kuzifanyia kazi kwa haraka. Na wala zisingefika hapa kwa sababu kitu ambacho kinazungumzwa Bungeni kinachohusu Benki Kuu, Benki Kuu ikitokewa na tatizo lolote mtaanza kuona tatizo kwenye *financial system* ya nchi jinsi itakavyokuwa.

Kwa hiyo, mimi nashauri tu kwamba tuwe wepesi sana katika *communication strategy* yetu kama Serikali kuweza kuhakikisha kwamba masuala kama haya yanazungumziwa kwa haraka. Kwa sababu kwa taarifa tu ni kwamba ile *dossier* iliyosambazwa ambayo Mheshimiwa Dr. Slaa aliizungumzia hapa ilikuwa kwenye mtandao wa *internet* toka mwezi wa saba mwaka jana. Sasa kuna mambo mawili, aidha, Serikali iliifanyia kazi kimyakimya na ingeweza kutoa *brief* kwenye Bunge *or else* Gavana aliachiwa aji – *hang* mwenyewe, inawezekana kabisa. Kwa hiyo, mimi nashauri

kwa Serikali kwamba suala kama hili lingeweza kuangaliwa kwa sababu kwa mfano, hata suala la Mbunge kuweza ………….!

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Hapo hapo ulipomalizia kwa siku za usoni Spika atakuwa mwangalifu sana na hizi taarifa za *Internet* kuletwa humu kwa sababu zinatuvushia mjadala mkubwa sana hilohilo tunalolihofu la ku-*tarnish* nchi lisipitie mkondo wa *anonymous internet messages*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge muda uliosalia ni dakika tisa tu na hauruhusu tuweze tukaendelea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, nimemwona sasa hivi ambaye hakuwepo mwanzoni anatokea Njombe kwenye mazishi, nitampa nafasi yake saa za jioni.

Kwa taarifa tu tunaweza kuwasikiliza kwa dakika 15 Waheshimiwa Wabunge 11 kwa kipindi cha jioni. Kwa hiyo, katika orodha yangu mpya ambayo tutaitoa hivi punde naomba niwasome kwa sababu ni vizuri watu wajiandae. Ni dhahiri hatuwezi kuwa na wote na kwa kuwa hatuwezi kuwaruhusu wote waliojiandikisha kwa sababu mbalimbali, nimeweza kupata wafuatao: Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye atakayeanza saa 11 jioni, Mheshimiwa Manju Salum Omar Msambya, Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa John Magale Shibuda, Mheshimiwa Thomas Abson Mwang'onda, Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu na Mheshimiwa Mussa Azan Zungu.

Nimeongeza na wengine, kwa kutazamia sijui kinaweza kutokea kitu gani lakini; au mtu mmoja anaweza kuchangia kwa kufupi, nao ni Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa.....! Nimemruka Mheshimiwa Prof. Feethan Filipo Banyikwa, aniwie radhi kwa sababu nilivutiwa na jina la Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya ambaye atakuwa anachangia kwa mara ya kwanza. Hayo ndiyo majina ya jioni na tutakwenda kwa utaratibu huo...! Nilimruka Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, naye atakuwa ni wa pili kwa Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye.

Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo fupi, kwamba leo Mheshimiwa Waziri Mkuu mnamo saa nane atazindua mashindano ya kitaifa ya riadha kwenye uwanja wa Jamhuri. Kwa hiyo, wale wote wapenda riadha na Waheshimiwa Wabunge wengine, tukitambua kuwa wanariadha wametoka mikoa yote, hata kisiasa ni vizuri tu kuwepo pale, unaweza kukuta wapiga kura wako ndiyo baadhi ya wakimbiaji, warusha tufe na kadhalika kwa hiyo ni vizuri kuwapo. Mashindano yatakuwepo leo na pia hata kesho, kwa hiyo, nyote mnaalikwa kuwaangalia vijana wetu.

Baada ya hayo na kwa kuwa muda wenyewe ndiyo huo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi kwamba nimebakiwa na muda gani maana nimeingiliwa sana.

**SPIKA:** Wakati wote saa huwa inasimamishwa, kwa hiyo, una dakita tatu tu!

*(Saa 06:55 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangaza tutaanza na Mheshimiwa Mariam Kasembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye wakati huo Mheshimiwa Shally Raymond, ajiandae.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu inayohusu hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Bajeti ya mwaka 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaanza kuchangia nami naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Ofisi ya Spika, kwa kazi kubwa ambayo imefanya ya kuandaa shughuli za mazishi za mwenzetu Marehemu Amina Chifupa, ambaye alifariki dunia na kuzikwa hapo jana. Mimi ni mmojawapo ambaye nilipata bahati ya kwenda kwenye mazishi kijijini kwake. Tunamshukuru Mungu tulimzika salama na tumeweza kurudi salama. Kilichobaki sasa tukae na kumwombea mwenzetu ili Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu Amina Chifupa, mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, suala la pili, naomba nishukuru kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeelezea mambo mengi ambayo yanatakiwa kutekelezwa katika mwaka 2007/2008. Lakini nishukuru zaidi pale ambapo umeandaliwa mpango kabambe wa kutekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais pamoja na za Waheshimiwa Wabunge ambazo tuliahidi wakati wa Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa sehemu kubwa hizo ahadi ndiyo kero kubwa ya wananchi kwenye maeneo ambayo tunatoka. Kwa hiyo, naomba sana katika Bajeti yetu lile tulilokusudia kulifanya, basi tulitekeleze ili kero hizo kwa wananchi ziweze kuondoka.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nianze kuchangia kwenye hotuba katika sekta ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, utaona mara kwa mara sisi Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Kusini kila anayesimama ni lazima achangie katika Sekta hii ya Miundombinu. Hii ni kwa sababu lile suala ambalo tunalilia kila siku kuhusu barabara ya Kibiti - Lindi mpaka hivi sasa haijakamilika. Kwa hiyo, sisi kama wawakilishi wa wananchi bado tunakuwa na wajibu mkubwa kila tunapopata nafasi ya kuchangia hoja hii ili Serikali kuipa msukumo iweze kumalizia maeneo yaliyobakia na sisi tuweze kupata barabara

nzuri ili wananchi wetu waweze kuondokana na tatizo kubwa wanalolipata la usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba tatizo hili ni la muda mrefu. Tangu Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania lilipoanza kila Mbunge aliyechaguliwa kuingia katika Bunge amekuwa akizungumzia suala la barabara ya Kibiti hadi Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, basi ukiangalia tunaweza tukasema sasa imekuwa ni kama ajenda ya kudumu kwa Waheshimiwa Wabunge tunaotoka Mikoa ya Kusini. Tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tatu ambayo yenyewe kwa makusudi mazima kwa kuona kero hiyo ilianza kutekeleza suala la ujenzi wa barabara hiyo. Tunashukuru kwa ujenzi wa daraja, kwa sasa kwa kweli tunapita bila wasiwasi wowote. Kwa hiyo, tunaomba kabisa Serikali hii ya Awamu ya Nne maeneo yaliyobakia basi iyamalizie ili hii ajenda ya kila Mheshimiwa Mbunge anayesimama kudai barabara ya Kibiti - Lindi ifungwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Serikali ya Awamu ya Tatu walishaifungua kwa kutengeneza barabara hii, tunakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atupelekee salamu zetu kwa Mheshimiwa Rais kwamba tunamkabidhi ile barabara kabla hajamaliza kipindi chake aifunge hiyo ajenda ili na sisi Waheshimiwa Wabunge wa Kusini tupate muda mzuri wa kuweza kuchangia mambo ya Kitaifa. Kutokana na muda mdogo tunaoupata wa kuchangia hapa Bungeni, tunajikuta kila tukisimama tunachangia jambo moja.

Kwa hiyo, tunawaomba sana watufungie hii ajenda, tuna mambo mengi ya kuchangia ya Kitaifa, tuna mambo mengi ya kuchangia yanayowakabili wananchi wetu kule Kusini. Lakini hatupati muda huo kwa sababu bado tunaona tuipe msukumo Serikali kuweza kumaliza barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati kikao cha Bunge safari hii kikiendelea Mheshimiwa Raynald Mrope, aliuliza swali hapa Bungeni. Lakini Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu alipojibu alitueleza kwamba barabara hiyo itakamilika mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naiomba Serikali ifanye jitihada zote kwa maeneo yaliyobakia watoe msukumo, wawezeshe ili barabara hiyo itakapofika mwaka 2009 iwe imekamilika ili mwaka 2010 tubakie na ajenda moja tu ya uchaguzi, mwaka 2010 pengine tukirudi tena tusije na ajenda ya barabara ya Kibiti – Lindi, ninaomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sambasamba na hilo la barabara sisi tunaotoka Mkoa wa Mtwara tuna eneo la barabara moja ya ulinzi ambayo inaambaa ambaa kwenye Mto Ruvuma. Barabara hiyo ilitumika sana wakati wa vita vya Msumbiji. Lakini katika barabara hii wananchi walilazimika kuhama ili kuiachia Serikali ifanye kazi zake za ulinzi katika maeneo yale ya mpakani. Lakini baada ya kumalizika vita wananchi wamerudi tena kule kwa hiyo, barabara hiyo wanaitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini cha kusikitisha ni kwamba wakati tulipopata vita vya Idd Amin, baadhi ya madaraja yalikuja kuchukuliwa kwenye barabara ile na kupelekwa Kagera baada ya kuharibiwa yale madaraja ya kule. Lakini baada ya kwisha vita madaraja hayo hayakurudishwa tena. Sisi wananchi wa Mkoa wa Mtwara tunasema nchi hii ni moja hatuna sababu ya kuidai Serikali kwamba yarudishwe madaraja yale na yanaendelea kubakia kule. Lakini napenda kuikumbusha Serikali kwamba kwenye yale maeneo ambapo yalichukuliwa madaraja bado kuko wazi wananchi wanapata shida, wanatembea kwa miguu hata wakati wa kampeni inabidi magari muyaache kwenye yale maeneo mnapita kwa miguu. Kwa hiyo, katika Bajeti zijazo, tunaomba sana Serikali ifikirie suala la kuyarekebisha maeneo yale ambapo madaraja yale yalichukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili, ambalo nataka kuchangia ni kuhusu kilimo. Kama nilivyoanza kuzungumzia kwamba sisi Waheshimiwa Wabunge tunaotoka Mikoa ya Kusini kila tukisimama tunakuwa na ajenda aidha ya Kibiti - Lindi au suala la kilimo hasa kwa upande wa zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umekuwa ukishuhudia katika Bunge hili jinsi ambavyo Waheshimiwa Wabunge tunaotoka Mikoa inayolima korosho tunavyokutana mara kwa mara kujadili hili suala. Mpaka sasa hivi Waheshimiwa Wabunge wenzetu hapa karibu wote wameshakuwa watani zetu. Tunavyotoka nje ya Bunge hawatuiti tena labda mama Kasembe, utasikia wewe mama wa korosho. Kwa maana kwamba kila wakati hili suala limeshazoeleka. Sielewi watu wanalitafsiri vipi, lakini nataka niseme kwamba sisi tunaotoka Mikoa inayolima zao hili la korosho hadi sasa zao hili halijapata ufumbuzi wa kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zao hili ni zao pekee ambalo sisi tunalitegemea, lingeweza kuondoa umaskini kwa wananchi wetu, lakini kwa masikitiko makubwa zao hili wananchi wanapata shida, bei haieleweki, pembejeo ni matatizo na wakati msimu unapofika hata bei zile ambazo tunakubaliana katika vikao vya wadau, hao wafanyabiashara wakubwa hawazifuati, matokeo yake wanakuwa wananunua korosho kinyemela kwa bei ndogo kitu ambacho kinawapelekea wananchi wetu kuendelea kuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali kwa kuwa wameshatwambia kwamba watatusaidia kuweka mikakati ya kuimarisha Ushirika, basi hilo suala lingefanyika haraka ili na sisi tuweze kujikomboa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ambalo mimi ningeweza kuiomba Serikali ni kwamba basi wanapopanga masuala ya ruzuku, ruzuku tuipate kwa wakati na ikiwezekana ile ruzuku tunayoipata ya Serikali basi tuongezewe kwa sababu mpaka sasa hakidhi mahitaji ya sisi tunaotoka kwenye Mikoa inayolima korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile kuna ushuru ambao kwa kweli ukiangalia ni haki yetu kupata kwenye Halmashauri zetu ule wa *export levy*. Lakini vile vile sielewi

ni kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi mara baada ushuru huo unapokuwa tayari kuturejeshea ili na sisi tuweze kupanga mikakati yetu na kuweza kuagiza pembejeo kwa wakati ili wakulima wetu waweze kunufaika na hilo.

Mheshimiwa Spika, katika suala la kilimo, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wote wa Halmashauri ya Mkoa wa Mtwara, Madiwani, Wakurugenzi, Maafisa Watendaji wa Kata, Watendaji wa Vijiji kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwahamasisha wananchi kwa sababu inafikia wakati wanataka kuliacha hili zao la korosho, wanakata tamaa kabisa hata palizi inakuwa ni matatizo. Lakini viongozi hao wa Wilaya wamekuwa wakisimama kidete kuwasimamia wananchi, kuwaelimisha wananchi na kuwahamasisha walielewe zao la korosho kwamba ndiyo zao pekee litakalowasaidia na wanafanya kazi katika mazingira magumu mno.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa wananchi wetu ni wasikivu kwa kweli wanajitahidi kuwasikiliza viongozi wao, lakini harakati hizi zote wanakuja kukatishwa tamaa pale msimu unapokuja kufunguliwa. Wanunuzi wakubwa hawafuati zile bei, hivyo kuwavunja moyo hao wenzetu katika kusimamia zao hilo. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali itufikirie na itutatulie tatizo hilo, tuache na sisi hapa Bungeni kukutana kila wakati Waheshimiwa Wabunge tunaotoka Mikoa inayolima korosho labda na sisi tutapata muda wa kukutana kujadili shughuli zingine za maendeleo siyo hili la korosho tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile nichangie kwenye sekta ya afya. Kwenye sekta ya afya tunaishukuru Serikali kwa kuwa sasa imeamua kwamba inaweza ikajenga zahanati kila kijiji. Naipongeza sana Serikali kwa sababu hili tatizo lilikuwa ni la muda mrefu na kujenga vituo vya afya kwenye kila Kata.

Mheshimiwa Spika, lakini sisi watu wa Mikoa ya Kusini tunalo tatizo kubwa sana la Hospitali ya Rufaa. Tunaishukuru Serikali yetu hili imeliona na kazi imeishaanza kufanyika vizuri, eneo liliishapatikana, wananchi wa maeneo yale wameishafidiwa. Sasa hivi kilichobakia ni Serikali kuanza utekelezaji. Tunaiomba sana Serikali suala la ujenzi wa hospitali hiyo ya rufaa utekelezaji wake uwe wa haraka kwa sababu wananchi wetu wanapata shida wanapotakiwa kutibiwa zaidi kwani ni lazima waje Muhimbili na barabara zetu ndivyo kama mnavyozisikia kila siku. Tunaomba sana utekelezaji wake uwe wa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchache wa fadhila kama sitazungumzia suala la Madiwani. Ninashukuru sana kwa kuwa Serikali imetamka kwamba viwango vya posho vya Madiwani itakuwa shilingi 60,000, mimi nashukuru. Lakini ningeomba Serikali kama itawezekana basi wangeweka wazi kwa zile Halmashauri ambazo wanao uwezo isiwe dhambi kuwaongezea posho Madiwani wao kwa sababu Madiwani hao sisi ndiyo tunaowategemea katika shughuli mbalimbali za maendeleo na wao ndiyo wanaosimamia shughuli za maendeleo. Lakini ukiangalia kwa kweli kwenye mazingira wanayoishi ni magumu, utendaji wa kazi kwao unawawia vigumu. Hivyo, ninategemea kwamba kama tungeweza kuwaongezea kiasi kidogo wao wenyewe pengine wangeweza kuchukua

jukumu na Halmashauri zao za kuweza kuwapatia hao wenzetu hata kama ni kwa mkopo vyombo vya usafiri ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho, ambalo mimi nataka kulizungumzia ni suala la maji. Suala la maji kwa Mkoa wetu wa Mtwara, tunazo Wilaya nne ambazo kwa kweli zina tatizo kubwa sana la maji ikiwemo Nanyumbu, Masasi, Newala na Tandahimba. Tunajua kwamba Serikali imeandaa mipango ya kuweza kutusaidia kutatua tatizo hili la maji. Lakini kwa kweli mipango hiyo inaenda taratibu mno na wananchi kule kwa kweli wanapata shida kubwa mno, akinamama wanapata shida, wanaamka usiku kwenda kutafuta maji, wanaacha nyumba zao, wanaacha waume zao, usiku kucha wao wapo visimani kutafuta maji. Tunaomba sana suala hili la maji mipango iliyopangwa katika sekta hii ya maji iweze kutekelezwa ili akinamama hao waondokane na hiyo kero ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nilitaka nizungumzie katika maeneo hayo manne, suala la barabara ya Kibiti - Lindi nimetoa salamu zangu kwamba tunaiomba Serikali ya Awamu ya Nne, itufungie ajenda hii ili tusisimame tena kudai barabara. Lakini nimesititiza tena suala la zao la korosho. Tunaiomba sana Serikali sisi ndilo zao tunalolitegemea, Mikoa inayolima korosho ni maskini, lakini tunaweza tukaondokana na umaskini huo kama Serikali ikisimamia vizuri kuweza kuboresha zao hili la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo ili na mimi niweze kuchangia machache katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba binafsi na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mbeya kuweza kutoa salamu za rambirambi kwa kifo cha Mbunge mwenzetu Marehemu Amina Chifupa, Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, pili naomba niipongeze Serikali kwa kutoa kipaumbele katika suala la elimu katika Bajeti yake ya mwaka 2006/2007. Najua kwamba kwa kufanya hivyo tumeshaelewa kwamba elimu ndiyo msingi wa maendeleo yoyote yale. Lakini vile vile na sisi tuweze kuwa katika nafasi ile ile ambayo inaendelea duniani sasa hivi katika mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikiwa ni kweli tunaona kwamba elimu itatoa mabadiliko, basi ni lazima tuzingatie elimu ya ufundi. Nasema hivi kwa sababu ya umuhimu wake. Ufundi ni jambo muhimu sana na mimi nilitazamia kwa sababu ya umuhimu huo basi lingeweza kujitokeza katika sura nzuri katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefanya vizuri sana kama hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inavyosema katika jitihada za kuwaandikisha watoto wa darasa la kwanza katika shule zetu za msingi. Lakini vile vile jitihada kubwa sana zimefanywa na Serikali na wananchi wote hapa Tanzania katika ujenzi wa shule za sekondari hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Tanzania kwa kuitika wito wa Serikali wa kuweza kujenga shule za sekondari nyingi sana hapa nchini. Sina takwimu sasa hivi kinchi, lakini najua shule nyingi sana za sekondari zimejengwa; na kwa kweli kuna mabadiliko makubwa, hilo lazima tulikubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nini hatma ya hao vijana ambao watakapomaliza elimu ya msingi au watakaomaliza elimu ya sekondari ili waweze kuwa watu wakamilifu ni lazima wawe wamepatiwa *skills* mbalimbali za kuweza kujitegemea katika maeneo yao wanapomaliza shule. Bila *skills* zozote mimi naona tunapoteza wakati. Wananchi wengi wanatazamia kwamba wanapokuwa na watoto wao shuleni wakitoka basi wawe na mchango wa aina fulani katika maeneo wanayoishi.

Huko nyuma kulikuwa na utaratibu huo ambapo mwanafunzi akitoka shule, kwa mfano katika shule zile ambazo zilianzishwa, nakumbuka waziwazi kabisa kwamba kulikuwa na elimu ya ufundi ikitolewa katika shule kama *Moshi Technical,* ikitolewa Elimu ya Ufundi katika Shule ya Sekondari Ifunda, vile vile huko Malangali nadhani hata Tanga. Utaona kwamba watoto wale waliokuwa wakitoka katika shule zile walikuwa wamejengewa misingi mizuri sana ya elimu ya ufundi. Walipokwenda katika maisha yao ya kawaida walikuwa na uwezo kabisa wa kuweza kujifanyia kazi zao za msingi. Kwa hiyo, mimi nafikiri jambo hili tumelilegeza na mimi naomba sana tulirudishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa tuna mipango na Ilani ya Uchaguzi imesema kwamba ifikapo mwaka 2010 basi kila Wilaya itakuwa na Chuo kimoja cha *VETA*. Lakini hapo mtoto ambaye angepata elimu ya ufundi akiwa shuleni ingekuwa ni bora zaidi kuliko hiyo ambayo ataipata baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shule hizi tunazojenga za sekondari tungeweza kuweka kwa makusudi mikakati ya kufundisha ufundi angalau tungeanza na shule moja katika kila Wilaya. Nazungumzia shule za sekondari siyo vyuo ambapo inaweza ikafundishwa elimu ya ufundi. Kwa hiyo, tukifanya hivyo tutakuwa tumejibu hoja nzuri sana ya elimu ya kujitegemea, tutakuwa tunajibu hoja nzuri sana ya mwanafunzi au kijana kwenda kuanza maisha ya kujitegemea katika sekta binafsi. Kwa hiyo, naomba sasa hili liweze kuzingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili la kuanzisha shule moja ya *VETA* kwa kila Wilaya. Serikali itwambie imefikia wapi, leo ni mwaka 2007, sijasikia kule Mkoani kwangu Mbeya kwamba kuna Wilaya ambayo tayari imeanza mpango wa kujenga chuo cha *VETA* kwa Wilaya. Tunayo *VETA* ya Mkoa, lakini *VETA* ya Wilaya haipo, sasa Serikali imefikia wapi, inawezakana ipo katika mipango ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya

Ufundi. Lakini naona kidogo tunakwenda taratibu na hili ni jambo la msingi sana. Lazima tujiandae vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watoto watakaomaliza sasa katika elimu ya sekondari ni wengi, kwa sababu tumejenga shule nyingi. Sasa bila *skills* hizo kwa kweli tutajikuta mahali pabaya sana. Wenzetu ambao wanajiita *Tiger Countries* kama Malaysia, China, Japan waliendelea wakafika hapo kwa sababu ya ufundi na teknolojia, ndivyo walivyosisitiza. Sasa leo Watanzania tumeanza kuzungumzia kuwa *Mini-Tiger*. Kuwa *Mini - Tiger* bila kusisitiza ufundi na teknolojia kwa kweli hatutaweza kufikia maendeleo ambayo wenzetu wamekwenda nayo. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ijaribu kuliangalia hilo vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba la pili, nizungumzie suala la uboreshaji wa Miji au Majiji hapa nchini na nijihusishe zaidi katika suala la mifumo ya kuondoa maji machafu katika Miji.

Mheshimiwa Spika, hili mimi naliona ni tatizo kubwa. Ni tatizo kubwa maji machafu yanayozunguka Miji yetu wakati wa mvua, hali hiyo inatisha na kwa kweli tusipojiandaa sasa hivi, mimi naona matatizo makubwa zaidi yatakuja kutokea. Ukichukua Jiji la Dar es Salaam peke yake nenda kwenye eneo kwa mfano la Vingunguti. Kule siku ikinyesha mvua kunafurika jamani haupitiki kabisa, kwa sababu gani, kwa sababu hakuna mifumo ya mifereji ya maji machafu. Sasa kila mtu anajenga nyumba na *septic tank* lake. Siku ambayo tutakuja kupata mafuriko makubwa tutapata shida kubwa sana, yale ma-*septic* yatakuja yafumuke, yatupe shida kabisa na tutaogelea katika maji machafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuanze sasa taratibu hizo katika Miji. Mimi nafikiri Dar es Salaam kama wanayo *sewage system* basi ni asilimia 5 tu. Lakini asilimia kubwa sana bado, ukiangalia Nigeria Mji wao ule mkubwa wa Lagos ilipaswa uhamishwe waupeleke Abuja kwa sababu ya mambo kama hayo. Sasa sisi tukichelewa basi tutapata shida kubwa sana. Miji inayojenga hivi sasa kama Dodoma, tuangalie mambo hayo ya kujengwa *Central Sewage Systems* ili maji machafu yaweze kuondolewa. Lakini Dodoma inajengwa mimi sijaona *Sewage system* zinajengwa, kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naweza kukubali kwa sababu fedha wanayopata kwa kweli ni kidogo na pengine haitoshelezi kabisa haja ya kujenga *sewage systems*. Kwa hiyo, naomba sana ili tuepukana na gonjwa hili la kipundupindu ambalo linatusumbua mara nyingi, Serikali ianze kuliangalia hilo kwa sababu bila mfumo mzuri wa maji machafu kipindukipindu kipo hapa na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, ambalo nataka kulichangia vile vile ni lile ambalo nafikiri Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa na *concern* nalo. Nalo ni posho za Madiwani. Mimi napenda kuipongeza sana Serikali hasa Waziri Mkuu nampongeza kwa kufikiria Madiwani ili na wenyewe waweza kuongezwa posho. Lakini shilingi 60,000 nikiangalia jiografia ya maeneo ambako natoka mimi uchukue wale Madiwani wanaotoka katika Wilaya ya Chunya kwa mfano, kule Lupa Tingatinga watembee mpaka Chunya

waje wapate shilingi 60,000 kwa kweli hazitoshi Mheshimiwa Waziri Mkuu, angalau tungefikiria hata kuanzia shilingi 100,000. Najua uwezo wa Halmashauri nyingi ni mdogo. Lakini sasa basi tujaribu kuliangalia kama Serikali inaweza kufidia ile *difference,* Halmashauri zilipe hiyo shilingi 60,000, lakini ile *difference* basi Serikali ingeitoa angalau wapate shilingi 100,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shilingi 60,000 hazitoshi na inapaswa sisi kama Waheshimiwa Wabunge tuwatetea kwa sababu wenzetu tunawaona jinsi wanavyofanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nzuri, nimeweza kuchangia hayo machache. Lakini ni katika kuboresha hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo kwa kweli imefafanuliwa vizuri na ni mambo ya msingi ambayo yamewekwa bayana. Tunalosubiri ni utekelezaji. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Bajeti ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Awali ya yote naomba kutoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wote na familia ya Marehemu Amina Chifupa na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, kwa jinsi ambavyo umetuwakilisha. Roho ya Marehemu ipumzike kwa amani. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kabla ya sijaendelea kuchangia niunge mkono hoja hii. Muda unakimbia naweza nikapitiwa wakati nikigongewa kengele.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishukuru Serikali kwa juhudi zake madhubuti za ujenzi wa madarasa ya shule za sekondari. Kwa kweli jambo hili limekuwa ni jambo zuri kwa sababu vijana wetu wanaomaliza darasa la saba umri wao ni mdogo na hata maumbile yao ni madogo. Siku za nyuma ilikuwa ikifika mwezi Julai, ndugu walio mbali wanaanza kuandika barua, naomba unitafutie mfanyakazi, lakini juhudi hizi za Serikali kujenga shule za sekondari zimepiga azma yao hiyo *stop;* na mimi nawatangazia kupitia Bunge hili kwamba vijana wanaomaliza darasa la saba kule Kilimanjaro hawatakwenda tena kufanya kazi kwa watu, kwa sababu walikuwa wanajituma kufanya hivyo wakiamini kuwa wakishatoa huduma hiyo huenda wakasomeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hilo na pia niwapongeze Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Makatibu Tarafa, Madiwani wetu na hao Makatibu Kata bila ya kuwasahau wananchi wenyewe na Wabunge wenzangu ambao hatukulala kwa sababu huo ulikuwa ni mchakamchaka kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo naomba sasa nijielekeze kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nikianzia ule ukurasa wa 11 mpaka wa 17, yote inazungumzia uwezeshaji katika nyanja mbalimbali. Hotuba hii ni nzuri, imeturahisishia mambo na imejibu mambo mengi ambayo labda hapa ningeuliza na sina haja ya kuuliza tena. Niseme tu kwamba kwa kweli hizi fedha za Mheshimiwa Rais shilingi bilioni 21

zinapatikana ndugu zangu, ila hazipatikani kwa kwenda kusimama tu Benki na kuzichukua. Fedha hizi zinapitia kwenye vyama, *SACCOS* au kwa wajasiriamali. Sasa basi, kuna kazi ambazo lazima zifanyike ili uweze kupata hela hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuunda vikundi hivyo, pili ni kushirikiana na Ofisi ya Ushirika, tatu ni kushirikiana na viongozi wa Wilaya na pia kuongoza vikundi hivyo vipitie kila eneo ambalo linastahili waweze kumudu au kukidhi majibu yote ambayo yanatakiwa huko Benki.

Mimi nasimama hapa nitoe ushuhuda katika Mkoa ninaotoka ambao ni Kilimanjaro hadi kufikia sasa kuna vyama vya ushirika vinne ambavyo vimeshachukua mikopo ya uhakika.

Kuna chama cha *SACCOS* cha UWAMOMASA, hiki ni chama cha pale mjini, akinamama wamejikusanya wamefungua *SACCOS* yao, lakini hawakufungua wenyewe tu wamesaidiwa na Ofisi ya Ushirika, wamesaidiwa sana na na Mkuu wetu wa Wilaya ya Moshi, Ndugu Samizi, wamesaidiwa pia na Mkuu wa Mkoa, zimezungumzwa taarifa zao kwenye taarifa za mkoa na hatimaye mimi mwenyewe nimejitahidi mpaka kumwona Waziri wetu wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mrajisi nimemwona na tukapata ukomo wa madeni. Chama hiki cha UWAMOMASA kimepata shilingi 470,000,000 sio jambo dogo kwa sababu nayo ni *SACCOS* kubwa yenye wanachama 1,200. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haikuishia hapo kuna Ndungu nasikitika leo saa hizi Mbunge wa Same amekwenda kwenye mitihani, lakini angekuweko Mama Anne Malecela nadhani angefurahi kwa sababu kile chama cha Ndungu cha *SACCOS* kimepata shilingi 600,000,000 na wao wanashughulika kilimo cha mpunga na tangawizi. Zipo pia *SACCOS* zingine ambazo zimepata fedha hizi na nyingine ziko katika *process* na wote hao katika kusaidiana na viongozi niliowataja. Mimi nimeona nitoe ushuhuda hapa ili wenzangu Wabunge niwaombe tuungane pamoja tuwaongoze hawa wananchi waweze kupata mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa kwamba fedha hizi katika awamu ya pili zitapitishwa kwenye vyombo vingine, hapa ningeomba kupata ufafanuzi kwa Waziri Mkuu. Wakati atakapokuwa anajibu hoja yake kama *SIDO* imefikiriwa kupitishiwa mikopo hii? Mimi nimeona nitamke *SIDO* kwa sababu ina uzoefu, *SIDO* ni mkongwe katika kusaidia wajasiriamali na wale ambao hawatajiunga na *SACCOS* mmoja mmoja anaweza akaenda *SIDO* akakopeshwa kiwango ambacho kinaweza kumsaidia yeye. *SIDO* ina ufuatiliaji mzuri. Kwa kweli *SIDO* inatoa elimu na hata kwenye maonyesho ya Sabasaba *SIDO* huwa ina *sponsor* watu kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba basi kama *SIDO* imefikiriwa ili niweze kuwaambia wananchi wangu huko Kilimanjaro kwamba hata *SIDO* pia ipo. Tunajua kwamba wengine wanapitia *NMB*, lakini pia kwenye Mkoa wangu kuna Benki ambazo ni za Kiwilaya. Kuna ile Benki ya Mwanga, Benki ya Uchumi, ningeomba pia Benki hizo ndogo ndogo ziweze kufikiriwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie pia suala la ajali barabarani. Hili limekuwa ni tishio. Kwa kipindi kifupi hata jana tena na leo imeandikwa ajali nyingine zimetokea. Sasa mimi najiuliza hivi hizi ajali ni kwa vile madereva hawajui udereva? Jibu ni hapana; wote wana leseni. Je, mabasi yote ni mabovu? Hapana. Je, ni usiku wanaendesha, lakini nakuta hapana, *accident* nyingi zinatokea mchana kweupe. Sasa tatizo ni nini? Nikaona labda pia madereva wetu huwa hatukagui hizo leseni mara kwa mara. Usalama wa Raia wanajitahidi na ma-*traffic* waliopo njiani wanajitahidi lakini je, akili za hawa madereva ni timamu?

Mheshimiwa Spika, wakati tukiomba leseni tunaulizwa kama macho yanaona, unakwenda na cheti cha daktari cha kuhakikisha kwamba macho yangu yapo vizuri. Lakini sijaona nikiulizwa kama akili zangu ziko sawa sawa? Sasa nilikuwa naomba labda katika kupata leseni tuangalie pia akili zao ziko sawa sawa na hapa sina maana kwamba ni wendawazimu tu, kuna watu ambao wanazubaa, hawapokei upesi katika kutaka kujihami labda *reflex action* iko *slow,* sasa watu hawa ni daktari tu ndiyo anaweza kufahamu, lakini sio *traffic* wala yeyote mwingine. Inatokea mtu anaendesha gari anakuta kitu mbele ghafla hawezi tena kufanya chochote ila ni kuliangusha gari. Nilikuwa naona kwa kweli tuwatumie madaktari wetu vizuri na wanaweza kutusaidia sana kuhusu hawa madereva wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo naona pia haya magari yanayopo mengine ni machakavu. Ukiangalia *spare parts* zinazokuja nchini nyingine ni *genuine,* nyingine sio *genuine* na zile ambazo sio *genuine* ni rahisi sana kwa hiyo, utakuta kwamba wengi wanapenda kununua *spare parts* za bei unafuu. Niombe basi hawa wenye mabasi na Serikali pia isimamie jambo hili. Mabasi yao yakishapimwa yaonekane pia kama yanastahili kutembea barabarani wakati wote au ni mabasi ambayo sasa yawekwe pembeni.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie mazingira na hapa nitaanza na Jiji letu la Dar es Salaam. Kwa kweli kwa macho Jiji ni zuri na wengi wanapenda kutembelea Dar es Salaam japo sio kuishi. Lakini usafiri wa pale Dar es Salaam unakuwa ni mgumu kutokana na hali yenyewe tu ambavyo magari hayatembei, yamejazana kwa wingi. Sasa hapa najiuliza leo Dar es Salaam imekuwa ni tishio inasaidiwa vipi? Bahati nzuri, kwenye kitabu cha Waziri Mkuu kimeeleza vizuri Dar es Salaam itasaidiwa vipi? Lakini najiuliza sasa baada ya Dar es Salaam kuna miji midogo ambayo inakuwa miji, miji mingine inakuwa miji mikubwa na miji mikubwa inakuwa Manispaa halafu Jiji. Sasa najiuliza je, kuna mipango gani ya siku za baadaye kuona kwamba hatutakuja tena kupata shida tunayoipata ya Dar es Salaam. Je, ujenzi unaoendelea sasa kwenye miji ambayo inakua nikiangalia mji kama Arusha hali kama hii inaanza kujitokeza, mji kama Moshi ni kwa vile tu watu wengi wanalala nje ya Moshi, lakini pia hali kama hiyo inajitokeza na miji mingine mikubwa. Sasa, nilikuwa naomba wakati ambapo ujenzi unaendelea tuweze kuweka tahadhari hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kilimanjaro unafahamika zaidi kwa ajili ya ule Mlima wa Kilimanjaro. Lakini nataka nifahamishwe kwamba katika huo mlima zaidi ya kusikia kwamba labda *TANAPA* wanatoa michango kwenye shule au kwenye *projects*

zinazoendelea je, kuna mpango ambao zile Halmashauri husika zinazozunguka Mlima zinapata chochote ili kuweza kusaidia basi wale wananchi wanaozunguka?

Mheshimiwa Spika, natambua kuna fungu linalotoka kwa ujirani mwema yaani wale watu wanazunguka mlima, lakini haiishi hapo hata mji wenyewe wa Moshi pia bila ya Moshi kuwa safi na mzuri hata hao watalii hawatapenda kukaa Moshi. Sasa niombe tu Serikali kueleza kama kuna mpango wowote wa kusaidia zile Halmashauri ambazo zinazungukwa na Mlima Kilimanjaro. Nimesikia wenzetu wenye machimbo wanazungumzia mrahaba, wanazungumzia kupata dola laki mbili, lakini mimi sielewi wale wa Mlima wa Kilimanjaro wanapata kitu gani! Kwa sababu naelewa pia hata wale wanaokaa karibu na Mbuga za wanyama wanapata chochote. Sasa nilikuwa naomba kujua kama wananchi wanaozunguka Mlima wa Kilimanjaro, Halmashauri zao zinapata chochote. *(Makofi)*

Natambua kwamba sasa hivi shughuli zote za Mlima zimeelekezwa zirudi *TANAPA* na wala sio Serikali Kuu iliyokuwa inasimamia misitu na wala sio katika Halmashauri. Lakini Mlima huu huwa unachomwa na wakati huo inakuwa ni patashika, wananchi na viongozi wao akianzia Mkuu wa Mkoa, Wilaya, Madiwani wanakimbizana kwenda kuzima moto katika Mlima, inakuwa ni zoezi kubwa na zoezi la dharura sana. Sasa sijui kama *TANAPA* yenyewe inatoa vitendea kazi vya kuzima moto kwa sababu vijana wetu wanavyoitwa kuzima mlima sijaona wakipatiwa chochote cha kujihami. Nilikuwa naomba jambo hili liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani kwa Benki ya *CRDB* kwa jinsi ambavyo wale *staff* wanashirikiana na akinamama katika kufanya mchakato wa kufanya miradi ambayo itakuwa ni endelevu hata baada ya kupata mikopo yao. Najua wale wanasimamia, wanakwenda kuona mradi uliopo, lakini hizi zote ni juhudi za *Microfinance* ambayo inajitegemea katika hiyo Benki ya *CRDB*.

Mheshimiwa Spika, niombe basi baada ya kusema hayo tuzidi kuomba Serikali itoe mafunzo endelevu ambayo watawapatia akinamama siku zote kwa sababu huko nyuma akinamama walikuwa wanasomeshwa kwenye Kata katika mafunzo ya maendeleo. Naomba basi mafunzo hayo ya ujasiriamali yaende mpaka kwenye Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nashukuru kwa nafasi hii na naunga hoja mkono tena. *(Makofi)*

**MHE. ALHAJ MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini kabla sijachangia naomba kwa niaba ya wananchi wapiga kura wangu wa Jimbo la Kigoma Kusini nami nitoe salamu za rambirambi kufuatia kifo cha Mbunge mwenzetu Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia na nimwombe Mwenyezi Mungu awajalie moyo wa subira wazazi, ndugu na jamaa wa familia ya Mzee Chifupa. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu za rambirambi, nianze awali ya yote kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimesoma hotuba hii kama vile nilikuwa nasomea mtihani. Kusema kweli aliyoandika Waziri Mkuu humu ndani na timu yake yamegusa Serikali yote, ndiyo maana ikawa ni Ofisi ya Waziri Mkuu maana ndiyo kiranja. Ukishasema hayo na ukasema hotuba imegusa Serikali yote unaweza ukashindwa uanzie wapi uishie wapi. Katika vitu ambavyo nimeandika nilidhani nitazungumza pointi 19 sidhani kama muda utaniruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mimi ninayetoka Magharibi mwa Tanzania ni vyema nianze kuzungumzia mawasiliano kwa maana ya barabara na reli. Hapa nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa ziara yake aliyoifanya hivi karibuni katika Mkoa wa Kigoma. Mheshimiwa Rais alipokuja Kigoma ametupa watu wa Kigoma matumaini makubwa na kwa matumaini haya si kwa watu wa Kigoma tu ni pamoja na watu wa Mkoa wa Tabora kwa sababu ndiyo tunaunganishwa na hili ninalotaka kulisema. *(Makofi)*

Katika imani ya Waislam tunaambiwa Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wale wanaosubiri. Mheshimiwa Rais alipokuwa Kigoma alinisimamisha kwenye mkutano wa hadhara nimsalime. Nilisema kauli hii ya Mwenyezi Mungu hasa hasa ilishushwa kwa ajili ya watu wa Kigoma. Kwa nini? Zimepita awamu tatu za Serikali, miundombinu ya barabara haikuguswa kabisa na moja ya awamu hizo kiongozi wa awamu siwezi kumtaja alipokuwa anaaga alikuja akatuaga Kigoma, akatueleza wananchi wa Kigoma nitaomba mniwie radhi sana Serikali iliwasahau. Ndiyo alizungumza kwenye mkutano wa hadhara wakati anaaga. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete miongoni mwake mtendaji mkuu wa Serikali hapa Bungeni Mheshimiwa Edward Lowassa wameitazama kwa jicho la huruma na wala sio jicho la husuda eneo la Magharibi mwa Tanzania tumeahidiwa kupata barabara. Barabara hii inaanzia Kigoma – Tabora – Itigi - Manyoni - Dodoma na tutaunganishwa na Dar es Salaam. Niliwahi kuzungumza hapa Bungeni mtu aliopo Dodoma akitaka kupanda treni kwenda Dar es Salaam hana hamu tu ya kupanda treni, kwa sababu ana uhakika wa kuchagua apande basi lipi kwa wakati gani, sisi hatuna uchaguzi. Tunaona Serikali sasa imekumbuka imeona hatuna uchaguzi imeamua kutuweka na sisi katika ramani halisi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunasikia fununu na Mbunge hatakiwi kufanya kazi kwa kusikia fununu lakini ukizisikia hutakiwi kuzipuuza. Barabara hii inaombewa fedha kutoka *Road Fund* lakini vile vile tunaambiwa wapo watu walishabadilisha mwelekeo wa barabara zao. Sasa ilitakiwa itoke Manyoni – Itigi – Tabora – Ipori - Mpanda badala ya Tabora - Kigoma. Tunaomba fununu hizo ziwe ni za kusikia na sio za halisi. Nia nzuri ya Serikali ambayo imeonyesha kwa Serikali kwa sisi watu wa Kigoma isije ikapotea. Kwa hiyo, tunashukuru sana Serikali kwa kutia mkazo wa ujenzi wa barabara lakini kubwa zaidi ni ile nia ambayo imeonyeshwa barabara itajengwa maana huwezi kujenga barabara bila madaraja. Serikali yetu imefanya mazungumzo na yamefikia hatua kubwa sana na Serikali ya Korea Kusini ya kujenga daraja pale Malagarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara mwaka jana pale Kigoma kwa makusudi ilionyesha kwamba na yeye anaguswa na Kigoma kuwa imebaki vile ilivyo angeweza kutoka Kigoma kurudi Dar es Salaam alisema nitakwenda kwa gari nikaone hapo mahali. Kwa kweli amekwenda pale tukakutana na viongozi wa Mkoa wa Kigoma na Tabora, Mheshimiwa Spika mwenyewe ni shahidi tumekutana pale, hii yote imetupa imani kwamba Serikali sasa inatazama kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukishatazama usafiri hasa wa barabara kwa Magharibi mwa Tanzania maana yake umefungua uchumi wa nchi. Hili niliunganishe na mipango ambayo Serikali hiyo imefanya imetuletea Mkuu wa Mkoa mchapakazi, mtu mwenye upeo mkubwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu anakumbuka maneno aliacha anatuagiza akitukabidhi rasmi sasa Mkuu wa Mkoa kwenye majumuisho wakati wa ziara yake pale Kigoma. Sasa kuna bahati mbaya sana wakati mwingine mkiletewa mtu mzuri anakaa muda mfupi anahamishwa, tunaomba, chonde chonde mtuachie huyu bado tunamhitaji. Tunajua angeweza kwenda Mkoa mwingine akafanya kazi lakini sasa ameonekana anataka kuisaidia Kigoma kwa jinsi mnavyomwelekeza. Tunaomba awepo pale na aendelee kuwepo, anataka kwa kushirikiana na huku *centre* kuifanya Kigoma iwe ni Dubai ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea la barabara, asubuhi niliuliza swali hapa Bungeni kuhusu reli. Tunaomba huduma za reli na kuiboresha, kuifanyia ukarabati na kuikodisha mipango ifanywe haraka. Tumekuwa tunasikia mwezi wa nane, tisa leo asubuhi nimeshtuka nilivyosikia mwezi wa tisa maana tarehe ya mwisho ilikuwa ni mwezi Agosti. Sasa leo nasikia tena mwezi wa tisa na ikiwezekana tena ikawa ni mwezi wa tisa wa mwaka kesho. Nashukuru Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ananihakikishia kwa kupiga kifua kwamba itakuwa ni mwezi wa tisa mwaka huu na mimi sina sababu ya kutokumwamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia masuala ya miundombinu ya barabara ya Kigoma - Tabora mpaka Dar es Salaam huku nizungumzie suala la barabara ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu atakumbuka alipokuja Kigoma, alipokuwa anasomewa taarifa nyumbani kwa Mkuu wa Mkoa pale Ikulu Ndogo nilitoa maelezo na nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu alimsimamisha Meneja wa *TANROAD* akamweleza aone ni namna gani anavyoweza kusaidia. Ni barabara inayotoka Ilagala kwenda mpaka Kalia na hatimaye hii barabara ya kuunganisha na Mkoa wa Rukwa.

Mimi nimetazama kwenye vitabu nimesikitika kuona kwamba tunatengewa shilingi 950,000,000 tu. Mheshimiwa Waziri Mkuu kama alitazama televisheni jana na leo asubuhi ameona jinsi watu wa *SUMATRA* walivyokuwa wanapambana na wasafirishaji kupitia maboti. Usafiri tunaotumia eneo lile ni maboti. Sasa kwa muda wa siku tatu mfululizo maboti yanayofanya kazi mwambao mwa Ziwa Tanganyika yamekuwa hayafanyi kazi, wananchi wamekosa huduma za usafiri kwenda na kutoka vijijini, hoja ni kwamba maboti hayana *safety gear,* yale maboya. Lakini tunaambiwa maboya hayo yanapatikana Mombasa na hata Dar es Salaam hakuna. Lakini *SUMATRA* wanataka huyu mtu apate maboya yale ambayo nchini hapa maboya hayapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tungemwomba Waziri Mkuu kwa kupitia kwako aweze kutusaidia, hatuna usafiri mwingine kwa sasa mwambao mwa Ziwa. Kwa hali hiyo, tunaomba basi wakati juhudi za makusudi zinafanywa upatikane utaratibu wa kuruhusu maboti yale yafanye kazi. Lakini barabara ya Kigoma – Simbo – Ilagala - Kalia itengewe fedha za kutosha na iharakishwe ili iondoe tatizo la usafiri mwambao mwa Ziwa Tanganyika Kusini.

Lakini pamoja na barabara hiyo lipo tatizo la kivuko pale Ilagala kwenye Mto Malagarasi. Kivuko kile nimshukuru Mheshimiwa John Magufuli alipokuwa Waziri wa Ujenzi kilihamishiwa Kigoma nafikiri kutoka Rufiji, sina uhakika lakini nadhani kutoka Rufiji. Tumeletewa kivuko kibovu kwa kweli pengine umeletwa mtumba uje uozee pale. Kinafanya kazi siku moja, mwezi mzima hakifanyi kazi. Lakini mbaya zaidi hata watumishi waliopo pale sasa wamekifanya kivuko kile ni mradi, ukitaka kuvuka unaambiwa ununue mafuta na Mbunge ili aende kijijini kwao lazima avuke bahari. Sasa Mbunge achangie mafuta na wanatazama kama Mbunge atavushwa bila ya kuchangia wanasema aah, kumbe na huu ni mradi wa Mbunge vile vile. Sasa tunaomba Serikali iangalie kivuko kile, ituletee kivuko cha uhakika sisi na watu wa Kigamboni hakuna tofauti. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, lipo suala la mawasiliano ya simu ambalo halikujibiwa nafikiri litajibiwa siku nyingine la kuhusu simu Usinge kule Urambo. Sasa sisi pale Nguruka ambayo ni jirani sana pua na mdomo na Urambo tumewekewa mitambo ya *Celtel* ina zaidi ya miezi sita sasa mitambo imekamilika lakini haifanyi kazi na watu waliopo Nguruka wakati mwingine ili wapige simu wanapanda juu ya miembe kwa kutumia mtambo ambao upo Usinge. Sasa tunaomba Wizara inayohusika isaidie kuharakisha mtambo uliopo Nguruka ufanye kazi ili wananchi wapate matunda ya mtambo ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu. Hili nitalizungumzia si kwamba wanapata au hawapati hapana, mimi ninaye kijana wangu ni mmoja katika watu wanaoomba kwenda Chuo Kikuu mwaka huu. Lakini nimeshtuka sana kuona kipengele fulani kwenye fomu za mikopo. Bahatu nzuri mimi nimeshiriki kuhesabu sensa ya kwanza mara baada ya Uhuru mwaka 1967 nikiwa Kidato cha Pili na nilikwenda kwa sababu Kasulu. Kwenye sensa ile kuna kipengele cha kutaja kabila na dini lakini sensa zilizofuata vipengele hivi vilitolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka hotuba moja ya Baba wa Taifa Marehemu Mwalimu Julius Nyerere ambayo ni nzuri tu ilieleza hakuna haja ya kutambuana kwa makabila, makabila yamebaki kwa ajili ya matambiko. Lakini kwenye fomu hizi za Elimu ya Juu kuna mahali mwanafunzi anatakiwa akasaini fomu hii kwa kiongozi wake wa dini ili iwe nini? *(Makofi)*

Mimi inanitia mashaka kuweka kipengele kile kwenye fomu hii. Vipengele vingine vilivyoko pale vya kupata uthibitisho wa mwanafunzi mimi sina matatizo navyo. Uongozi wake wa Kijiji wa Serikali alipo ilikuwa ni mwisho. Tunapotaka kumtambua

kwa dini yake tunataka kumtambua ili tumpe mkopo kwa sababu ni Mkristo au Muislam au ni vipi? Ningeomba Ofisi ya Waziri Mkuu iingilie hili, tunaweza tukaona ni jambo dogo, mwanzo wa moto ni cheche na mwanzo wa ngoma ni lele. Ningeomba sana Serikali ilizingatie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ya kwanza ya pili? Naomba Mwongozo.

**SPIKA:** Nakupa faida kwa sababu kila mtu hata meza hainisaidii, kwa hiyo, endelea.

**MHE. ALHAJ MANJU S. MSAMBYA:** Nashukuru.

**SPIKA:** Pia Mheshimiwa Manju, mambo unayoyasema yanaelekea karibu na Urambo pale kwa hiyo ….*(Kicheko)*

**MHE. ALHAJ MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la kuhamia Dodoma. Wenzetu Malawi, Pakistan na Nigeria waliamua miji yao mikuu baada ya uamuzi wetu sisi. Pakistan wamehamia Karachi kutoka Islamabad baada ya uamuzi wetu sisi. Malawi walihamia Lilongwe kutoka Blantyre, baada ya uamuzi wetu sisi, Nigeria wamehamia Abuja kutoka Lagos, baada ya uamuzi wetu sisi, lakini sisi hapa kila wakati tuko mbioni, mbio hizi zinakwisha lini? *(Makofi/Kicheko)*

Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Serikali ya Awamu ya Tatu ilikuwa na Wizara ya Ushirika na Masoko ikiwa ni Wizara inayojitegemea. Serikali ya Awamu ya Nne, Kilimo, Chakula na Ushirika ni Wizara moja. Wizara ya Ushirika kwenye Serikali ya Awamu ya Tatu ilikuwa imeletwa Dodoma. Tulipokuwa kwenye Kamati katika kudodosa masuala haya ya Bajeti tunaambiwa sasa Idara ya Ushirika inatoka Dodoma inarudi Dar es Salaam, hivi kweli tunakusudia kuhamia Dodoma? Napata wasi wasi mimi kwa sababu badala ya kusema kwamba sasa na Wizara zingine zije huku ile sehemu ya Wizara iliyokuwa Dodoma inarudi Dar es Salaam maana yake tunarudi Dar es Salaam wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine linahusu Ofisi ya Bunge, siku ile Bajeti inasomwa na hata Kikao cha Bunge kilichopita walikuja watu hapa wanazungumzia masuala ya UKIMWI, ni jambo zuri sana. Lakini nilishtuka nilipoona watu wanasema wanauza dawa za kutibu UKIMWI na watu hawa wamepata ridhaa ya Bunge kwenda kukaa pale wanauza dawa na hawasemi kwamba ni za kupunguza makali, wanasema ni dawa za kutibu UKIMWI. Wana vielelezo vya barua vya kutoka Ofisi ya Rais Jamhuri ya Kenya, Wizara ya Afya Kenya ni kwamba zile dawa ziko *confirmed* na Ofisi ya Bunge imewapa kibali cha kuja kujitangaza pale.

Mheshimiwa Spika, mimi nilitegemea Bunge lingetakiwa kujua wanachoeleza pale ni nini. Hawa watu wanatoa mawazo potofu, wanawapa imani kwamba sasa dawa ipo. Kwa sababu wamekuja na barua inayoonyesha Ofisi ya Rais wa Kenya , mimi sina hakika kama dawa inapatikana na kama imepatikana si basi umma utangaziwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumzia maslahi ya Madiwani na mimi ni vyema nikazungumzia lakini kule kwenye maslahi ya fedha. Nadhani wenzangu wamezungumzia vya kutosha pengine nitasema laki tatu inawezekana hazipo. Mimi nizungumzie Madiwani kwa maana ya usafiri. Wabunge tuko hapa, Madiwani wanachakalika kwa niaba yetu na kwa ajili yetu wote wakiwa kule, lakini maeneo wanayozungukia wengi wanakwenda kwa mguu. Nafikiri ifike wakati Serikali kama inavyowafikiria Wabunge kwa usafiri iwafikirie na Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDUL JABIR MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Aidha, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kibiti na Wilaya ya Rufiji kwa ujumla tunamtakia maisha mema Marehemu Amina Chifupa, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin*.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu kwanza niishukuru sana Ofisi yake hasa TAMISEMI kwa kutoa kero moja kubwa katika Wilaya ya Rufiji ambayo ilikuwa ni Wilaya pekee ambayo kwa muda mrefu watendaji wa vijiji walikuwa hawajapata mishahara yao. Sisi Wabunge tulikuwa tunawasiliana mara mara na Mawaziri wahusika kuweza kuona ni namna gani watumishi hawa wanaweza kupata mishahara yao. Lakini nashukuru mshahara wa mwezi huu wa sita wameupata watendaji wote 39 na kero hiyo imekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nashukuru sana Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI wakishirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kuweza walau kupeleka walimu maeneo yale ya Delta ambako kwa muda mrefu kulikuwa hakuna walimu wa kutosha lakini sasa hivi eneo lile lina walimu wa kutosha ambao kwa sasa wanafanya kazi ingawa wanafanya kazi nusu nusu kwa sababu familia zao zote hazipo kule wamekwenda wao wenyewe tu.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze kutoa matatizo machache ambayo yanaikabili Wilaya ya Rufiji hasa Jimbo la Kibiti. Katika Jimbo la Kibiti tuna maeneo mawili makubwa. Kuna eneo la Delta ambalo lina wakazi zaidi ya 40,000 na eneo ambalo ni kubwa zaidi lina wakazi wengi zaidi ya laki moja. Lakini ninazungumzia hasa maeneo ya Delta ambayo ni *under served* kwa muda mrefu sana. Eneo hili ukianzia kisiwa cha kwanza mpaka unafika kisiwa cha mwisho lina urefu wa kilomita zaidi ya 65, si eneo dogo. Ukianzia kisiwa cha kwanza mpaka cha mwisho ni zaidi ya kilomita 65 ndani yake humo kuna visiwa vidogo vidogo vingi, kuna shule za msingi 18, kuna Kata nne ambazo zote kwa ujumla wake zinakuwa na wakazi kama 40,000. Lakini kwa muda mrefu Mheshimiwa Waziri Mkuu eneo hili halina watumishi wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu, kuna upungufu wa walimu ingawa wamepelekwa wachache sasa hivi *at least* shule ina walimu watano, hakuna waganga, zahanati zipo lakini hali ya zahanati zenyewe nazo ni duni, watumishi wa aina nyingine wote kule hawaendi. Eneo hili hakuna usafiri wa kuaminika wanasafiri kwa mitumbi kwa zaidi ya saa kumi na mbili kwenda katika vijiji hivyo. Eneo hili halina umeme, halina maji safi, eneo hili hakuna mawasiliano yoyote ya simu wala mawasiliano mengine. Ni eneo ambalo kwa kiasi kikubwa limekaa kama vile halihudumiwi. Nimezungumza hapa kwa kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, nilikwenda pale mwaka jana mwezi wa nne na Mheshimiwa Naibu Waziri na nashukuru pia Mheshimiwa Mizengo Pinda ameshafika Mbwera na anakuelewa vizuri na pia Mheshimiwa John Malecela alipokuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais mwaka 1994 alikwenda Mbwela. Hawa wanaelewa vizuri mazingira ya kule. *(Makofi)*

Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu nilipokwenda na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, nilimtaka awe *advocate* wa kule kwa sababu wengi wa watumishi wa Serikali hawakuelewi, hizo kilomita 65 za urefu hawakuelewi wanaona eneo la *Delta* ni eneo dogo sana labda la kilomita moja ama mbili lakini halipo hivyo lina urefu zaidi wa kilomita 65. Sasa namshukuru sana Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, ame-*advocate* kwa muda mrefu na sasa hivi Serikali inaelewa kwamba katika eneo la *Delta* kuna watu. Namshukuru pia Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mama Ishengoma naye alikwenda kule akaona nae amekuwa *advocate* mzuri sana wa eneo lile. Sasa kuna matatizo niliyotaja ni mengi tutayatatua namna gani matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaombi kwamba ili utatue matatizo ya Delta kwanza ni lazima tupate usafiri wa kuwapeleka wananchi kwenda kule. Mpaka leo wanatumia mitumbwi ile ambayo haina injini. Watu hao 40,000 wanatembea katika maisha ya kubahatisha, wanazama sana, wanakufa wengi tu kutokana na kupinduka kutokana na mawimbi na wanyama. Sasa kwa watumishi na wananchi wa kule wanapata shida sana kuyafikia maeneo hayo. Upande wa watumishi wamepelekwa walimu, lakini walimu wote waliokwenda kule hakuna hata mwalimu mmoja ambaye amekwenda na mkewe, wanaogopa. Wameamua akinamama na watoto wanakaa huku juu, kwa sababu kule hata kama ukiumwa atampakia kweli mkewe kwenye mtumbwi ili ampeleke Hospitali ambayo iko zaidi ya kilomita 100, haiwezekani. Watumishi wameamua kukaa peke yao na sababu kubwa ni usafiri. Sasa mwaka jana niliuliza swali langu Bungeni hapa kuiomba Wizara hasa TAMISEMI kama Serikali inajenga barabara kutoka *point* moja kwenda nyingine hivi inashindwaje kutoa boti angalau tatu au nne kuwasaidia wananchi wa maeneo yale kuweza kusafiri kwa urahisi? Kwa nini tunawaweka katika mazingira magumu hawa watu wa kule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawapati elimu, hawapati matibabu mazuri, maisha yao ni duni kwa nini tunawafanyia hivyo? Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba sana tuna Kata nne na hizo Kata zote ni kubwa, tunaomba utusaidie angalau tupate boti za kuweza kuwasafirisha watumishi waende ili na wao waweze kuwahudumia wananchi wa kule. Bila ya kupata usafiri kwanza basi jitihada zote za kupeleka walimu hazina maana kwa sababu mwalimu akikaa kwa muda wa wiki mbili akimkumbuka mama watoto wake anarudi huku huku alikotoka na watumishi wengine vile vile. Tunaomba

sana Mheshimiwa Waziri Mkuu utupatie angalau boti za kuweza kuwapeleka watumishi kule pamoja na wananchi waweze kusafiri maisha ya usalama, wasisafiri maisha ambayo yamepitwa na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusu kituo cha afya Mbwela. Mara nyingi kituo cha afya kinapojengwa kinapatiwa na usafiri wake. Kwa mfano, maeneo ya huku juu wanapewa magari pale ambapo Serikali ina uwezo. Lakini kituo cha afya Mbwera ambacho ndicho pekee kilichokuwepo kule visiwani ni kimoja tu kina hudumia Kata zote. Sasa kituo kile ambacho kilizinduliwa mwaka 1994 kimefunguliwa na Mheshimiwa John Malecela aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais baada ya kufunguliwa kimeachwa solemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna hata boti ya kusafirisha wale wananchi wanaopatwa na matatizo kutokana na pengine kujifungua au magonjwa ya mlipuko yakitokea, kumtoa pale kwenye kile kituo cha afya kumpeleka kwenye Hospitali ya Wilaya hakuna boti ya namna hiyo. Hivi kweli Serikali haina uwezo wa kutoa *ambulance* kwa ajili ya kituo hiki ili iwahudumie watu wa huko *Delta?*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba sana hili nalo liangaliwe, tupewe kipaumbele kwa kupatiwa walau boti ya kusafirisha wananchi ambao kwa bahati mbaya wanapata matatizo makubwa lakini hawana uwezo wa kusafiri. Wanasafirishwa na mitumbwi na wengi wanafariki kabla ya kufika popote na wanasafiri kwa mitumbwi kwa zaidi ya saa kumi na mbili ili kuweza kufika Muhoro waingie kwenye gari ndiyo wapelekwe Utete kilomita zaidi ya sitini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala zima la walioathiriwa kwa kupitisha njia ya umeme. Tunashukuru sana Serikali kwa kuleta umeme eneo la Kibiti hasa Jimbo la Kibiti. Lakini katika eneo lile wananchi wengi wamekatiwa mazao yao ili zile nguzo za umeme ziweze kupita. Tangu mwaka jana wengine mwaka juzi, lakini jambo la kushangaza watu hawa hawajalipwa fidia zao. Hivi kweli kama haya mazao yaliyokatwa yangekuwa yamekatwa katika maeneo mengine kweli Serikali isingechukua hatua za haraka sana kuweza kukamilisha kulipa mazoa yao? Mtu umekatiwa mazao yake ambayo yanakupatia fedha kwa mwaka mzima ambao ulikuwa unategemea upate fedha sasa hivi umelikosa. Serikali bado haijatoa fedha. Naomba sana Wizara ya Nishati na Madini, tayari wameshaandaa majina, vitabu vimepelekwa kwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Wilaya wameshasaini muda mrefu tu. Vikapelekwa kwa Mkuu wa Mkoa, Mama Ishengoma ameshasaini muda mrefu lakini malipo yao mpaka leo ni utata. Nimefuatilia *Songas* wanasema kwamba wao kwa sasa hivi haina uwezo wa kulipa suala hilo bado linaendelea kujadiliwa lakini hela za kutosha hawana. Watapata lini hawa watu? Yale mazao waliyokuwa yakiwapatia fedha sasa haya kazi yoyote yameshakatwa watakula nini? Naomba sana suala hili la ulipaji wa hawa watu walioathirika na kupitiwa na nguzo za umeme liweze kufuataliwa kwa makini na waweze kupata hela zao haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

La mwisho ni kuhusu kituo cha afya Kibiti. Katika kituo hiki cha afya Kibiti, kilichojengwa tangu miaka ya 1960 na ndiyo kituo pekee kwa upande wa juu

kinachohudumia wakazi zaidi ya 120,000. Katika Jimbo la Kibiti tuna vituo viwili. Kituo kimoja kipo Mbwera na kituo cha pili ni hiki cha Kibiti. Lakini hali yake ni mbaya sana, magodoro ya wagonjwa ukiyaona yanatisha. Halmashauri ya Wilaya ilishafanya mpango wa kupeleka fedha *MSD* kwa ajili kupewa vifaa hivyo lakini miaka inapita *MSD* hawajapeleka.

Mheshimiwa Spika, ukienda pale hakuna shuka, hakuna magodoro, magodoro yote tangu miaka ya 1960 mpaka leo hakuna godoro jipya. Sasa naiomba Serikali hawa watu wa *MSD* kama wanameshindwa kufanya kazi zao warudishe hizi fedha ili tutafute vifaa mahali pengine ili watu waweze kuhudumiwa. Kuendelea kuwaendekeza hawa watu kwa kuziweka fedha huko na kazi zenyewe hazifanyiki ni kupoteza muda.

Mheshimiwa Spika, naomba sana fedha ambazo zimekwenda *MSD* za Wilaya ya Rufiji na Wilaya zingine kama *MSD* imeshindwa kufanya kazi basi fedha hizo zirudishwe Halmashauri ya Wilaya ili tutafute maeneo mengine ya kununula vifaa tunavyovikusudia.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Jimbo labda nimalizie kwa hilo, katika Jimbo langu la Kibiti ninakaa kwenye Ofisi ya Katibu Tarafa, tupo pamoja pale ndiyo tunafanya kazi kwa pamoja. Akiwa ana kazi yake yeye anafanya, nikiwa na kazi yangu mimi basi namwondoa aende akakae pembeni na mimi nifanye kazi yangu. *(Makofi/Kicheko)*

Mimi naomba kwamba yale Majimbo ambayo yako nje ya Makao Makuu ya Wilaya kwa kuwa kuna Ofisi 40 zilijengwa, kipaumbele yapewe Majimbo hayo ambayo hayana Ofisi kabisa mojawapo Jimbo la Kibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii adimu na adhimu ili na mimi nipate fursa ya kuchangia hotuba hii au hoja hii iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Kwanza sina budi na mimi nitoe salamu za rambirambi kwa niaba ya wananchi wangu na mimi mwenyewe, kwa jamaa, ndugu na marafiki kwa msiba wa mwenzetu uliyempata Mheshimiwa Amina Chifupa, Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi na awajalie subira wazee wake, ndugu na marafiki awape roho ya subira ili waweze kusahau.

Mheshimiwa Spika, la pili ningeomba nichangie kidogo kuhusu hali ya kiuchumi na fedha na nitangulize kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishani na Madini kwa leo kufika hapa na kutupatia tamko la Serikali yumkini limetusaidia sana na wakati mwingine limezidisha hoja nyingine nzito. Lakini amefanya hivyo kwa sababu katumia kifungu chake cha sheria au kwa mujibu wa sheria na sisi Waheshimiwa Wabunge tusingezua hoja zile pasingekuwa na tamko la Waziri wa Nishati na Madini wala la Waziri wa Fedha kuhusu masuala yale na yamekuja kwa sababu tumehoji mambo na tumehoji kwa sababu tumetumia wajibu wetu wa Kikatiba. Kifungu cha 63(2) na (3),

kinachotutaka sisi Wabunge wajibu wetu ni kuihoji Serikali na kuielekeza Serikali na kuishauri Serikali. Wajibu huo pia tumepewa zaidi upo katika Kifungu cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 100(1) ambacho kinatupa fursa wa majadiliano na mahojiano katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda niseme *Auditor General* ana haki ya kisheria ya kuchunguza hesaabu ya taasisi yoyote ya Serikali aidha, yeye mwenyewe au kwa kutumia wakala wake. Hicho ni kifungu chake cha kisheria, anaruhusiwa kisheria na sisi Wabunge tunayo haki hiyo kwa Ibara hizo nilizozitaja. Kwa hiyo, tunapofanya hivyo wale wenzetu ambao hawajaelewa bado hii *seperation of powers,* wasilaumu ni haki yetu ya Kikatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimempongeza Mheshimiwa Waziri kwamba lile tamko la Serikali inawezekana na kwa upande mmoja lime-*create* hoja nyingine nzito zaidi ambayo bado Kambi ya Upinzani inasema ile haja ya kuwa na *select committee* aidha, Kamati zinazohusika za Bunge au *select committee,* tunakuomba ufanye hivyo, uteue ili kujisafisha na kuwasafisha wananchi. Sisi tunaweza tukatumia *data* za Serikali lakini Bunge halilazimishwi, linaweza kutumia *data* au uchunguzi wa Serikali lakini Bunge pia lina wajibu kwa upande wake kujiridhisha. Kwa hiyo, bado tunaomba ile hoja au maombi ya kuundwa *select committee* tunaomba iwepo pale pale. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nataka nizungumzie suala la uchafuzi wa mazingira na hili kidogo ni suala linalotisha, liko hasa katika Kijiji cha Nakabale, Wilayani Geita. Mwaka 2000 na 2001 kulitokea matatizo katika kijiji hiki yalitokana na uchafuzi wa mazingira. Mto uliopo pale wa Mtakuja maji yake yakaharibiwa kwa kuingia sumu inayotokana na madini. Matokeo yake, Mwenyekiti wa Kijiji cha Nakabale, Ndugu Stafano Mzimanunu Lifungulo, tena Mwenyekiti wa CCM, ng'ombe wake 16 na kondoo wawili wakafa na isitoshe kuna ndugu yetu mmoja Bwana Kanana Benedicto alipotelewa na mama yake, ndugu yake, mtoto wake na shemeji yake yaani watu wanne katika familia ya nyumba moja kwa kula sungura waliomwokota pembezoni mwa ule mto.

Mheshimiwa Spika, baada ya muda yupo mwingine Ndugu Tano Mwita, mke wake akaenda kuoga pale akavimba, akaumuka mwili kama andazi na mwisho wake akafariki mwaka 2001 mwezi Januari. Sasa basi Ofisi ya Waziri Mkuu walikwenda wakashuhudia matatizo hayo kwa kushirikiana na *DC* wakati ule Marehemu Ernest Nyanda na Afisa Usalama, Bwana Masale na tunategemea hayo masuala yamekwisha.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa yako, juzi tarehe 26 Juni, 2007, siku ya Jumanne ng'ombe 28 wamekufa kwa kunywa maji yenye sumu kwenye hilo bwawa na mara hii ni kwenye ile sehemu ambayo maji yote machafu yanahifadhiwa. Hawa wawekezaji hawajajenga uzio wa namna yoyote, matokeo yake ng'ombe wamekwenda juzi wamekufa pale pale. Hiki kijiji cha Nyakabale, kimepimwa, kimesajiliwa na kina hati lakini kina athirika au wananchi wa pale wanaathirika sana. Nyumba zinapasuka mpaka akinamama mimba zinatoka pale. *(Makofi)*

Mimi naishauri Serikali ichukue hatua mara moja kwa sababu uzito ni nini hapa? Na Mwalimu wangu hapa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, ananisikia na anahusika vizuri, Serikali ichukue hatua aidha, kijiji kile kihamishwe pale watafutiwe eneo lingine au litafutiwe ufumbuzi mwingine. Kwa sababu lipi bora, uchumi wa hao wawekezaji au uhai wa maisha yetu? Hali ilivyo Nyakabale ni mbaya sana. Hilo suala langu la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala langu la tatu, bado nipo Geita. Kuna kijiji cha Kasota, mimi nasema kuna ndugu yetu mmoja John Jeremia, alikuwa katika nyumba ya mdogo wake akavamiwa na majambazi, akapigwa mapanga, akanyang'anywa saa, viatu, *t-shirt* na fedha taslimu shilingi 27,000. Wale watu wakaonekana wakakamatwa na walipokamatwa wakawekwa ndani. Baada ya siku tatu, nne wamekwenda kuchukuliwa dhamana. Kuanzia tarehe hiyo hakuna chochote kingine kilichoendelea, wale watu wameachiwa, yeye ameshaumizwa na anamajeraha na makovu tele, mali yake imepotea; sasa kusema kweli nasikitika hii ndiyo kitu tunaita *double standard* kwa sababu kwa nini na kwa sababu gani hatua hazijachukuliwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu huyu Mwenyekiti wa Kasota alikuwa CCM na baadae akaenguka akaingia *CUF* na akashinda uchaguzi. Kwa hiyo, ni Mwenyekiti wa kijiji cha Kasota kwa tiketi ya *CUF.* Sasa kwa vile yeye kafanya hivyo hakuna hatua zozote zilizochukuliwa na si yeye tu kuna mifano mingi na hili nilimwandikia Waziri wa Katiba na Sheria na Waziri wa Usalama wa Raia kuhusu kesi za kubambikizwa jinsi zilivyokithiri lakini mpaka leo sijapata majibu yoyote. Ningeomba hali kama hii, hawa wote ni raia wa Tanzania, raia wetu awe CCM, awe *CUF* pasiwe na *double standard*. Wengine wachukuliwe hatua, wengine wasichukuliwe. Hili lipo Geita katika kijiji cha Kasota. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la nne labda kidogo nizungumzie hili suala la Benki Kuu lakini kwa upande mwingine. Hii asilimia ya Zanzibar ya 4.5 kwenye hotuba hii ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 10 na 11. Mimi nashindwa kufahamu hii asilimia 4.5 ya misaada ya nje ya Bajeti nini kinakusudiwa hapa? Nafikiri wakati ukifika Mheshimiwa Waziri Mkuu atatufafanulia. Sasa kwa nini iwe nje ya Bajeti? Suala hili lingefaa lifafanuliwe. Kama ni kero za Muungano zipo muda mrefu na haya mazungumzo anayofanya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi tayari yameshachukua muda mrefu. Kidonda chochote ukikiachilia bila ya dawa kitazidi kuumuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri muda umeshakuwa mrefu na mambo yapo mengi ni vyema sasa hivi *at least* tuambiwe hizo kero za Muungano ni ngapi zote na zipi zilizopatiwa ufumbuzi mpaka leo na isitoshe tunafahamu hizi kero zinawagusa Watanzania wote. Wanaozungumza ni watu wa upande wa chama kimoja na wengine wanao haki ya kuzijua na kushiriki kusaidia kutatua matatizo. Haiwezekani siku zote Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi halafu hatupati majibu. Tunataka Mheshimiwa Waziri Mkuu angalau utufafanulie ni yapi na umefikia wapi na sisi tujiridhishe. Matatizo mengi wakati unapita, kuna masuala ya mafuta na gesi, yote hayo yanahitaji ufumbuzi. Gesi imeshaanza kuchimbwa muda mrefu sasa hivi lakini ushiriki wa Zanzabar hatuujui.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nadhani hayo uje utufafanulie na sisi kidogo tujiridhishe angalau watu wapate kujua nini kinaendelea na nini cha kufanya baadae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache nafikiri inatosha ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, ahsante sana, nimekusikia unazungumzia sana Geita lakini hujatuambia isije ukawa umepata mchumba Geita wewe. *(Kicheko)*

Namwita Mheshimiwa John Magale Shibuda, atafuatiwa na Mheshimiwa Thomas Mwang'onda na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu ajiandae.

**MHE. JOHN M. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote natoa shukrani za dhati kwa kunipatia fursa hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa Ofisi yake pamoja na Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijachangia, naomba kwanza nitangulize pole zangu kwa msiba uliotufika sote sisi Wabunge na hususan familia ya hayati Amina Chifupa. Mola amlaze mahali pema peponi na awajalie wanafamilia moyo wa subira katika majaribu mbalimbali. Kwani alitakalo mola ndiyo linalomfika binadamu.

Mheshimiwa Spika, wahenga husema usione cha elea, kimeundwa na kina wenyewe. Tanzania itajengwa na Watanzania wenyewe. Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alituasa kwamba chama legelege kitazaa viongozi legelege. Nashukuru sana wosia huo Watanzania wamekuwa wakiuzingatia na ndiyo maana Chama cha Mapinduzi kimekuwa kikipata ule ushindi wa kishindo. Nimesema hivyo kwa sababu chama legelege huzaa viongozi legelege, chama legelege huzaa hoja legelege, chama legelege huzaa husda na vijicho vilivyofichika katika tuhuma na mambo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza wananchi wa Maswa wote husasan wana-CCM kuanzia ngazi ya Mashina, Matawi na Kata, watendaji wa Vijiji, Kata, Halmashauri na Serikali Kuu ya Wilaya ya Maswa kwa ushirikiano mbalimbali ambao wananipatia mimi ili niweze kufaulisha usimamizi wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga katika changamoto mbalimbali akishirikiana na watendaji wa Mkoa na taasisi mbalimbali katika Mkoa wetu katika kuwezesha kuhamasisha mchakato tukafanikisha kuibua amko jipya la elimu katika Mkoa wetu na katika Wilaya ya Maswa. Hongera sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na wenzako wote! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge hili, napenda kusema ya kwamba Tanzania hii iko mikononi kwa wale wote wenye upendo na mshikamano wa nia njema kwa maslahi

ya umma. Wahenga husema; “hakuna masika yasiyokuwa na mbu.” Kwa hiyo, napenda kusema ya kwamba katika mchakato wa kuhamasisha, tuibue elimu na tujenge madarasa, wapo waliong’atwa na mbu, kwa hiyo, naomba wastahimili kwa sababu kila jambo lina sadaka yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme machache na kupongeza juhudi za Serikali ya Muungano na Serikali ya Baraza la Mapinduzi Zanzibar iliyozaliwa na Mapinduzi matukufu yakazaa haki Zanzibar, napongeza mashirikiano mbalimbali wanayokaa na kujadiliana kiuungwana ili watatue mapungufu yanaojitokeza katika safari ya ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, naomba tu kuhamasisha ya kwamba Serikali ya Muungano kwa vile tuna rasilimali nyingi kama madini, maliasili, mazao ya kilimo, basi tuchangie kwa juhudi na kwa kuthubutu kwa *SACCOS* mbalimbali za Zanzibar ili waweze kufaidika na matunda ya umoja ni nguvu.

Mheshimiwa Spika, *SACCOS* za Zanzibar hivi sasa ziko katika mtiririko wa upatu. Sasa wakati umefika Serikali ya Muungano tuwawezeshe wenzetu hususan katika maeneo yanayokaliwa na Vyama vya Upinzani, kwa sababu wanahitaji *drip* maalumu za kuinua ustawi na maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana hapa palizuka neno ya kwamba wajasiriamali Maswa hawakupata pesa. Napenda kuthibitisha ya kwamba Maswa, Benki ya *NMB* na ninaipongeza sana, ilitoa jumla ya shilingi milioni 34.9 kwa wajasiriamali 25 na bado tunaendelea jinsi gani Serikali itaboresha na kufanikisha utoaji wa misaada. Napenda kutahadharisha kwa ndugu wa Maswa kwamba tunapozungumzia mjasiriamali, siyo mtu anayetaka shilingi milioni 20 na huyo huyo akaamua kwenda kuungana na watu kuja kuleta nongwa Bungeni, hapana! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchumi wa Maswa, naomba Serikali ijenge utaratibu maalumu wa kuboresha zao la Pamba na vile vile kutoa huduma mahsusi kwa wafugaji. Nasema hayo kwa sababu zao la Pamba ndio uti wa mgongo kwa wananchi wa Maswa. Naomba vile vile tufungue milango ya kuhamasisha hususan kujenga barabara kati ya Dar es Salaam kupitia Dodoma – Tabora – Shinyanga – Mwanza ili barabara iweze kuwa ni kichocheo murua kwa ustawi na maendeleo kwa wananchi wa Mikoa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maswa tupo tayari kutumia mila na desturi zetu ili tukopesheke. Mwaka jana tulitembelewa na Afisa Mfuko wa Pembejeo wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Wakati sasa umefika, naiomba Serikali itoe tamko itatusaidia vipi kufanikisha wananchi wa Maswa kukopeshwa, kwa sababu sisi tuna nyumba za matembe, hatuna hatimiliki na MKURABITA hivi sasa unasua sua. Kwa hiyo, naomba kwamba MKURABITA huu hivi sasa kwa sababu hauwezi kufikia maeneo yote kwa pamoja na kwa haraka, basi pawepo na mipango mikakati ya muda mfupi ili tuweze kuinua na kupiga vita umaskini katika vijiji vyetu hususan Maswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma ya maji, naomba nimpongeze Mheshimiwa Dr. Dr. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Maji kwani alifika mara moja baada ya

kupasuka Bwawa la Zanzui na amenitaarifu kwamba amepeleka hoja hiyo ya dharura Ofisi ya Waziri Mkuu. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atutolee tamko la Serikali jinsi gani Bwawa la Zanzui litapata hatma ya kuweza kurejeshwa ili wananchi wa Maswa pamoja na mifugo yetu tuweze kupata maji. Naomba sana msaada huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maswa ina kilomita za mraba 3400 za Wilaya. Sasa Wilaya hii ambayo ina kilomita za mraba 3400, ina *ambulance* moja. Itahudumia vipi wananchi na hapo hapo tunasemwa ya kwamba tuna imani za kichawi na waganga wanapotosha! Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie kutatua tatizo hilo, naomba nimuonyeshe ukweli wa tatizo hilo kwamba tarehe 12 Januari, mtoto Jeremia alizaliwa mbugani kwa sababu ilibidi mama yake apelekwe na mkokoteni unaovutwa na ng'ombe kwenda hospitali hii ni kwa sababu ya uchakavu wa barabara. Naiomba Serikali itutazame kwa moyo wa huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme machache kuhusu shukrani kwa Bajaeti ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wasukuma tuna tatizo moja, hatuna kona kona tunapozungumza kwa sababu hatuna asili ya kula ubwawa wa mafuta ya nazi. Wahenga husema: "Nyani haoni kundule na pole kwa mjane, haimuondolei majonzi ya upweke wa kifo cha mmewe." Hapa Bungeni kumetokea jambo moja ambalo linasikitisha sana! Sisi Wabunge ni wawakilishi wa raia wote na sisi Wabunge ndio tunaosimamia Katiba ya nchi na kuhakikisha kwamba raia wote wanapata haki za nchi. Sasa inapoibuka hoja ya kutuhumu na kusuta mtu ambaye hayupo katika Bunge hili, kwa kweli tunakuwa hatutendi haki na Bunge hili tutaonekana tunaumiza watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania hivi karibuni tunaingia katika Shirikisho la Afrika Mashariki, je, tumejiandaa vipi wakati Kenya wazalendo wameshika hatamu za uchumi? Sisi hapa hatujashika hatamu za uchumi? Leo akija Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya na wazo zuri, nongwa! Je, tutaibua wazalendo wangapi na lini kwa hisia za nongwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri uendelee kuwa na semina za kutukumbusha wajibu wetu. Nashauri vile vile ya kwamba Serikali iendelee kuthubutu kuwezesha wazalendo kushika hatamu. Naipongeza sera ya CCM pamoja na Serikali yake. Kila vumbi halikosi kikohozi na Watanzania ndio watakuwa majaribio ya kushika hatamu za uchumi. Je, kama tutaanza kuwakatisha kwa tuhuma na lugha za kejeli, tutafika wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wingi wa majonzi, naomba kusema ya kwamba haki za raia wa Tanzania zitalindwa ndani ya Bunge hili na haki ya kusikilizwa mtu apewe kabla ya kumtuhumu na kumsuta na ndio maana Bunge lina Kamati zake na watoa habari huwa wana kinga hata kama ni *PCB*. Kauli mbiu ya Usalama wa Raia ni kwamba wananchi tushirikiane katika kutatua au kupiga vita ujambazi. Je, iwapo watu humu ndani wana taarifa, kwa nini hawajazipeleka kwenye Kamati zetu, wakaitwa wahusika wakahojiwa, badala yake watu wanakuja kusuta hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majadiliano Bungeni yanapaswa kuwa ndio urithi mzuri kwa hao watakaokuja kuwa Wabunge wa kesho. Napongeza Wabunge wa CCM kwa moyo wa subira na busara na hekima ya kutosuta watu hadharani, bali huwa wana majadiliano ya hekima. Nimeshauri haya kwa sababu walalamikaji waliosuta wenzao wangeweza kutumia Kamati za Bunge na ninaona bado tunaendelea kurutubisha hayo mapungufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wale binadamu waliojeruhika ukweli ni binadamu walio na nyongo na hao wamejeruhika kupitia Bunge hili. Kwa hiyo, naomba ikiwa Kamati ya Uongozi ya Bunge inaweza ikakaa na kutafakari vyema, wanastahili barua za kupewa pole na kuombwa msamaha kwamba wametuhumiwa na kusutwa katika Bunge hili na wale waliowasuta na kuwatuhumu, Kamati ya Uongozi wa Bunge iwajadili na kuona itafanya nini! Hakuna uhuru usio kuwa na unyago wa miiko. Kwa hiyo, naomba sana tujitambue kwamba na sisi Wabunge ni binadamu, tunastahili kutendewa haki na haki tunayoidai, tuwatendee wengine.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja! *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shibuda, ahsante! Nina hakika mjadala huo utaendelea tu, kwa hiyo sina la kusema kwa sasa ila namwita Mheshimiwa Thomas Mwang'onda. Wakati huo huo Mheshimiwa Zaynab Vullu amepatwa na msiba, kwa hiyo Mheshimiwa Mama Florence Kyendesya achukue nafasi yake na baada ya hapo atafuata Mheshimiwa Lazaro Nyalandu. Mheshimiwa Mwang'onda hayupo naye! Kwa hiyo, Mheshimiwa Florence Kyendesya kwa mara ya kwanza tangu kuapishwa humu Bungeni! *(Makofi)*

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mara yangu ya kwanza kuingia humu Bungeni ili nami niweze kutoa machache au nichangie machache kuhusu hotuba ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu na kwa unyenyekevu mkubwa kabisa, namshukuru kwa kukiwezesha Chama changu cha CCM kuniteua kuwa Mbunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, japokuwa nimeingia kwa kuchelewa, lakini namshukuru sana Mwenyezi Mungu. Aidha, nawashukuru wananchi wa Mkoa wa Mbeya hususan wanawake walionichagua kwa kura nyingi sana ambazo zilitosha kabisa kwa mara ya kwanza kuingia humu Bungeni. Lakini, yote ilikuwa ni mipango ya Mwenyezi Mungu, sikuweza kuingia pamoja na Wabunge wenzangu. Lakini, kwa vile sauti ya Mungu ni sauti ya wengi na Mungu ni mwema, leo niko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole nyingi sana kwa wazazi wa Marehemu Amina Chifupa, kijana mdogo, msichana mdogo kabisa ambaye ametangulia mbele ya haki. Mungu ailaze mahali pema, roho yake peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze kwa dhati kabisa Serikali ya Awamu ya Nne inayoongozwa na Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Waziri Mkuu pamoja na Baraza lote la Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya ili kuyaleta maendeleo ya wananchi wa Tanzania ingawa wapo ambao wanasema hakuna kinachofanyika, lakini hilo mimi sielewi kwa sababu wao wenyewe wamepata matunda wanayaona, wamekula matunda, Watanzania kutokana na maendeleo yanayoletwa na Serikali na wapo hapa. Mimi hilo la kusema hakuna kilichofanyika, naona tungekuwa tunaangalia pande zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sikuelewa jana kuna Mbunge mmoja wa upande mwingine, tena namshukuru sana alisema na umri wake hajafikia miaka 30. Akasema nchi hii imepata Uhuru miaka 45 iliyopita, lakini hakuna kilichofanyika! Sikuelewa kwa sababu hata nusu ya umri wangu hajafikia! Lakini mimi matunda ya Serikali nimeyaona na yeye mwenyewe anayaona. Kwa kweli mengine tuwe tunapima tunapoongelea kuilaumu Serikali, kwani wananchi wanatusikiliza na wanatuona, watatuelewaje! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabla ya kuchangia, nimshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu kwa kasi yake kuhusu maendeleo ya elimu, ujenzi wa shule za sekondari. Nitakuwa sijamtendea haki Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, bila kumpongeza kwa kusimamia vizuri shule za sekondari. Namshukuru sana na nampongeza sana. Wakati wa kuchangia, kuna Mbunge mwenzangu mmoja ama Wabunge wenzangu fulani, wameomba Serikali iboreshe maslahi ya walimu na mimi nakubali na naungana nao kabisa kuboresha maslahi ya walimu. Lakini sikuelewa kidogo pale aliposema Serikali iwajengee walimu nyumba kwa sababu wanapostaafu wanakuwa na hali mbaya. Hivi kweli Serikali inaweza ikamjengea mwalimu mmoja mmoja nyumba! Sisi kule Mkoani Mbeya tuna Chama cha Kuweka na Kukopa ni *SACCOS,* kinatoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu, wanajijengea nyumba na wao wanashukuru sana katika hilo. Lakini tunaomba Serikali iongeze kuboresha! Lakini kwa kweli kumjengea mwalimu mmoja mmoja, sijui kama Serikali inaweza ikawa na uwezo huo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo kuhusu mafungu ya fedha yanayotolewa na Serikali kwa Halmashauri za Wilaya. Mafungu hayo ambayo kila Halmashauri inapewa shilingi milioni moja kwa ajili ya mikopo ya wanawake na vijana, fedha hizo kwa kweli hazitoshelezi. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anielewe vizuri, fedha hizo ni nzuri sana, zinawasaidia sana wanawake na vijana, lakini ni kidogo sana, zinaleta lawama kwa Serikali kwa wale ambao hawapati. Sasa, Halmashauri ipate shilingi milioni moja, itampa nani, atakosa nani? Naomba fungu hilo liongezwe ili angalau zisaidiane zikiongezwa hizo pesa zitawasaidia wanawake na vijana, halafu zitapunguza kidogo malalamiko, zitasaidiana na zile za mfuko wa JK. Zile pesa za JK ambazo zinatolewa kupitia Benki, upatikanaji wake ni mgumu sana mpaka sasa bado haujakaa sawa. Kukiwa na mfuko ule wa JK utakapoanza kufanya kazi yake vizuri, halafu ukichukua na za Halamashauri, mimi naona zinaweza zikasaidia sana kuboresha hali za wanawake na vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye suala la pensheni ya watumishi wa Serikali. Suala hili limeongelewa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi. Mheshimiwa

Waziri Mkuu ajue kwamba hili suala linaongelewa sana, basi lina uzito wa pekee. Naipongeza sana Serikali kwa jinsi ambavyo imekuwa ikiboresha pensheni ya watumishi wa Serikali waliostaafu. Hawa wastaafu huko nyuma, mimi nazungumzia kuhusu kima cha chini hasa waliostaafu kabla ya mwaka 1996. Kima cha chini kwa mara ya mwisho huko nyuma ilikuwa ni shilingi 2000/= kwa maana kwamba miezi sita anapata 12,000/=. Serikali ikaboresha, ikafika 10,000/= kwa mwezi. Kwa maana hiyo, kwa miezi sita ndiyo shilingi 60,000/=. Ikaendelea mpaka hivi sasa ni shilingi 20,000/= kwa mwezi ambayo kwa miezi sita ni shilingi 120,000. Tunaishukuru sana Serikali kwa maana imekuwa ikijali, inaona hili jambo, inajali na tunaomba iendelee kujali. Lakini hizo shilingi 20,000/= kwa mwezi, kweli kulingana na hali halisi ya sasa na kupanda gharama ya maisha, kwa kweli ni ngumu sana na mimi niko huko, ila kwa sababu Mungu amenileta hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasoma hotuba ya Waziri wa Fedha ukurasa wa 45, kifungu kidogo cha (i) kwamba kuna makubaliano ambayo yamefikiwa, naomba nisome kodogo: “Utafiti uliofanywa na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Mfuko wa Pensheni, umebaini kwamba malalamiko ya wastaafu yametokana na sababu nyingi, baadhi zikiwa ndani ya uwezo wa Wizara na nyingine zikiwa nje ya uwezo wa Wizara ya Fedha. Kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa kati ya Serikali na Mifuko ya Pensheni ya Hifadhi ya Jamii, wastaafu wote ambao wanalipwa malipo ya uzeeni na Wizara ya Fedha, wanahamishiwa kwenye Mfuko wa *NSSF* na mingineyo.”

Mheshimiwa Spika, sasa hapa ndiyo nimekuwa sielewi, kwa sababu sijui katika Mikoa mingine, katika Mkoa wa Mbeya hakuna kero kuhusu upatikanaji wa malipo. Malipo, hakuna kero, Wizara ya Fedha imefanya utaratibu mzuri sana, mtu akiwa na barua na kitambulisho, anakwenda Benki, anachukua pesa yake, anajiondokea.

Tatizo kinachogomba hapa ni malipo madogo, hela ndogo, hii 20,000/= haitoshi. Kama kuhamisha, sielewi kule mtakakohamishia, sijui kutakuwa na manufaa yapi, hapo ndio sielewi, labda tutafafanuliwa wakati Waziri mhusika wa Utumishi atakapotoa ufafanuzi. Kero hakuna, ila ni pesa kidogo, shilingi 20,000/= haitoshi. Wazee wetu kweli wengine wamechoka, wamekuwa mababu, siyo babu kama Mzee Ngombale, Mzee Ngombale ana nguvu, wapo ambao wamechoka kweli. Halafu wakae na hiyo shilingi 120,000/= kwa miezi sita, inakuwa ngumu sana. Labda Serikali ingeliangalia upya badala ya miezi sita ingefanya miezi mitatu ama kila mwezi mtu ajipatie maana yake ndiyo amefika wakati wa saa 12.00 jioni, atangoja saa ngapi miezi sita? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kuwasahau watumishi waliokuwa wa mashirika ya umma nao wana matatizo. Hawa wengi wao walipata hela kwa mkupuo.Wakapata kwa mkupuo ndio basi kwa heri, nao wengine wamechoka. Pengine, Serikali sijui inawafikiriaje ama ina mikakati gani ili nao waweze kupata ile ya kila mwezi kama ilivyo ya watumishi wa Serikali. Hilo ndilo tunaiachia Serikali iangalie uwezekano huo.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze kidogo kama walivyozungumza Wabunge wengine wanaokaa Mikoa yenye Maziwa hasa wa Kanda ya Ziwa

wamezungumzia sana hilo na watu wa Mafia nimewasikia wamezungumzia kuhusu kuwa na *Patrol Boat* kwenye Maziwa.

Mheshimiwa Spika, na sisi huko Mbeya tunalo Ziwa huko Kyela, Ziwa Nyasa. Huko kuna wavuvi wanatumia mitumbwi na humo wamo wanaopotea. Huko Kyela, basi tujue kwamba kuna *Matema Beach*. Huko Matema *Beach* Watalii wanakwenda huko wanatalii, wanafunzi wanakwenda Matema *Beach* na wengine wamewahi kupotea humo Ziwani. Tusikumbushane vidonda; kuna Mpwa, mtoto wa dada yake na Waziri fulani humu ndani, alipotea, alikuwa anasoma sekondari. Lakini, hakuna *Patrol Boat.* Wakati Serikali inafikiria kupeleka *Patrol Boat* kwenye Mikoa yenye Maziwa, basi mtukumbuke na Kyela, Mkoa wa Mbeya ambako pia kuna wavuvi ambao wanavua samaki aina ya Mbasa ambao ni watamu kuliko samaki wengine hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niupongeze Mkoa wa Mbeya kwa usimamizi madhubuti walioufanya kuhusiana na zoezi la Ihefu. Wale ambao hawajafika Ihefu wanasikia tu, wanaweza pengine wasielewe kulikuwaje. Kule kulikuwa na mgogoro mkubwa sana kati ya wafugaji na wakulima. Mauaji ya kila mara yalikuwa yanatokea, wakulima walikuwa wanauwawa kila wakati. Wafugaji wanapeleka mifugo yao kwenye mashamba, wakulima hawataki, basi ugomvi kama mnavyojua wafugaji na wakulima. Kwa kweli nawapongeza kwa kazi nzuri waliyoifanya. Halafu kulikuwa na uharibifu mkubwa sana wa mazingira, maana yake pale ni chanzo cha mto Ruaha. Tunakumbuka kwamba mwaka jana kulikuwa na ukame mkubwa sana hadi tukakosa umeme kutokana na Bwawa la Mtera kukosa maji. Leo ukifika Ihefu kuna boti, unakwenda, tunachacharika tu kwenye boti na hali imekuwa nzuri na tunaamini kabisa kwamba pengine ukame usitokee tena kutokana na huko Ihefu. Lakini, ambao hawakufika Ihefu hawakuona, inakuwa kama vile ni hadithi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nina haki zote za kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na kuipongeza Serikali kwa uamuzi huo na uongozi wa Mkoa kwa usimamizi mzuri. Nisije nikagongewa kengele, mimi sina zaidi ya hayo, maana mimi nilikuwa wa mwisho mwisho, Waheshimwa Wabunge wameongea mengi. Naunga mkono hoja asilimia mia moja! *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana! Ni mwanzo mzuri! Namwita sasa Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, atafuatiwa na Mheshimiwa Abbas Mtemvu, wakati huo na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, ajiandae!

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, na mimi naomba niungane na wenzangu, na kwa niaba ya wananchi wa Singida Kaskazini, nitoe salaam za rambirambi kwa baba yake mzazi Amina Chifupa na familia yake kwa msiba mkubwa sana uliowapata.

Mheshimiwa Spika, Amina Chifupa, alikuwa nyota ya asubuhi na sisi sote tutamkumbuka sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu kwa asilimia zote. Nachukua nafasi hii kipekee kumpongeza sana Waziri Mkuu kwa juhudi ambazo amezifanya za dhati. Ni rahisi mara nyingi tunapoamua kusimama, kupongeza, watu wakaanza kuhoji, hawa Wabunge wa CCM mbona wanapongeza tu! Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja katika kijiji cha Kijota, Singida, akaja katika kijiji cha Ilongelo na kwa ujumla usimamizi wa ujenzi wa shule za sekondari na yale ambayo Serikali imeyafanya, tutakuwa wakosefu sana kutowapongeza. Naomba nirudie tena, kwa niaba ya wananchi wangu wa Singida Kaskazini kuipongeza Serikali kwa hilo lililofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi ya maji Singida Kaskazini imeendelea vizuri sana. Kufikia mwaka huu, Singida Kaskazini peke yake tumefanikisha miradi ya zaidi ya shilingi bilioni moja na huu ni usambazaji wa maji ya mabomba, visima virefu na *distribution systems* zilizojengwa vijijini. Hakuna, hata miaka ya nyuma wananchi wa kawaida walioweza kwenda kwenye bomba na wakachota maji na kinatokea sasa hivi, *I'm very grateful* na tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwa jitihada zile za Awamu ya Tatu, niliambiwa katika Manispaa ya Kigoma, Wenyeviti wa Mitaa 70 wa Vyama vya Upinzani, walirudi CCM. Niliambiwa vile vile katika Halmashauri ya Kigoma peke yake, Diwani na Wenyeviti wake 18, wamerudi katika Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba mimi ningesikia kule Singida Kaskazini kwamba Diwani mmoja tu wa kwanza amehamia Chama cha Upinzani nafikiri ningekimbia sana nikaanza kusemezana nao. Hayo yote ni matunda ya kazi nzuri. Naomba nimpongeze kipekee na nasema kipekee kwa sababu kazi ya mtu akiifanya anastahili heshima na sisi tumeambiwa wazee watawalao vema wanastahili heshima maradufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Parseko Kone amekuja Singida kama Mkuu wa Mkoa muda siyo mrefu. Alipoingia tu amepambana na majanga ya ajabu, majanga ya *unmet* lakini amekuwa shupavu na Wabunge wa Singida kwa pamoja tumekubaliana kulisema hili mbele ya nchi. Yeye pamoja na wakuu wengine wa Mikoa wanaofanyakazi nzuri wanastahili kuungwa mkono na wanastahili kupongezwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba hilo nili-*register* kwako ifikie Serikali na wananchi wote ambao wananisikia ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nielekee kule Singida. Habari zinasemwa hapa Tanzania kwamba Singida ni Mkoa maskini. Miaka ya nyuma nchi zilizokuwa zinaitwa maskini zilikataa zikasema sisi sasa tutaitwa nchi zinazoendelea. Kwa hiyo, naomba kuanzia sasa hivi Singida ujulikane kama Mkoa unaoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *centre* ya Tanzania iko katika Wilaya ya Manyoni. Iko *system* ya Tanzania inaanzia pale Manyoni na siyo Dodoma kama watu wengi wanavyofikiria. Mwaka 1995 *GDP* ya Mkoa wa Singida ilikuwa shilingi milioni 84, hadi kufikia mwaka

2003 na kuendelea *GDP* ya Mkoa wa Singida ilifikia shilingi milioni 283,241 hilo lilikuwa ni ongezeko la asilimia 236. Ukuaji wa uchumi wa Mkoa wa Singida katika miaka hiyo niliyoitaja ilikuwa ni asilimia 236 ukuaji huu hauko sehemu yoyote duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pato la wastani la mwananchi wa Mkoa wa Singida takwimu zile zile za Serikali za mwaka 1995 mwananchi wa kawaida wa Singida alikuwa anapata shilingi 90, 896 kwa mwaka. Miaka mitatu 2003/2004 na kuendelea mwananchi wa Singida ameanza kupata kipato cha shilingi 256,948 ongezeko hili ni la asilimia 183 la ukuaji wa pato la mwananchi wa Singida, haijawahi kutokea hata Wachina ambao *the growth rate of Chinese domestic product* haijafikia ukuaji wa wananchi wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa bado barabara ya lami haijafika iunganishe Singida na inajengwa. Barabara ya lami kutoka Singida kwenda Qateshi – Babati - Arusha ndiyo inaanza kujengwa, wananchi wa Singida wameweza kupata *growth rate* ambayo ni *sustained* zaidi ya kiwango chochote katika sehemu yoyote hapa duniani. Mimi ningeomba hiki kitambuliwe. Watu wengi wanadhani Singida ni Mkoa wa mwisho hapa Tanzania labda niwakumbushie uchangiaji wa uchumi, uchangiaji wa kitu kinachoitwa Pato la Taifa unaotokana na Mkoa wa Singida sasa hivi umezidi asilimia 2.89 Mkoa wa Singida unachangia katika pato la taifa na hapa bado hauna uwanja wa ndege. *(Makofi)*

Naiomba Serikali tafadhali tujengewe uwanja wa ndege kama wenzetu wengine. Labda niseme tu Dar es Salaam kama Jiji letu ni asilimia 14.85 Mkoa wa Mwanza ni wa pili asilimia 8.34. Mkoa wa Shinyanga katika hesabu nilizonazo ni wa tatu asilimia 6.6 unafuatwa na Mkoa wa Arusha asilimia 6.1, Mkoa wa Mbeya asilimia 5.8 na kuendelea na kuendelea. Mkoa wa Singida umekuwa wa 18, ukuaji wa uchumi wa Mkoa wa Singida unatia fora na wananchi hawa wa Singida, watoto wadogo wa Singida waliozaliwa jana na waliozaliwa mwaka jana wakue wakijua Mkoa wa Singida ni Mkoa wa matumaini. Mkoa wa Singida ni Mkoa wa watu wanaopenda kazi na ningeomba hilo Serikali iweze kulikiri isikie kwamba tunakoelekea ni kuzuri kuliko tulikotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asilimia 90 ya uchumi wa Singida ni kilimo. Lakini kilimo kinachangia asilimia 60 ya *Growth Domestic Product (GDP)* ya Mkoa wa Singida. Ardhi inayofaa kwa kilimo Mkoa wa Singida ni zaidi ya hekta 1,134,400 mpaka sasa hivi kiwango ambacho kinalimwa ni hekta 281,000 na matumizi haya ni asilimia 25 tu ya ardhi tuliyonayo. Tumeomba ardhi ya Singida ipimwe. Ardhi ikishapimwa ina thamani. Hekta zaidi ya milioni moja haiwezekana ukawaambia hawa watu ni maskini. Hawa watu wana ardhi ya ajabu. Zaidi ya asilimia 75 ya ardhi inayofaa kwa kilimo Singida bado haijaweza kulimwa. Hapa tumeomba Serikali irekebishe ukopaji wa pembejeo za kilimo. Suala zima la ruzuku ya mbolea walisemea watu wengine sitalirudia lirahisishwe zaidi kwa wakulima kuweza ku-*access* mbolea. Suala zima la masoko lirekebishwe wale wanaofuga nyuki, asali waweze kupata stahili yao.

Mheshimiwa Spika, suala zima la miundombinu na hapa naomba niipongeza sana Serikali kwa sababu kwa mara ya kwanza Singida inazungumzia kuunganishwa na

Dodoma, inazungumzia kuunganishwa na Arusha na Mwanza na Tanzania itastaajabu *ability* ya Singida kufanya maajabu. Tangu mwaka 2005 wananchi wa Singida, Wilaya zote za Singida tumefanikiwa kwa kiasi kizuri sana kuweka miundombinu ya maji. Naipongeza Serikali kwa kushirikiana na benki ya dunia kwa kuweza kufanya kila waliloweza. Miradi hiyo sasa inaiunganisha Singida kwa mtandao mzuri ambao utafanya afya za wananchi ziongezeke. Tunawashukuru tena kwa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niseme baada ya barabara kuanza kujengwa ajali Singida zimeongezeka, sina hakika ni asilimia ngapi labda Mkuu wa Mkoa angenisaidia. Lakini magari yanayopita Singida hadi sasa hivi kutoka Arusha kwenda Mwanza *trucks* zaidi ya 900 kutoka Singida kwenda Arusha zaidi ya 470 kwa siku, kutoka Dar es Salaam - Singida zaidi ya *trucks* 500. Haya yote yanafikia Singida, Singida hasa hospitali ya Mkoa wa Singida iliyojengwa miaka ya 1950 wakati ilikuwa ikitibu wagonjwa 250,000 imeelemewa kupita kiasi na mambo yanayotokea mazuri. Kwa sasa hivi wananchi wa Singida ni zaidi ya milioni 1.1 ni zaidi ya wananchi wote walioko Zanzibar. Lakini Hospitali ya Mkoa wa Singida sasa inahitaji ifanyiwe ukarabati wa hali ya juu. *(Makofi)*

Katika kikao chetu cha *RCC* tumekubaliana kwamba tutatenga eneo maalumu kwa ajili ya ujenzi wa hospitali na wametenga hekta 40 zaidi ya ekari 80. Nimeambiwa katika Bajeti hii tumeomba zaidi ya milioni 600 tunaomba tupate bilioni moja ya kuanzia kujenga hospitali ya Mkoa. Hospitali hii itaokoa maisha, mnakumbuka ajali ya Mheshimiwa Stephen Kazi na wenzake ilipotokea ilibidi waite ndege kuwabeba majeruhi. Lakini Hospitali ya Singida itagusa maisha ya watu wa Mwanza, Mbeya, Dar es Salaam wanaopita hapa kwenye *central corridor.*

Hii hospitali ni lazima ijengwe mpya isiyo tu shindani lakini itakayokuwa na ubora wa kisasa itakayoweza kutimiza haya mambo ambayo tumeyasema. Nimeambiwa jitihada za Mkoa tayari ramani zimeshachorwa, Mkoa unashirikiana na madaktari wa *global out* kutoka Oministota na wengine wa Stem ninaomba sana Serikali itusaidie kwa jambo hili. Wilaya ya Singida ina Singida Kaskazini na Mjini, Singida kuna hospitali kadhaa, kuna Hospitali ya Makyungu iliyopo Singida Kusini kwa kaka yangu Mheshimiwa Mohamed Missanga na Hospitali ya Singida Kaskazini inaitwa Mtinko. Tumeomba Hospitali mojawapo kati hizi iwe ni hospitali teuli ya Wilaya kuokoa maisha ya wananchi. Singida Kaskazini wako wananchi laki tatu, Singida Kusini wako laki mbili.

Mheshimiwa Spika, nafikiri ukipiga hesabu unajua tu wapi wapewe hiyo hospitali ambayo itakuwa na heshima ya kuwa *district designated hospital* ambayo itakuwa ni hospitali ya Mtinko kwa ajili ya kuona maisha ya watu wengi sana ambao wanaitegemea. Kanisa ya Kilutheri sasa linajenga Chuo Kikuu Singida na Hospitali ya Iyambi, itakuwa ni hospitali ya kufindishia na tunawashukuru sana kwa lile ambalo wanalifanya.

Tunaomba Serikali i-*declare* kwamba misitu minene ya Singida, ambayo ina hekta zaida ya 17,750 kuwa ni hifadhi ya namna moja ya Taifa, ili kulinda mazingira na kuli-*store equal system* ya mvua ambayo tunaitegemea sana kwa kilimo na maendeleo ya

Singida. *Pressure* ya kukata magogo na kuyapeleka China, ninaomba iweze kufutwa kwa azimio la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho barabara zimejengwa lakini Watanzania wanalala saa kumi na mbili, saa kumi na mbili wanaamka, ikiwepo mabasi na magari ya mizigo yanasimama hayatembei kwa saa kumi na mbili ikishafika tu saa kumi na moja dereva analala, tunaingia ubia na Wakenya na Waganda na watu wa Burundi, hawa jamaa pamoja na kwamba wamekuwa kwenye vita wanafanya kazi saa 24, dereva huyu anasimamisha gari mwingine anachukua kwa sababu *function* ya uchumi *productive hours* ambazo nchi imeziweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali iangalie uwezekano wa kuzifanya barabara zetu zote za nchi hii zipitike saa yoyote zipitike mchana kiusalama, zipitike na usiku ikiwezekana tutumie *over walking force* kuzilinda barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja  na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, kwa mchango mzuri umetuelimisha sana kuhusu mkoa wa Singida basi muandae andae viwanja huko tunaweza kuchangamkia. *(Makofi)*

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini nikupongeze kwa kutusimamia vyema. Niwashukuru sana wananchi wa Temeke ambao waliniwezesha kunipa kura nyingi sana karibu 100,005 kuweza kuwa Mbunge wao na kufanya Temeke sasa hatuna upinzani, upinzani uliokuwa unatupa shida pale nyote mashahidi wote karibu sasa wako CCM, pale ni wimbo mmoja tu ni CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nitoe pole za dhati kwa wananchi 52 waliofariki kwenye ajali za Singida na Arusha na maeneo mbalimbali, lakini nitoe salamu za pole za pekee kabisa kwa baba wa Amina Chifupa wa Mpakanjia, na kwa mwenyewe Mohamed Mpakanjia kwa msiba mkubwa sana na kwako wewe Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge wote, Mwenyezi Mungu ailaze pema roho ya Amina Chifupa Mpakanjia peponi. *Amin.* Sisi Wabunge wa Dar es Salaam, tunakusudia baada ya kikao cha Bunge tutafanya kisomo maalumu pale Dar es Salaam kwa ajili ya Mheshimiwa Amina Chifupa, Waheshimiwa Wabunge, tunawakaribisheni wote, Zungu ndio mratibu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa dhati kabisa kumshukuru Waziri Mkuu kwa bidii zake za dhati, sisi tuliokuwa Dar es Salaam kwa kweli tunanufaika sana na bidii zake, Dar es Salaam tulikuwa na msongamano mkubwa sana wa magari, Mheshimiwa Waziri Mkuu kausimamia kwa bidii kabisa, akiongozwa na majemedari wake baada ya kushusha amri chini, majemedari wanaomsaidia Mheshimiwa Abbas Hussein Kandoro na ma-*DC* watatu wa Dar es Salaam, wakapokea kwa kweli utekelezaji ni mzuri na tunaendelea vizuri.

Taa za barabarani juzi nilisikia mtu anazungumzia taa za Dar es Salaam, sasa sikujua katika yale majimbo saba anatoka jimbo gani? Maana yake kwa bidii ya Waziri Mkuu taa za barabarani za Dar es Salaam, zinatengenezwa na Halmashauri ya Jiji ya Dar es Salaam imenunua gari mpya kabisa kwa ajili ya kushughulikia taa hizo. Mkuu wa mkoa yuko pale juu wanasimamia kwa nguvu zote akishirikiana na Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Mstahiki Adam Kimbisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli Dar es Salaam na hasa Wilaya ya Temeke tunaishukuru Serikali nyote ni mashahidi, Dar es Salaam ni mji ambao watu wanachangisha lakini Dar es Salaam kwenyewe kulikuwa hakuna shule. Lakini katika *operation* hii ya shule za sekondari Temeke tulikuwa na shule 45, sasa tuna shule 100. Pia niishukuru Serikali na kuipongeza Serikali kwa ule mradi wa mabasi yaendayo kwa kasi. Serikali imeweza kutoa shilingi bilioni 10 kwa Dar es Salaam kulipa fidia na mambo mengine tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu nina ombi moja wakati tukisubiri mradi ule uanze kwa mwaka 2008/2009 tunacho chombo cha nchi nzima *SUMATRA,* lakini Dar es Salaam ndio nafikiri kinasimama daladala, sijui mikoa yote kama nako inasimamia daladala. Kasi yake kwa Dar es Salaam, ni ndogo na kama unavyojua Jiji la Dar es Salaam sensa ya mwaka 2002 tulikuwa tupo karibu milioni 2.9 kwenye milioni tatu hivi ukitizama sasa hivi tuko karibu milioni tano.

Sasa ombi langu daladala bado tatizo la msongamano na kuvunja sheria na bado tutakwenda nao mpaka mwaka 2008/2009 ni kero kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu, kule nyuma kulikuwa na mtu anaitwa David Mwaibula, sijui yako hai au amekufa, kwa kweli daladala alisaidia kusimamia huu mpango wa daladala. David Mwaibula na watu wake alikuwa anakwenda mwenyewe barabarani na daladala walikuwa wakimuona Mwaibula, hata *traffic* walikuwa hawaogopi kama walivyokuwa wanamuogopa Mwaibula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikuombe, nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu kama kuna uwezekano basi kama yuko hai atafutwe atusaidie kwa kipindi hiki kupambana na hii hali mpaka tutakapofika kwenye ule mpango wa mabasi yaendayo kwa kasi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi nimefurahi sana kikao cha Bunge hili tofauti na kile cha kwanza, kila aliyesimama amesimama ameonyesha kilio chake zaidi ya Dar es Salaam, matatizo ya barabara Dar es Salaam, matatizo ya njia za kupitishia maji machafu na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nikuombe na nimuombe Waziri Mkuu na niwaombe Wabunge wote kuwa sungura ni mdogo, tunatakiwa tugawane wote basi tukubaliane kichwa tu tuwaachie Dar es Salaam, kile kichwa cha sungura tukubaliane tuwaachie Dar es Salaam na Mheshimiwa Waziri Mkuu hili halina kificho Wabunge wengi pamoja wanakaa kwenye majimbo yao lakini ni wakazi wa Dar es Salaam, Wabunge mbona hampigi makofi nasema kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri dalili ni nzuri, Wabunge wengi wameonyesha kulikubali hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nataka kuongelea ajira binafsi kwa mitizamo miwili, kusaidia wafanyakazi kwenye ajira binafsi vikiwemo vyombo vya habari vinavyomilikiwa na watu binafsi yakiwemo mahoteli, mashirika ya ulinzi, baa, wauza maduka, wafanyakazi kwenye hospitali binafsi, wafanyakazi kwenye makampuni binafsi, wafanyakazi kwenye baa na wafanyakazi majumbani kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mshahara wao ni mdogo sana na Serikali katika hili hatusemi lolote hawa ni Watanzania, nitoe mfano tu kampuni ya ulinzi inakulinda unailipa laki moja au laki moja na nusu, lakini yule askari anayekuja kwako kukulinda anapewa shilingi 30,000 au shilingi 40,000, unatarajia kutakuwa na usalama? Lakini kuna jambo moja tunalalamika mapato, hivyo hii sekta ya ajira binafsi hawa wafanyakazi wake, wanachangia mapato katika Pato la Taifa?

Mheshimiwa Spika, sasa mimi niombee Serikali kupitia kwa Waziri Mkuu tunatoa vitambulisho vya Taifa, tuhakikishe wafanyakazi wote ya sekta ya ajira ya binafsi kila anayepata kitambulisho basi tujue anafanya kazi wapi na njia rahisi ya kutusaidia kupata mapato mishahara yao yote hawa kupokelea benki kwa *cheque*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niishukuru tena Serikali mimi nina kero kubwa pale Yombo Vituka, Yombo Makangarawe wale wananchi walihamishwa kutoka Kurasini na walivyohamishiwa waliahidiwa barabara, Wabunge wote waliotangulia wamepita, ilikuwa pale sharti lake ukifika ni barabara na mimi nilikwenda kifua mbele nilivyoambiwa unataka kura, nataka kura, hapa barabara nikasema barabara Serikali italeta barabara. Nishukuru katika hotuba ya Waziri Mkuu barabara ya *Jet Club* kupitia Yombo, kupitia *Devis Corner* mpaka Mtongani imetamkwa, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niombe Temeke tunao utaratibu, Temeke sasa tumeondoka kwenye changarawe na barabara za vumbi kwa sababu tunayo greda, tukiweka mafuta tunapitisha. Temeke hata tukipata kidogo tu tunajenga barabara ya lami, kwa hiyo, mtakachotuletea tutaanza barabara ya lami tukisubiri hizo nyingine tuendelee nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko tatizo la msingi Kurasini, wananchi wa Kurasini alikwenda *DC* pale akafanya mkutano, alikwenda Mkuu wa Mkoa tulikwenda na sisi ule mji sasa unatakiwa uwe *Industry area,* wananchi wakaridhia kwa roho nyeupe. Novemba mwaka jana wakaenda watathmini pale wakafanya tathmini, makubaliano mwezi wa pili watalipwa fedha zao. Lakini hadi leo hawajalipwa, sasa pale kuna maneno, naomba Mheshimiwa Waziri atakaposema aseme neno kuhusu wananchi wa Kurasini, ni lini watapata fedha zao ili waweze kuondoka na wanunuzi wa Kurasini wako tayari, Serikali mkisema hata kesho naweza kuwaletea wakanunua kama tatizo ni pesa, tutapata pesa tukalipa tukaendelea na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko tatizo la kivuko, juzi tulipokuwa tunawachangia *Taifa Stars* wananchi pale Kigamboni kesho yake kwa saa sita, tukasemwa sana Wabunge kule Serikali inachangia kule *Taifa Stars* lakini sisi inatusahau. Sasa Serikali itoe tamko la Kivuko na itoe tamko la daraja na mimi nasema kama *NSSF* hawawezi au hatumtaki wako Wachina, Waziri Mkuu wako Wachina na *write up* yao iko ofisi ya Miundombinu, kama wamepoteza ninayo kopi mimi nitawakabidhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mkopo wa JK, tunashukuru sana lakini shilingi bilioni moja kwa Dar es Salaam, mkoa mkubwa jamani watu wengi lakini hata hivyo utaratibu wake uboreshwe zaidi ili wananchi wengi waweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la Madiwani, mimi nasema kama linawezekana tuna mapato mengine mazuri sana, tuna mapato ya majengo, kodi za majengo hatukusanyi ipasavyo na mimi nashauri kama inawezekana *TRA* ikusanye tutapata pesa nyingi tutakuwa na uwezo wa kulipa Madiwani hata shilingi laki tatu na pikipiki za kuwakopesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Temeke ni Wilaya mojawapo yenye viwanda vingi sana tena vikubwa lakini wale wenye viwanda wamenituma zile barabara zao nyingi ni mbovu na wao wanachangia sana Pato la taifa. Kwa hiyo, naomba pia hilo tulitizame, lakini naomba hii *Mbozi Road* sasa ni barabara ya Taifa, kuna *Kawawa Road,* kuna *Nyerere Road* hii *Mbozi Road* ndiyo inakwenda uwanja wa Taifa wa kisasa na tuna Chuo Kikuu cha Elimu lakini barabara ni mbovu, tuna *VETA* pale makao makuu barabara ni mbovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. MUSA AZZAN ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwakilisha wananchi si wa jimbo la Ilala tu bali wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam na wananchi wa Tanzania nzima. Nichukue nafasi hii na mimi kwanza nitoe pole zangu za dhati kabisa kwa familia mzee Hamis Gabriel Chifupa, yeye ndugu zake na sisi Wabunge wote kwa msiba mkubwa ambao tumeupata hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasahau kwa raha na starehe naanza kuunga hoja hii mkono kwa asilimia mia moja na yoyote atakayeona Bajeti hii kwake haifai basi ashindwe na alegee. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru na nimpongeze sana Waziri Mkuu kwa namna alivyochangamkia masuala ya shule katika mkoa wetu wa Dar es Salaam. Waziri Mkuu alitupongeza Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kutushukuru kumstua na kumweleza hali halisi ya elimu ya mkoa wa Dar es Salaam. Lakini siri ya mafanikio haya yote yalitokana na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza, ndiye hasa aliyetuambia na sisi tukamwambia Waziri Mkuu, naipongeza sana Naibu Waziri Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, kwa namna alivyotusaidia.

Nampongeza Mkuu wa Mkoa Ndugu Abbas Kandoro, kwa namna alivyohangaikia mkoa wetu na kwa namna alivyounyoosha na kuuweka katika mazingira

mazuri. Nampongeza Meya wa Jiji Mstahiki Adam Kimbisa, nawapongeza pia Mameya wote watatu, Abu Juma, Salum Londa na Bwana Husi kwa namna walivyoshirikiana na Serikali katika kujenga shule hizi mpya na haya ndiyo matunda ya Uhuru, kuna watu wanasema matunda ya Uhuru hawajayajua lakini tutawaelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza *club* ya *Manyema Football Club* ya Jimbo la Ilala kuweza kupanda na kuingia katika *premiere legue* na kuzifanya timu kutokana na jimbo la Ilala kuwepo katika *premiere legue* ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza *club* ya *Young Africans* kwa kufanya uchaguzi wao kwa amani na usalama na kuonesha kuwa sasa wanataka kuhangaikia mpira sio tena masuala mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kupongeza majeshi yetu….

**SPIKA:** Mbona hukutaja *Simba Sports Club,* kuna nini? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE MUSA AZZAN ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, Simba walishafanya uchaguzi, na wanangoja ubingwa tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza majeshi yetu, napongeza majeshi ya ulinzi na majeshi ya usalama, nchi yetu inaheshimika kutokana na uimara wa majeshi haya na uwezo wa majeshi ya ulinzi ambao wanao, majirani zetu wanatuheshimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye masuala ya barabara, ni jimbo la Ilala peke yake katika nchi hii ambayo barabara zake hazihudumiwi na Serikali, hatuna hata barabara moja iliyopo chini ya *TANROADS*. Kwa hiyo, barabara zinazojengwa unazosikia leo zilizotajwa ni vyanzo vya Halmashauri yenyewe na ni nguvu za wananchi wa Wilaya ya Ilala.

Mheshimiwa Spika, tunaomba barabara hii ya Uhuru ambayo ina *sentimental value* kwa Taifa letu, tumeshamwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumeshamwambia Mheshimiwa Waziri na ndiyo barabara ambayo inabeba wageni wa Kitaifa na wageni wa nje, barabara hii sasa ichukuliwe na *TANROAD* ili iweze kutengenezwa na iwe sura safi ya Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo unaochangia, nilizungumzia asubuhi ndiyo unachangia pato kubwa sana la kodi ya mafuta. Tunaomba licha ya kwamba mikakati ya kutengeneza *wing roads* na barabara za pembeni basi barabara za kati, barabara ya Kawe, Kinondoni, Chang'ombe, Mtoni, Kigamboni, Shingo Feni - Ilala, Gerezani, Ilala, Kariakoo, Upanga na Jangwani nazo zifikiriwe ili ziweze kupitika na wananchi hawa waanze kuona namna wanavyochangia mapato yao na namna wanavyorudishiwa ili barabara hizi ziweze kupitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mtindo sasa hivi wa baadhi ya watendaji wa Serikali inapokuja mipango mizuri kama daraja la Kigamboni, kulifanya lisijengwe kwa sababu

hakuna uchumi Kigamboni. Uchumi Kigamboni utapatikana baada ya daraja kujengwa, watu watawekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunavyozidi kuchelewa kujenga daraja hili, gharama zinazidi kukua. Watendaji wetu wengi wao wanakuwa *part of problems* siyo *part of the solution,* Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuomba sasa hivi mwaka 1970 sisi tulikwenda Zanzibar kwenye michezo ya majeshi, tukakutana na Hayati Mzee Karume, akatuambia kwamba wanangu mimi sijengi kwenda juu kama New York, najenga kwenda hivi, ndiyo zile nyumba za Michenzani na yote sababu aliweka *decision,* ali-*decide* tujenge. Sasa tuwe na maamuzi ya kusema tujenge, tutapungoza kwamba sijui kuna upembuzi yakinifu. Haya mambo hayataenda na sisi muda wetu wa kukaa katika uongozi una kipimo. Kwa hiyo, mimi naomba sasa kuwe na wakati wa kuweka maamuzi ya kuweza kukamilisha na kujenga hivi vitu.

Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Temeke kazungumzia masuala ya mishahara na mimi naunga mkono kabisa. Inasikitisha kabisa kuona wawekezaji wa viwanda, mahoteli mpaka leo wanalipa mishahara kiwango cha chini sana. Ukienda kwenye hoteli zetu mshahara wa juu kabisa wa mfanyakazi ni kati ya shilingi 60,000 mpaka shilingi 80,000/=.

Mheshimiwa Spika, hizi hazitoshi. Hawa wawekezaji wengi wao wanapata misamaha ya kodi na ukiona katika viwanda vya nguo namna ya uwekezaji wao ni wa mashaka vile vile. Mitambo yao mingi si mizuri, hali ya halisi ya sakafu ndani ya viwanda vyao vile vile haviboreshwi zaidi ya kujali tu *revenue* ambayo wao wanazozikusanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Nyumba, ifike wakati sasa Shirika la Nyumba Serikali liachane nalo. Nchi zote za nje unapokwenda nyumba hizi zinamilikiwa na *Council,* Halmashauri ndiyo zinamiliki nyumba hizi na hazipandishwi kodi kufuatana na soko la mjini, zinakuwa na kodi yake ya chini ili kuwasaidia wananchi wa kawaida na wao waishi katika mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *mandate* ya *National Housing* si kukodisha nyumba, ni kujenga na kuuza. Ni bora nyumba hizi sasa Serikali ikafika wakati sasa kuziacha wazipe Halmashauri zetu.

Kuna kijidudu nacho kinapitapita, maana kila wakati Halmashauri hazina uwezo, Halmashauri haziwezi, haya ni maneno ambayo yanapandikiziwa kuharibu majina mazuri ya Halmashauri ambazo zina nafasi kubwa sana ya kumiliki nyumba hizi na kuzikodisha kwa wananchi na kupata mapato ya kuwarudishia tena wenyewe wananchi.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa benki ya nje. Nchi nyingi za jirani wananchi wa kawaida katika Taifa lao wanaruhusiwa kumiliki benki haya ya nje, kwa maana faida inayopatikana inabaki nchini, yote haindi nje. Leo ni Tanzania tu pekee ambayo hatuwezi kumiliki au kuweza kununua *share* mabenki ya nje, na hii haitusaidii katika kuendeleza wananchi kimapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala imejenga *OPD* mpya kwa vyanzo vyake yenyewe, haya ndiyo matunda ya Uhuru. Halmashauri hii vile vile sasa inamaliza kujenga wodi za wazazi. Haya ni matunda ya Uhuru.

Wanawake wazazi hawazalii tena chini, Wanawake wajawazito au wazazi sasa wanazalia kwenye vitanda na wanahudumiwa kwa utaalamu na kwa ufanisi mkubwa. Tatizo tunalolipata ni moja, Serikali inaweka mpango wa kutoa dawa kwenye Hospitali, lakini kuna uzembe kwenye *MSD,* hizi dawa hazifiki kwa muda unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Halmashauri yetu kugharamia wodi ya wazazi kwa mwezi ni shilingi milioni 15. Kama hizi dawa haziji kwa muda unaotakiwa, inabidi tufanye utaratibu mwingine kuwasaidia wazazi hawa.

Kwa hiyo, tunaomba yule anayehusika kama ananisikia sasa hivi kama hataweza tena kuleta pesa ambazo Serikali inampa, ashindwe na alegee. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Ilala tumejenga shule 27 chini ya usimamizi wa Waziri Mkuu. Haya ni matunda ya Uhuru. Kiwango cha watoto waliofaulu na kuweza kuingia kidato cha kwanza, tuliingiza watoto asilimia 18 tu katika watoto 9,300.

Ni watoto 1,800 tu waliopata nafasi ya kuingia. Matunda ya Uhuru tumejenga mashule 27 sasa tuna kiwango 76. Haya ndiyo matunda ya Uhuru tunayoyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali kwa kutuletea mradi wa *TASAF.* Maji ukienda sasa hivi Ilala mengi tunategemea ya visima, lakini *TASAF* imetusaidia. Tuna maji sasa tunaweza tukauzia Jimbo la Ukonga kutoka Bungoni, kutokana na msaada wa *TASAF.*

Lakini bado tuna shida ya maji ya bomba kwenye maeneo mengine katika Jimbo la Ilala. Tunamwomba Waziri mhusika, Ilala ni mjini, tungependa na sisi kufungua maji katika nyumba zetu. Kwa hiyo, tunamwomba atuletee suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa nyumba Mchikichini. Tuna mwekezaji ambaye yuko tayari ku-*invest* dola milioni 300. Mradi huu toka tuanze kuuzungumzia sasa ni mwaka mmoja, hauendi, haushuki unazungukazunguka tu. Tunataka wananchi wa Ilala wakae kwenye makazi mazuri. Tunataka *first lift* mpya katika jimbo letu la Ilala ili na watu wakija waone mfano na hao wako tayari ku-*invest* kwenye majeshi na polisi na nyumba zingine za Serikali ili waweze kujenga. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali wauchukulie mradi huu kwa makini ili uweze kuanza.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii vile vile kupongeza Serikali kwenye michezo. Naipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu kwa kujenga uwanja. Naipongeza

Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuvalia njuga michezo na matokeo yake tumeyaona. Sasa hivi kila mchezaji mpira anataka kujiunga na Timu ya Taifa ile ari imerudi.

Lakini nichukue nafasi vile vile kupongeza Kampuni ya *Coca cola* kwa kuanzisha kikombe cha kuanza kupata vipaji vya watoto chini ya miaka 17. Watoto hawa ndiyo itakayokuwa sura ya timu ya Taifa huko tunakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesoma kwenye gazeti la Nipashe, napongeza sana gazeti hili kwa namna linavyowakumbusha *TFF* kuweka kumbukumbu za mchezo wa mpira katika nchi yetu. Wachezaji wa *Taifa Stars* wa sasa hivi ukimwuliza mara ngapi amechezea timu ya Taifa hajui na kwa vile siku hizi hatufungi magoli atakumbuka goli alilofunga kwa sababu ndiyo goli lililofungwa miaka minne iliyopita.

Lakini ukimwuliza kaka yangu Kitwana Manara sasa hivi kachezea *Taifa Stars* hajui, kafunga magoli mangapi hajui. Kwa hiyo, kuna umuhimu sana wa *TFF* sasa hivi kuweka kumbukumbu za michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuvitaarifu vyombo vya nje vizungumzie vizuri Afrika na Tanzania. Afrika na Tanzania *can deliver* wakipewa nafasi. Kuna magazeti wanaandika Afrika wanasema *is a passive recepient of aids and not an agent of its own development* haya ni matusi kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nampongeza Rais na naviomba vyombo vya habari vya nchi za nje sasa watuzungumzie, mambo mazuri ambayo nchi yetu yanafanya. La mwisho, Serikali hivi karibuni imechagua Wilaya. Tunaomba na sisi Mkoa wa Dar es Salaam uwe na Mikoa mitatu. Vyombo vya usalama vinafanya kazi kwa mikoa mitatu. Vyombo vya ulinzi vinafanya kazi kwa mikoa mitatu. Tunaomba sasa Dar es Salaam ipangiwe ni mikoa mitatu yaani Kinondoni, Ilala na Temeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatupati uwakilishi sahihi katika Bunge hili, tupo watu siyo chini ya milioni tano lakini Wabunge ni saba, siyo sahihi. Tunastahili na sisi sasa kuwa na Wabunge zaidi ya 12 ndani ya Bunge hili kutoka Mkoa wa Dar es Salaam ili tuweze kuwawakilisha wananchi wetu kwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo machache nimpongeze tena Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna alivyoiandaa Bajeti yake. Niipongeze Serikali, sikupata nafasi ya kuchangia kwenye Bajeti lakini kwa kweli Bajeti nayo ilikwenda vizuri na ninashukuru sana namwombea kheri Bajeti hii na Watanzania tuko tayari kushirikiana na Serikali, Wabunge tuko tayari kushirikiana na Serikali na kusaidia Serikali yetu na siyo kila saa tunainyooshea kidole, tuishauri na tuisaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuje na *solution,* tusije na malalamiko tu peke yake, baada ya hayo maneno machache najua kengele inakuja na saa mbili kasoro robo hii kila mtu akapumzike na leo nasikia kuna Miss Kanda ya Kati Dodoma, kwa hiyo, naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:**Ahsante sana Mheshimiwa Zungu, ila hao unaowataka walegee na washindwe sidhani kama watalegea wala kushindwa kwa sababu hukusema ni kwa nguvu zipi? *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hautuwezeshi kuendelea tena na mjadala sasa ndiyo umefungwa. Siku ya Jumatatu tarehe 2 Julai, 2007 utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:-

Baada tu ya kipindi cha Maswali na Majibu, Waheshimiwa Naibu Mawaziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa robo saa kwa kila mmoja watachangia kuanzia saa nne na nusu hivi nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Masuala ya Bunge kwa dakika 30.

Saa 5.00 asubuhi au karibu ya hapo nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI, yeye ni kwa saa moja kwa sababu mambo ni mengi na mwisho kabisa mtoa hoja Mheshimiwa Waziri Mkuu anayo mambo ya msingi tu ya kufafanua kwa hiyo kwa nusu saa naye, kwa mpangilio huo. Ndiyo! Ndivyo tulivyokubaliana. *(Makofi)*

Baada ya majibu yote hayo bado mnataka Waziri Mkuu aendelee tu kwa muda mrefu, basi saa sita na nusu au wakati kama unakaribia au saa sita na dakika thelathini na tano, tutaingia katika Kamati ya Matumizi, ikibidi tutaomba kutengua Kanuni tuendelee kidogo, tunadhani kwamba itachukua labda kipindi siyo kirefu sana.

Hii itawezesha saa 11.00 jioni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi aweze kusoma hotuba yake saa 11.00 jioni hiyo siku ya Jumatatu tarehe 2 Julai, 2207 na wengi wetu tunaisubiri kwa hamu, haswa wale tunaoishi kwa mishahara. Kwa uhalali tu wa mishahara, kwa sababu tunadhani siku hiyo kuna mambo mazuri yatatamkwa na basi tutaendelea kwa mtiririko huo kama ratiba ilivyoonyeshwa. *(Makofi)*

Nikumbushe tu kwamba kesho Waheshimiwa Wabunge tuna Semina ya *Unit Trust* ambayo itaanza saa tatu kamili katika Ukumbi wa Pius Msekwa, nyote mnakaribishwa. Ni muhimu sana na masuala mengi yanahusu uwekezaji, ujasiriamali na mfuko huu wa *Unit Trust* unavyofanya kazi yataelezwa. *(Makofi)*

Baada ya hapo muda wa kuahirisha Bunge umefika, kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi siku ya Jumatatu tarehe 2 Julai, 2007 saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 2 Julai, 2007 saa tatu asubuhi)*